

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Nne - Tarehe 1 Novemba, 2013

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona *Order Paper* yetu leo, kule mwisho kutakuwa na hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili mambo muhimu ya dharura. Mtakumbuka kuwa tarehe 30 Oktoba, 2013 Mheshimiwa Said Juma Nkumba na Mheshimiwa Alphaxard Lugola kwa kuzingatia Kanuni ya 47 na Kanuni ya 55 ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la 2013 waliomba Bunge liahirishe shughuli zake ili lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma.

Waheshimiwa Wabunge, uamuzi wangu katika hoja hizo mbili ulikuwa, Serikali ikazifanyie kazi na kuleta maelezo hapa Bungeni ili hatimaye Waheshimiwa Wabunge waweze kupata fursa ya kujadili. Hoja za Waheshimiwa hawa zilikuwa kama ifuatavyo:-

Hoja ya Mheshimiwa Said Nkumba ilijikita zaidi kwenye tatizo pana la migogoro kati ya wakulima na wafugaji, hifadhi, wawekezaji na watumiaji ardhi wengine.

Aidha, alionesha wasiwasi wake kuhusiana na operasheni mbalimbali nchini zinazosababisha adha na hasara mbalimbali kwa wakulima na wafugaji za kupoteza mifugo, mazao, kusababisha ulemavu, umasikini na kupoteza

[SPIKA]

maisha. Vilevile wasiwasi wake unatokana na kurudia zoezi la kuwaondoa wafugaji wakati Serikali ilisitisha zoezi hilo mwaka 2009 ili kufanya kazi kasoro zilizojitokeza wakati huo na ambazo bado nyingi hazikufanyiwa kazi na Serikali na sasa zoezi hili limeanza tena.

Kutokana na maelezo hayo, hoja ya Mheshimiwa Nkumba imejikita kwenye Sera ya matumizi ya ardhi kwa maana ya maeneo ya wakulima, wafugaji, hifadhi, wawekezaji na watumiaji wa ardhi nyingine. Hiyo ndiyo ilikuwa hoja ya Mheshimiwa Said Nkumba.

Hoja ya Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, ilijikita kwenye vitendo vinavyofanywa na watendaji katika operesheni iliyoanzishwa na Serikali ya kupambana na majangili, maalumu kama Operesheni Tokomezwa. Katika zoezi hili kumekuwepo na ukiukwaji wa haki za binadamu, uharibifu wa mali, mauaji ya ng'ombe, uporaji na dhuluma dhidi ya wafugaji.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Serikali kuwasilisha maelezo yake na kwa kuzingatia uzito wa hoja zote mbili nitatoa fursa kwa mujibu wa Kanuni ya 30(4)(h) ya Kanuni za Kudumu za Bunge ili Bunge liweze kujadili hoja hizo. Kwa maana hiyo ni kwamba baada ya kipindi cha maswali tutapewa taarifa nilizoagiza Serikali walete kwa hoja mbili tofauti halafu tutatoa na muda wa kujadili.

Vile vile wakati tutakapofikia nusu ya maswali, nitaomba Kamati ya Uongozi ya Bunge wote turudi nyuma kwenye *Speakers Lounge* tuweze kujadiliana baada ya mjadala wote mwishoni tunataka kiwe nini.

Kwa hiyo, nitawaomba mara baada ya kukabidhiana na Mheshimiwa Mwenyekiti hapa, Kamati ya Uongozi mtakwenda kwenye *Speakers Lounge* tupate muda mfupi tuweze kujadiliana hatma ya hoja ya kila mmoja tuone tunaimalizaje. Kwa hiyo, tunaendelea. Katibu.

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu atauliza swali la kwanza na kwa niaba yake Mheshimiwa Zedi.

Na. 39

**Huduma za Wataalamu na Dawa za Hospitali
za Amana, Temeke na Kinondoni**

MHE. CAPT. SELEMANI J. ZEDI (K.n.y. MHE. MUSSA A. ZUNGU) aliuliza:-

Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala - Kinondoni zimepandishwa hadhi na kuwa Hospitali za Mkoa lakini hazina wataalamu wala dawa, hivyo kuathiri huduma mbalimbali kama vile huduma za wazee na watoto.

Je, Serikali inasema nini juu ya changamoto hiyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Jimbo la Ilala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala iliyoko Wilaya ya Kinondoni zilipandishwa hadhi na Serikali na kuwa Hospitali za Rufaa za Mkoa na gazeti la Serikali *GN* namba 828 la tarehe 12/11/2010, kwa kifungu xxi (Amana) xxii (Mwananyamala) na xxiii (Temeke), na hivyo Serikali imeshazitambua kuwa na hadhi ya Hospitali za Rufaa za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi wa Afya, Serikali katika Hospitali ya Amana imeongeza Madaktari na Wauguzi kutoka watumishi 379 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia watumishi 396 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 sawa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)]*

na ongezeko la asilimia 16. Kwa upande wa Hospitali ya Mwananyamala, Madaktari na Wauguzi wameongezeka kutoka watumishi 488 hadi kufikia watumishi 501 kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Aidha, Hospitali ya Temeke imeongezewa Madaktari na Wauguzi kutoka watumishi 489 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia watumishi 527 kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Amana imeongezewa bajeti kwa ajili ya dawa na vifaa tiba kutoka Shilingi bilioni 1.2 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi Shilingi bilioni 3.0 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 60. Kwa upande wa Hospitali ya Mwananyamala, Serikali imeongeza bajeti kwa ajili ya dawa na vifaa tiba kutoka Shilingi bilioni 2.2 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia Shilingi bilioni 2.6 kwa mwaka wa fedha 2014/2014 ambapo ni ongezeko la wastani wa asilimia 11.8. Aidha, Hospitali ya Temeke imeongezewa pia bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba kutoka Shilingi bilioni 6.6 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia Shilingi bilioni 8.5 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 sawa na ongezeko la asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, wazee wote wanatakiwa kutibiwa bure na kwamba kila Halmashauri inatakiwa kuwapa vitambulisho pamoja na kutenga dirisha maalumu kwa ajili ya matibabu ya wazee wetu.

Napenda kutumia fursa hii kuzikumbusha tena Halmashauri zote nchini kutekeleza matakwa haya ya Kisera. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Zedi, swali la nyongeza.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa na swali moja la nyongeza. Nilitaka kujua, kwasababu karibu hospitali zote zenye hadhi ya Mikoa ikiwemo Hospitali ya Kitete ambayo ni Hospitali ya Mkoa wa Tabora, kuna tatizo kubwa la upungufu wa watalaamu, upungufu wa vifaa tiba

[MHE. S. J. ZEDI]

na upungufu wa madawa. Nilitaka kujua kama Serikali ina mpango mkakati maalumu wa kuhakikisha kwamba baada ya kipindi fulani kwa kiwango kikubwa angalau 80% au 90% matatizo haya yatakuwa yamepungua. Kwasababu bila kuwa na mpango mkakati, tutakuwa tunafanya kazi ya Zimamoto. Sasa nataka kujua kama Serikali ina mpango huo mahususi wa kuhakikisha kuwa tatizo la madawa, vifaa tiba na wataalamu katika hospitali zote zenye hadhi ya Mikoa linafanyiwa kazi kwa kipindi maalumu.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Afya.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, mpango mkakati maalum wa kupunguza tatizo la uhaba wa wataalam katika hospitali zetu upo. Tumeongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa kwenye Vyuo vya Afya, sasa hivi tumefikia wanafunzi 7,000 kwa mwaka. Lengo ni kufika wanafunzi 10,000 tukifika mwaka 2015. Hiyo ninazungumzia kwa upande wa Serikali, lakini bado Serikali inasaidia Vyuo vya Watu Binafsi na Vyuo vya Mashirika ya Dini ili na wenyewe waweze kuongeza udahili tupate wataalamu wengi zaidi, na baada ya kuwazalisha wataalam hawa, Serikali imekuwa ikiongeza idadi ya vibali vya ajira mwaka hadi mwaka ili hatimaye tuweze kupunguza uhaba mkubwa ambao sasa hivi unakadiriwa kuwa zaidi ya 43% nchi nzima katika vituo vyote. Kwa hiyo, huo ndiyo mpango maalumu kwa upande wa uzalishaji na uajiri wa wataalam.

Kuhusu dawa na vifaa tiba kama swali la msingi lilivyojibu, kila mara kila mwaka tunaongeza bajeti ya dawa na vifaa tiba katika hospitali zote mwaka hadi mwaka. Lakini tunatambua kuwa bajeti hizo bado hazikidhi haja ndiyo maana tukaweka Mfuko Maalum; Mfuko wa Bima ya Afya pamoja na Mfuko wa Afya ya Jamii. Endapo fedha zitakusanywa vizuri na kutumika vizuri kwa ajili ya kwa ajili ya kununua dawa za ziada, tatizo hili la dawa litapungua. Tatizo tunaloliona mpaka sasa ni kwamba bado fedha hizi hazitumiki au hazikusanywi na kutumika inavyotakiwa. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tushirikiane katika hili tuhakikishe kwamba fedha hizo zinakusanywa na zinatumiwa kupunguza

[WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII]

uhaba wa vitendea kazi pamoja na madawa katika Zahanati zetu na hospitali kwa ujumla. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Rita Mlaki.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ambao watu wanaoishi pale pamoja na wale wanaokuja kutembea wanakadiriwa kufika milioni tano na zaidi kwa siku na wakiugua wote wanakumbilia hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala: Je, Serikali itakuwa tayari kwa kupitia Serikali Kuu ama Halmashauri zake kuwasomesha na kuwalipia wanafunzi wa *private* ambao wako tayari na wameshaanza Vyuo lakini wanakosa malipo? Ningeomba tamko la Waziri kama Chuo cha *IMTU* ambacho kiko tayari na wanafunzi wanashindwa kulipa na kipo tayari kuwasomesha madaktari?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inasomesha wanafunzi katika Vyuo vya Serikali na Binafsi kwa upande wa Madaktari wa Shahada ya kwanza kwa maana kwamba kwenye Vyuo ambavyo viko chini ya Wizara ya Afya, zaidi ya wanafunzi 13,000 wanalipwa na Serikali hivi sasa. Kwenye Vyuo vinavyotoa shahada ya kwanza kikiwemo cha *IMTU* na vinginevyo, Serikali inawasomesha kupitia ule Mfuko wa Mikopo kwa Wanafunzi.

Tatizo tunalitambua kwamba fedha hizo hazitoshi, wako wengi sana ambao bado hawapati mikopo hiyo. Lakini kadri siku zinavyokwenda, Serikali inaongeza bajeti ya mfuko huo, na sasa hivi kama tulivyoambiwa, kuna mpango maalum wa kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanapata *admission* katika Vyuo vinavyofundisha udaktari, waweze kupata mikopo ya Serikali. Hilo linaendelea kufanyiwa kazi.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Gekul atauliza swali hilo.

Na. 40

**Kukamilika kwa Ujenzi wa Hospitali ya
Mkoa wa Manyara**

MHE. PAULINE P. GEKUL aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Manyara imeanza kujengwa muda mrefu na mpaka sasa bado haijakamilika:-

- (a) Je, ni tatizo gani linasababisha hospitali hiyo isikamilike?
- (b) Je, hospitali hiyo itaanza kutumika lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA
MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara ilianza kujengwa mwezi Novemba, 2009 baada ya maandalizi ya awali ya kupata eneo, kulipa fidia, kuandaa michoro na mkandarasi kupatikana na mkataba kusainiwa. Gharama za kujenga majengo yote ya hospitali zilikadiriwa kufikia Shilingi bilioni 16.5 (kwa bei za mwaka 2008/2009). Majengo hayo ni pamoja na wodi ya wazazi (*martenity ward*), wodi ya wagonjwa wa nje (*OPD*) ikiwa pia ni ofisi za Utawala, jengo la kufulia (*laundry*), jengo la kuhifadhia maiti (*mortuary*), jengo la maabara na tanuru la kuchomea taka (*incinerator*).

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha ujenzi wa hospitali, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka ili kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo. Mpaka sasa Serikali imekwishatoa jumla ya Shilingi bilioni 5.7 kati ya Shilingi 8.5 zilizoidhinishwa tangu kuanza kwa mradi mpaka sasa, sawa na asilimia 66. Fedha zilizotolewa kila mwaka ni kama ifuatavyo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)]

Mwaka 2008/2009 Shilingi bilioni mbili, 2009/2010 Shilingi bilioni 1.9, mwaka wa fedha 2010/2011 Shilingi milioni 650, mwaka wa fedha 2011/2012 Shilingi 391, mwaka wa fedha 2012/2013 Shilingi milioni 700 na mwaka wa fedha 2013/2014 zimetengwa Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, majengo ambayo yameshajengwa hivi sasa ni pamoja na wodi ya wazazi ambayo ina sehemu za wodi ya kusubiria wagonjwa, wodi ya kujifungulia (*Delivery wards*), chumba cha upasuaji mdogo (*Mini Theatre*), wodi ya waliokwisha kujifungua (*Post Natal*), wodi ya watoto njiti (*Neonatal wards*), wodi ya akinamama wenye matatizo baada ya kujifungua, Kliniki ya Watoto, wodi ya watoto wenye magonjwa ya kuambukiza (*Isolation Children wards*), vyumba vya madaktari (*Consultation rooms*), jengo la maabara, wodi ya wagonjwa wa nje (msingi na nguzo – *columns*), jengo la kuhifadhia maiti (*mortuary*), jengo la kufulia (*laundry*) na uzio wake pia. Maeneo yote yameshajengwa.

(b) Mheshimiwa Spika, hospitali imeanza kutoa huduma kwa kutumia majengo ya wodi ya wazazi ambayo yamekamilika. Vitengo ambavyo vimeanza kazi ni vya Kliniki ya Macho, Kliniki ya afya ya Kinywa na Meno, Kliniki ya Kisukari na Magonjwa ya Moyo, Kliniki ya Kifua Kikuu, Ukoma na Ngozi, Kliniki ya Ushauri Nasaha na Upimaji wa Virusi vya UKIMWI.

SPIKA: Mheshimiwa Gekul, swali la nyongeza.

MHE.PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa makubaliano ya awali ni kwamba Serikali ingekuwa inatoa Shilingi bilioni mbili kwa kila mwaka wa bajeti ili hospitali hii ikamilike ndani ya mika nane kwa bajeti ya Shilingi bilioni 16; na kwa kuwa hadi sasa tunavyoongea Serikali ina deni la Shilingi bilioni 2.8 kwa kutopeleka fedha hizo kila mwaka; na kwa kuwa

[MHE. P. P. GEKUL]

makandarasi wameshaondoka kwenye *site*, naomba nifahamu: Serikali iko tayari kulipa deni hili la Shilingi bilioni 2.8 ili makandarasi hawa warudi kwenye *site* na ujenzi uendelee?

Swali la pili, nawapongeza Madaktari wa Mkoa wa Manyara ambao wanafanya kazi katika hospitali hii waliojitolea *on call allowance* zao zaidi ya Shilingi milioni 100 kwa ajili ya kununua vifaa tiba na mahitaji mengine ili hospitali hiyo ianze; na kwa kuwa jengo la *mortuary* halijakamilika kitu ambacho...

SPIKA: Eeeh, Mheshimiwa uwe *precise* eh! Uwe *precise* maswali yako mawili, Haya endelea.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nirudie swali la pili. Kwa kuwa, Madaktari wa Mkoa wa Manyara walijitolea zaidi ya Shilingi milioni 100 fedha ambazo zilikuwa ni za *on call allowance* zao kwa ajili ya kununua vifaa tiba; na kwa kuwa, wameshindwa sasa kuendelea na operasheni hii ya hospitali kwasababu jengo la *mortuary* halina umeme, na tangu mwezi wa Tano limeshapelekewa majokofu, naomba nifahamu: Serikali ipo tayari kupeleka fedha kiasi cha bilioni 1.4, ambazo zilitengwa katika mwaka huu wa bajeti ili fedha hizo za kuweka umeme katika jengo hilo la *mortuary* zipatikane haraka na operesheni iendelee?

SPIKA: Ukiuliza maswali marefu utajibiwa ovyo, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa maelezo ambayo Mheshimiwa Mbunge, ameeleza kwamba hospitali bado ina deni na Mzabuni na Mkandarasi ameshatoka kazini, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba kazi ambayo tunaikusudia inafanywa. Kwa kuwa sasa tuna deni hili la kumlipa Mkandarasi ili aweze kuendelea na kazi yake; na kama ambavyo nimeeleza kwenye jibu la msingi, ni kwamba Serikali inaendelea na utaratibu wa kuhakikisha hospitali hii inakamilika, na fedha ambazo tumezitenga zitaendelea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)]

kutolewa kadiri zinavyopatikana ikiwemo na deni ambalo lipo, ni sehemu ya kazi ambayo tayari ameifanya na ni sehemu ya makadirio ambayo tulikuwa tumeshayakadiria.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, nami pia niungane na Mheshimiwa Mbunge kwa kuwapongeza Madaktari hao kama kweli waliweza kufanya yale ambayo ameyaeleza kwa kutoa fedha zao kwa ajili ya kuweza kuhakikisha kwamba shughuli zote zilizokadiriwa eneo lile zinakamilika. Wajibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba vifaa tiba vinapatikana na huduma inatolewa ili wagonjwa waweze kupata huduma hiyo. Kwa hiyo, hii ni pamoja na yale yote yanayotakiwa kukamilishwa ili shughuli ziweze kuanza, tutaweza kufanya hivyo ili kuhakikisha huduma inaendelea kutolewa.

SPIKA: Mheshimiwa Shekifu, swali lingine la nyongeza.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, naomba kutangaza *interest* kwamba nilikuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara kipindi hospitali inaanza kujengwa. Nina swali moja la nyongeza la kiseri.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ilipoamua kuanza kujenga hizi hospitali za Mkoa hasa hii ya Manyara, ni kweli ilihaidi Shilingi bilioni mbili za kujenga hospitali hii kwa miaka nane; na kwa sasa Sera inataka kuwepo na Hospitali ya Rufaa kila Mkoa, na imeongeza Mikoa minne. Serikali ina mkakati gani wa dhahiri ambao sasa hivi tupo katika kufanya mipango, kuhakikisha Hospitali za Mikoa katika Mikoa mipya zinaanza na zinajengwa kwa wakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Mimi pia nina Mkoa mpya.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba katika kila Mkoa tunakuwa na Hospitali ya Mkoa inayokidhi mahitaji kama Rufaa ya Hospitali zetu za Wilaya zilizoko katika Mkoa huo ili ziweze kutoa huduma na kupunguza idadi ya wagonjwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*[NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA
NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)]*

ambao wanalundikana sana kwenye Hospitali za Rufaa kama Muhimbili na Bugando na Mikoa mingine. Sasa tunayo hii Mikoa mipya kama ambavyo hata Mheshimiwa Spika amesema kwamba hata kule kwake Njombe nako pia tayari ni Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba hata Mikoa Mipya nayo inajengewa. Kwa hiyo, tunachofanya ni kuhakikisha kwamba tunajitahidi kuongeza bajeti za kutosha ili tuweze kukamilisha hospitali ambazo tumeanza, na kuanza majengo mapya kwenye maeneo ya Mikoa mipya ili kuimarisha eneo la uwepo wa Hospitali za Mikoa kama Hospitali za Rufaa za Wilaya zake ndani ya Mkoa husika. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango wa Serikali upo wa kuimarisha hospitali zinazoendelea kujengwa, na kuanzisha miradi mipya pindi tutakapopata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwa na Hospital za Mikoa zinazofanya kazi inayokusudiwa.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa, naomba tuendeleo na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Innocent Kalogaris atauliza swali hilo.

Na. 41

Vituo Visivyo Rasmi vya Ukaguzi Barabarani

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS aliuliza:-

Kumekuwa na vituo visivyo rasmi vya ukaguzi wa Polisi, TRA na biashara ndogo ndogo katika Barabara Kuu zote nchini hali inayosababisha ucheleweshaji usio wa lazima wa abiria, madereva, mizigo na wafanyabiashara; Vituo hivyo pia vimekuwa vikisababisha uharibifu mkubwa wa barabara unaolazimu Serikali kuendelea kutenga fungu kwa ajili ya matengenezo yasiyo ya lazima.

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya uharibifu huo unaogharimu pesa nyingi kila mwaka?

[MHE. I. E. KALOGERIS]

(b) Je, ni lini Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi, Mambo ya Ndani ya Nchi na Fedha zitaangalia uwezekano wa kuwa na vituo vya pamoja (*One Stop Centre*) katika maeneo maalum katika barabara kuu zote nchini ili kupunguza usumbufu kwa wasafiri na mizigo na uharibifu wa barabara?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mbunge wa Morogoro Kusini, lenye sehemu (a) and (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Usalama Barabarani Na. 30 ya mwaka 1973 (*The Road Traffic Act 1973*), Sheria ya Usalama Barabarani Sura ya 168 ya mwaka 2002 (*The Road Act Cap. No.168*) pamoja na kanuni za Usalama Barabarani za mwaka 2001 [*The Road Traffic (Maximum Weight of Vehicles) Regulations, 2001*], Wizara imeendelea kujenga vituo vya mizani ili kulinda barabara zetu nchini. Mpaka sasa kuna vituo vya mizani vya kudumu 24 na vya mizani ya kuhamishika 17.

Mheshimiwa Spika, ili kurahisisha usafirishaji na biashara kati ya Tanzania na nchi jirani, Serikali inajenga vituo vya kutoa huduma kwa pamoja, mipakani (*One Stop Border Posts*). Vituo hivyo ni Mutukula (Tanzania/Uganda); Tunduma (Tanzania/Zambia); Namanga (Tanzania/Kenya), Rusumo (Tanzania/Rwanda), Holili (Tanzania/Kenya), Horohoro (Tanzania/Kenya), Sirari (Tanzania/Kenya), Kabanga (Tanzania/Burundi) na Kasulumu (Tanzania/Malawi).

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi wa vituo vya mizani, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine inajenga vituo vya pamoja vya ukaguzi *One Stop Inspection Stations* kwenye maeneo mbalimbali katika barabara kuu ili kurahisisha usafirishaji na biashara. Kwenye barabara za ukanda wa kati, kutoka Dar-es-salaam kupitia Dodoma, Isaka hadi Rusumo vituo vitatu vinategemewa kujengwa katika maeneo ya Vigwaza, Manyoni na Nyakanazi.

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kupitia mradi wa *Southern Africa Trade and Transport Facilitation Project (SATTFP)* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, vituo viwili vya ukaguzi wa pamoja *One Stop Inspeccion Stations* vinatarajiwa kujengwa kati ya Morogoro na Tunduma/Kasumulu na kufanya vituo vya ukaguzi wa pamoja kwenye barabara ya Ukanda wa Dar es Salaam kuwa vitatu kikiwemo pia kituo cha Vigwaza. Vile vile kwa kupitia mradi huu wa *SATTFP*, Dola za kimarekani milioni moja zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa magari ya Jeshi la Polisi kwa ajili ya *Patrol* kwenye barabara ya Dar es Salaam – Tunduma – Kasumulo na hivyo kupunguza baadhi ya vizuizi barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo Serikali italinda barabara zake inazojenga kwa gharama kubwa, lakini pia kuhatarisha biashara ndani na nje ya nchi.

SPIKA: Ahsante. Swali la nyongeza, Mheshimiwa Kalogeris.

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Serikali nadhani nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la utekelezaji wa Serikali ni la muda mrefu kwasababu linahitaji upatikanaji wa fedha. Je, wakati Serikali inasubiri upatikanaji wa fedha au ujenzi wa vituo hivyo, Wizara haioni muhimu katika kulinda barabara zake kwa sasa kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani, Fedha na Uchukuzi; kukaa kwa pamoja kutenga maeneo maalum, katika Mkoa kwa barabara zote kuu za Mikoa, ambazo zitaweza kuhimili magari kupaki na kuzuia kuleta uharibifu wa barabara zetu, mfano Chalinze, Morogoro, Dumila Dodoma, Mikumi na Ruaha?

Pili, je, kuna sheria yoyote ambayo ipo ambayo pengine kwa namna moja au nyingine inamruhusu Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa kuweza Kupiga faini au kudhibiti uharibifu wowote unaotokea katika Mkoa wake? Kama ipo tungependa tuijue, na kama haipo, kwa nini isije ili

[MHE. I. E. KALOGERIS]

tuweze kuhimili kutunza barabara zetu badala ya kwenda kuwaachia mapolisi, wanajificha pembeni, wanachukua...

SPIKA: Mheshimiwa, maswali yawe mafupi jamani! Yanakuwa marefu, inakuwa hotuba!

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Kalogeris kwa kuliona hili. Kweli ni dhamira ya Serikali kwamba vituo hivi ambavyo tumeviweka ni kwa nia nzuri, siyo kwa nia mbaya. Tunahitaji kulinda barabara zetu na ndiyo maana kwenye Sheria ya Barabara, ipo kwenye kanuni, kwamba magari haya kwa mfano yanapaki mahali halafu yanamwaga *oil*, kwenye sheria ni kwamba wamevunja Sheria. Kwa hiyo, kwenye kanuni ipo na wanapewa adhabu kama Mheshimiwa Kalogeris alivyosema. Mameneja wa *TANROADS* wanayo mamlaka ya kutoza adhabu kwa watu wanaovunja sheria kwa maana kwamba kama umepaki ama gari limeharibika na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kwa hiyo, masuala ya kukaa pamoja kati ya Jeshi la Polisi na Uhamiaji, Serikali ni moja. Haya mambo tunayafanya, tumekuwa tunawasiliana mara kwa mara kuweza kuboresha. Ni vitu vipi katika vituo hivi inatakiwa viwe vinakaguliwa. Sio kwamba unaweka tu kizuizi kwa maana ya kuweka kizuizi, lazima kuwe na dhamira maalumu kwa ajili yakuendeleza nchi hii. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Sakaya.

MHE.MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushuru kwa kuweza kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa *traffic Police* wamekuwa wakisimamisha magari katikati ya barabara kwenye vituo ambavyo siyo rasmi na kusababisha adha kubwa kwa vyombo vya usafiri, pamoja na kwa abiria pia, na wakati mwingine kwenye maeneo hayo kunatokea ajali, au msururu wa magari mahali ambapo magari hayana sehemu ya kuegushwa.

[MHE. M. H. SAKAYA]

Je, Serikali sasa ipo tayari kutoa agizo kwa *Traffic Police*, kusimamisha magari maeneo ambayo kuna uwezekano wa kuegesha magari badala ya kusimamisha magari katikati ambayo yanaleta usumbufu mkubwa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nadhani siyo sahihi *Traffic Police* kusimamisha magari mahali ambapo inaleta athari nyingine kwa mfano, kusababisha ajali. Naagiza kwamba Polisi wote waangalie hilo. Mahali ambapo wanasimamisha magari wawe wanameangalia kwamba usalama wa wanaotumia barabara unakuwepo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Chilagati, swali la nyongeza.

MHE JOHN Z. CHILAGATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri kwenye jibu la msingi, ameeleza Bunge hili kwamba ili kupunguza usumbufu wa magari ya Mizigo kusimamishwa kila mahali, Serikali imeweka vituo vitatu vya ukaguzi wa magari haya, na ametaja Vigaza, Manyoni na Nyakanazi. Kwakuwa pale Manyoni sijaanza kuona harakati ya mchakato wa ujenzi wa kituo hicho, nataka kujua tu, huo ujenzi utanza lini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, nimesema Serikali inao mpango. Kwa hiyo, ipo kwenye mchakato, kwanza kufanya maandalizi ili tuweze kujenge vituo hivi. Kwa hiyo, tupo katika zile hatua za awali. Tutakapokuwa tayari, basi Mheshimiwa Mbunge tutakujulisha.

SPIKA: Ahsante. Tuendeleo na swali linalofuata, Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe.

MHE.DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, naomba nifanye marekebisho. Kile kijiji cha mwisho ni Kijiji cha Lwilo siyo Kijiji cha Luto. Baada ya marekebisho hayo machache, naomba nipate majibu ya swali hilo.

Na. 42

Ujenzi wa Daraja la Ruhuhu

MHE.DEO H. FILIKUNJOMBE aliuliza:-

Daraja la Mto Ruhuhu ni muhimu sana kwa wananchi wa Ludewa, Manda, Masasi na Lwilo.

Je, ujenzi wa daraja hilo utanza na kukamilika lini?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kukujibu swali la Mheshimiwa Deo Haule Fulikunjombe, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi ilianza maandalizi kwa ajili ya usanifu wa daraja la Mto Ruhuhu mwaka 2009/2010. Kufuatia kuanza kwa zoezi hili, Wizara ya Maji ilitoa pendekezo la kuunganisha nguvu ili kujenga *structure* moja itakayotumika kama Daraja na wakati huo huo kama Bwawa litavyotumika kuboresha shughuli za umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya mapendekezo hayo, mnamo mwezi Agosti, 2010 Kikosi Kazi cha wataalam toka Wizara ya Ujenzi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Maji na Kilimo, Chakula na Ushirika kiliundwa ili kushughulikia suala hili. Kikosi Kazi hiki kiliendelea na kazi ya kuandaa hadidu za rejea pamoja na kabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandishi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu.

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Mheshimiwa Spika, wakati nyaraka za upembuzi yakinifu na usanifu zanaandaliwa, mradi huu ulionekana kuwavutia Washirika wa Maendeleo na mwaka 2013. *Department of International Development Facility (DFID)* kupitia Shirika la *Climate Resilient Infrastructure Development Facility (CRIDF)* walijitokeza kuufadhili mradi huu. Hivi sasa wataalamu wa Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Chakula na Ushirika na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wanaendelea na kukamilisha na majadiliano na *CRIDF* ili itekeleze mradi huu kwa ufadhili wa *DFID*.

Hizi ni jitihada za Serikali kupata fedha za kugharamia mradi huo mkubwa wa kutatua matatizo wanayowakabili wananchi wa Ludewa, Manda, Masasi na Lwilo. Katika kuchangia gharama za awali za mradi, Wizara ya Ujenzi, imetenga Shilingi milioni 200 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Filikunjombe, maswali ya nyongeza.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, kwakuwa ujenzi wa daraja la Ruhuhu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais Kikwete kupunguza adha ya usafiri kwa wananchi wa Mbinga, na Ludewa; naomba Mheshimiwa Waziri alithibitishie Bunge hili, atoe kauli thabiti katika mambo mawili yafuatayo:-

(1) Je, ujenzi wa daraja utaanza lini?

(2) Daraja hili litakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante kwa maswali mafupi. Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli daraja hili ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ndiyo maana Serikali imeshaanza kushughulikia kufanya upembuzi sanifu na usanifu

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

wa daraja hili. Kwa sasa hivi siwezi kusema lini utaanza kwasababu kwanza kazi ya usanifu lazima ikamilike. Ni lazima tujue gharama ya mradi huu ndio sasa tunaweza kupata Mkandarasi wa kujenga hii. Sasa ndani ya kandarasi ndiyo tutajua ujenzi utachukua muda gani.

SPIKA: Mheshimiwa Mhagama, swali lingine la nyongeza.

JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Ujenzi wa Daraja hilo kama alivyosema Mheshimiwa Deo Filikunjombe, utachochea maendeleo ya Mkoa wa Ruvuma na Mkoa Njombe kupitia Ludewa. Lakini utachochea pia azma ya Serikali na agizo la Mheshimiwa Rais la kujenga barabara ya lami kutoka Ludewa makaa ya mawe Liganga lakini kufikia Kijiji cha Mahanjo, Jimbo la Peramiho mpaka Madaba Jimbo la Peramiho: Je, shughuli hiyo nayo inakwenda sambamba pamoja na Ujenzi wa Daraja hilo kama ilivyokuwa imepangwa toka awali?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna uwekezaji mkubwa unaotarajia kuanza mwezi Januari, 2014, kwa maana ya mchuchuma pale pale Liganga. Ni kweli kwamba wakishamaliza uwekezaji ule, tutahitaji kupeleka chuma kile kwenye soko; na tunahitaji tujenge barabara ya lami. Serikali imeshatambua hilo na inajipanga kuweza kuangalia namna ya kufanya usanifu wa barabara inayotoka Ludewa - Liganga mpaka Madaba kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa John Damiano Komba, swali lingine la nyongeza.

MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Mwaka mmoja na nusu uliopita Mheshimiwa Rais alisema kwamba daraja hili ni muhimu sana. Aliwaambia Wizara hiyo na Waziri aliyekuwa anajieleza hapa alikuwepo;

[MHE. J. D. KOMBA]

kwamba pale wanapokwama wamfwate na atawasaidia mara moja. Wamemfuata? (*Kicheko*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu; umemfuata? Ndiyo au hapana jamani! (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais anafuatilia kwa karibu Ujenzi wa Daraja hili, ndiyo maana kwenye jibu la msingi tunasema tayari, kuna *commitment* ya wafadhili ambao wako tayari kuufadhili mradi huu mkubwa. Kwa hiyo, kazi hiyo itafanyika kama vile Mheshimiwa Rais alivyoagiza.

SPIKA: Kwa hiyo, ulimfuata! (*Kicheko*)

Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria na Mheshimiwa Kibona atajibu swali hilo. Hongera kwa kumaliza somo la *Masters Degree*, nakutakia uendelee zaidi.

Na. 43

Wilaya ya Ileje Kutokuwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya

MHE. ALIKO N. KIBONA aliuliza:-

Wilaya ya Ileje kwa muda mrefu haina Hakimu wa Mahakama ya Wilaya, hali inayolazimu Hakimu kutoka Wilaya ya Mbozi kupanga kalenda ya kwanda kusikiliza kesi katika Wilaya ya Ileje na kurudi Mbozi:-

(a) Je, ni lini Serikali itarejesha huduma za Mahakama Wilayani Ileje ili kuwaondolea kero wananchi wake?

(b) Je, Serikali iko tayari kulirudisha gari lililopangiwa kuhudumia Mahakama ya Wilaya ya Ileje na baadaye kurudishwa Mkoani kwa kisingizio kwamba Ileje hakuna kazi zinazohitaji gari?

[MHE. A. N. KIBONA]

(c) Kwa uamuzi wa kuondolewa Mahakama na Hakimu wa Wilaya, pamoja na gari katika Wilaya hii: Je, Serikali haioni kuwa wananchi hao wamedhalilishwa na kufanya wajisikie kuwa wanakosa sifa za kuwa Wilaya?

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona, Mbunge wa Ileje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama ya Wilaya ya Ileje hapo mwanzo ilikuwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya kuanzia Februari 2010 hadi Februari 2011. Hakimu huyo aliyekuwepo hapo awali baadaye alikwenda kujiendeleza kimasomo na tangu hapo hajapelekwa Hakimu mwingine na hii ni kutokana na uhaba wa Mahakimu Wakazi. Hata hivyo, hivi sasa wapo Mahakimu 70 ambao watapangwa upya katika vituo vya Mahakama za Wilaya, na Mahakama ya Wilaya ya Ileje nayo pia itapangiwa Hakimu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Serikali italirudisha gari lililopangiwa katika Mahakama ya Wilaya ya Ileje pindi atakapoteuliwa Hakimu wa Wilaya hiyo. Gari lililokuwepo awali kwa ajili ya Mahakama ya Wilaya ya Ileje liliondolewa na kupelekwa Mkoani baada ya kuthibitika kwamba gari hilo lilikuwa linatumika visivyo na walioachiwa baada ya Hakimu wa Wilaya aliyekuwepo kuondoka.

Mheshimiwa Spika, siyo dhamira ya Serikali kuwadhalilisha wananchi wake kwa hali yeyote ile, lakini kutokana na sababu zisizozuilika, Hakimu wa Mahakama ya Wilaya alikwenda masomoni na gari la Mahakama lilitumiwa vibaya baada ya kiongozi huyo wa Mahakama kuondoka na hii ndiyo ilisababisha hali hiyo kutokea. Vile vile niseme tu kwamba kutokuwepo kwa Hakimu wa Wilaya na kutokuwepo kwa gari kwa hivi sasa haiwezi kuikoshesha Wilaya ya Ileje sifa ya kuwa Wilaya na kuwafanya wananchi wake kujisikia kwamba Wilaya yao haina sifa ya kuwa Wilaya.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kibona, swali la nyongeza.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja tu la nyongeza. Kusema kweli majibu ya Serikali yameniridhisha, lakini niulize kwamba, pamoja na mambo mengine, sababu zinazowafanya Watumishi hasa wa Mahakama, Walimu na wengine kutokuripoti kwenye maeneo waliyopangiwa ni ukosefu wa miundombinu hasa majengo na vitendeakazi vingine. Je, Serikali imejiandaa vipi kukarabati Mahakama nyingi ambazo zipo katika hali mbaya ili wale watakaopangiwa wasiweze kukosa kuripoti maeneo hayo na kukaa kwa usalama? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda tu kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mahakama imejipanga vilivyo na ni mpango wa Mahakama kukarabati Mahakama zote zilizochakaa, lakini mara nyingi imekuwa kasi inakwenda kidogo kutokana na ufinyu wa bajeti. Lakini siyo kukarabati tu, tunao mpango pia wa kujenga Mahakama mpya kwa sehemu ambazo hazipo lakini pia kwa sehemu ambazo kuna majengo ya Mahakama ambayo yamechakaa kabisa na hayawezi kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha tunatarajia kujenga Mahakama mpya za Wilaya sita; Mahakama ya Bariadi, Mahakama ya Bagamoyo, Mahakama ya Bukombe, Kilindi, Nkansi, lakini pia tunatarajia kujenga Mahakama za Mwanzo 12.

Hivyo basi, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba tunakarabati na kujenga Mahakama zote ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika Majibu ya nyongeza, Mheshimiwa Waziri amezungumzia juu ya ujenzi wa Mahakama, na Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka kwamba kati ya Mahakama ambazo zimekuwa zikitolewa ahadi katika miaka mitatu ya fedha mfululizo ni Mahakama ya Kawe. Sasa yeye akiwa kama mkazi wa Jimbo la Kawe, mwananchi wangu; nilitaka aniambie: sasa hivi ujenzi wa Mahakama ya Kawe umefikia kiwango gani? Kwa sababu hizi *sound* wameshazipiga sana kwa miaka mitatu. Sasa nataka aniambie ujenzi huo umefikia kiwango gani?

SPIKA: Wewe uliona umefikia kiwango gani? Naibu Waziri, majibu. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge wangu na mimi pia mkazi wake na huenda nikagombea huko. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ujenzi wa jengo la Mahakama ya Kawe, napenda tu kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalipa kipaumbele tena na yeye mwenyewe amesisitiza kwamba na mimi ni mkazi wa huko, kwa hiyo, nalifuatilia kwa karibu sana na tayari kwa taarifa nilizonazo msingi tayari umeshawekwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa utekelezaji wa Serikali kuhusu ahadi za Wabunge ni kufuatana na ni yupi alianza kupeleka maombi; kwa kuwa tulishapata ahadi ya kujengewa Mahakama ya Wilaya ya Iramba na Manyoni toke enzi ya Mheshimiwa Mary Nagu, lakini mpaka sasa hivi utekelezaji haupo: Je, Naibu Waziri atakuwa tayari kukiri kwamba sasa kipaumbele kitatolewa kwa Wilaya hizi kwa sababu ahadi ni ya miaka mingi mno? (*Makofi*)

SPIKA: Hizo zote ni mpya tu. Mahakama hata mimi nahitaji. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba huko nyuma Serikali iliahidi kujenga Mahakama ya Wilaya ya Iramba pamoja na Manyoni, lakini kutokana na hali ya kifedha ndiyo maana tumeshindwa kuwa katika nafasi ya kufanya hivyo. Lakini napenda tu kusema kwamba, katika mwaka ujao wa fedha 2014/2015 tunaiahidi Wilaya ya Iramba tutawajengea Mahakama ya Wilaya ya Iramba.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

Na. 44

Mafao ya Askari Polisi

MHE. RASHID ALI ABDALLAH (K. n. y. MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA) aliuliza:-

Je, ni Askari wangapi wa Jeshi la Polisi ambao bado wanadai mafao yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpaka kufikia Juni, 2013 jumla ya Askari 629 walikuwa hawajalipwa mafao yao. Madai hayo yanajumuisha malipo ya kumaliza mikataba, waliostaafu kwa lazima, madai ya mirathi na fidia za kuumia au kufariki kazini.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa kulipwa kwa madai kama haya, husababishwa pamoja na mambo mengine na ufinyu wa bajeti, kukosekana kwa baadhi ya nyaraka na taratibu za uhakiki.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI]

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kulipa mafao ya Askari kwa haraka ili kukidhi madhumuni ya mafao hayo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, swali la nyongeza.

MHE. RASHID ALI ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, madai haya ni ya Askari 629. Kati ya Askari hao ni wale ambao wamestaafu, waliofariki na wale walioumia kazini. Askari hawa walifanya kazi nzito ya kulinda Usalama wa Taifa letu, leo hii familia za Askari hawa wanateseka na matatizo na wale walio hai wanadhalilika. Mheshimiwa Naibu Waziri atueleze, ana mpango gani wa haraka wa kuweza kuwalipa mafao wanaohusika kwa haraka sana?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, idadi ya Askari 629 tayari ni idadi ndogo kuliko idadi ambayo ilikuwepo mwanzo. Jitihada kubwa zinafanyika kuhakikisha kwamba idadi hii inapungua na hatimaye kila mstaafu au anayepata ajali alipwe mara baada ya kutokea hicho kitendo.

Mheshimiwa Spika, ninachomhakikisha Mbunge ni kwamba kuna changamoto ambazo huwa zinachelewesha malipo hayo ambazo Wizara yangu pamoja na taasisi nyingine husika tunazishughulikia na kupitia hizo, basi tuna hakika kwamba tutakuwa na uharaka wa kulipa kuliko ilivyo sasa.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Machali, swali la nyongeza.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali moja dogo la nyongeza. Askari wengi waliostaafu hasa wa Jeshi la Polisi wakiwemo wanaopatikana katika Jimbo langu la Kasulu Mjini, wanalalamika sana hivi sasa na wanaendelea kunitumia meseji, wanacheleweshewa sana kulipwa mafao yao kila baada ya miezi mitatu. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na usumbufu huu ambao wanaupata wastaafu hawa ambao wanalipwa kupitia Mfuko wa *GEPP*?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa mwelekeo wa swali ni kwamba wanaochelewesha ni Taasisi za Kijamii, zile ambazo zinasimamia utoaji wa mafao na baada ya miezi mitatu *in fact*, ni taratibu ambayo tulikubaliana walipwe. Kama kuna watu ambao hawapati mafao yao kila baada ya miezi mitatu, naomba tuwasiliane na Taasisi zinazohusika hasa Mifuko ya Jamii au Wizara ya Fedha kwa maana ya Hazina, ili tuhakikishe kwamba wanalipwa kwa wakati.

SPIKA: Ahsante. Naomba tuendeleo na swali linalofuata. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza atauliza swali hilo. Mheshimiwa Leticia kwa niaba yake.

Na. 45

Kufanya Ukarabati wa Bandari na Meli

MHE. LETICIA M. NYERERE (K.n.y. MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA) aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Bandari za Mwanza na Kemondo ili ziweze kulingana na hadhi yake?

(b) Je, ni lini meli ya MV. Victoria itafanyiwa ukarabati?

SPIKA: Wenyeviti wa Kamati za Bunge Kamati ya Uongozi naomba mwende *Speaker's Lounge* sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mchakato wa zabuni ya kumpata mtalaam mwelekezi kufanya upembuzi yakinifu wa mahitaji ya kuendeleza bandari kuu za maziwa umekamilika na mkataba utasainiwa mwezi huu wa Novemba, 2013. Aidha, wawekezaji binafsi wamealikwa kuonesha nia, yaani *Expression of Interest (Eoi)* ya kuendeleza bandari ya Mwanza Kusini na tarehe ya mwisho ilikuwa 20 Julai, 2013. Tathmini imekamilika na *proposal*/zitaitishwa mwezi huu wa Novemba, 2013 ili kubaini mwekezaji mwenye manufaa zaidi kwa Serikali. Ujenzi utafanyika mara tu zoezi la kumbaini mwekezaji mwenye manufaa kwa Serikali litakapokamilika.

(b) Mheshimiwa Spika, meli ya MV. Victoria inafanyiwa matengenezo mara mahitaji yanapojitokeza. Aidha, meli hii ipo katika mpango wa kufanyiwa ukarabati mkubwa, yaani *refurbishment* na *DANIDA*. Ratiba iliyotolewa na *DANIDA* inaonesha kuwa ukarabati mkubwa wa meli hiyo utafanyika kuanzia mwezi Juni, 2017 hadi Machi, 2018.

SPIKA: Mheshimiwa Leticia Nyerere, swali la nyongeza. Jamani, umeme unakatikatika sasa.

MHE. LETICIA M. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahadi ya Mheshimiwa Rais, popote pale katika mfumo wowote ule hutekelezwa na Serikali yake na sio yeye mwenyewe. (*Makofi*)

Katika uchaguzi wa mwaka 2010, Mheshimiwa Rais aliahidi kununua meli tatu kwa ajili ya Ziwa Victoria. Je hizi meli ziko wapi?

[MHE. L. M. NYERERE]

Swali la pili; Serikali imeshaahidi kwa nyakati tofauti kufanya ukarabati wa MV Butiama, lakini mpaka sasa hivi hakuna chochote ambacho kimefanyika. Naomba Kauli ya Serikali. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni za uchaguzi wa mwaka 2010 hakuahidi meli tatu katika Ziwa Victoria, isipokuwa aliahidi meli tatu; moja katika Ziwa Victoria, moja katika Ziwa Tanganyika na moja Ziwa Nyasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mchakato wa matengenezo wa hizi meli unaendelea na tumekuwa tukieleza hapa Bungeni kwamba wenzetu wa *DANIDA* wanafanya maandalizi ya ujenzi wa meli hizi, lakini pia wenzetu nchi ya Korea na wao wameonesha nia na tunaendelea na mchakato na tunakaribia mwisho wa mazungumzo kuhusu utengenezaji wa hizi meli tatu katika Ziwa Tanganyika, Nyasa na Victoria.

Mheshimiwa Spika, (b) ukarabati wa *MV. Butiama* unaendelea sambamba na matengenezo ya *MV. Victoria* na *MV. Liemba*. Serikali imekwishatia saini mkataba wa matengenezo ya meli hizi na kampuni ya *DIAK* ya Uingereza kwa gharama ya Shilingi bilioni sita na ukarabati utaanza mwezi Januari mwaka kesho 2014.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mwijage, swali lingine la nyongeza.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kabla meli ya MV Bukoba haijazama, ilionesha dalili mojawapo ikiwa ni *instability* kutembea upande upande. Ni wazi kwamba *MV. Victoria* haina hali nzuri. Naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri na Serikali, hamwoni hii mipango yenu ya

[MHE. C. J. P. MWIJAGE]

kuikarabati kwa kutumia hao Wa-Denmark mwaka 2017 meli ya Victoria mnatuandalia janga lingine sisi watu wa Ukanda wa Ziwa?

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Mwijage. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, usalama wa hivi vyombo ni jambo ambalo linapewa kipaumbele cha hali ya juu sana na Serikali kupitia wamiliki wenyewe, yaani *Marine Services Company Limited* na Wadhibiti wa Usafiri wa Majini na Nchi Kavu (*SUMATRA*).

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vinafanyiwa utafiti, vinakaguliwa mara kwa mara, na hayo aliyoyasema, yaliyotupata, tumekwishajifunza na kwa hiyo, vinaangaliwa vizuri. Ni kweli *MV Victoria* ni ya siku nyingi kwa hiyo, hilo hatuwezi kukana, imechakaa. Lakini kwamba usalama wake uko hatarini, halina msingi wowote.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, namwomba Mwenyekiti aendelee na maswali ili kusudi na sisi tufanye ushauriano mdogo kabla hatujamaliza maswali.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Wizara ya Maji, swali namba 46 Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar.

Na. 46

Wananchi Kuruhusiwa Kutumia Maji ya Visima vya JICA

MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR aliuliza:-

Katika Kata za Mabama na Ufuluma Jimbo la Tabora Kaskazini kuna mradi wa *JICA* wa uchimbaji visima na miundombinu yake ya kusambaza maji ambapo visima viwili vyenye maji safi na salama vimepatikana katika Kata ya

[MHE. S. A. SUMAR]

Mabama; hata hivyo, kuanzia mwaka 2010 mradi huo haujaendelea na wananchi hawaruhusiwi kutumia visima hivyo:-

(a) Je, kwanini Serikali isiruhusu wananchi watumie visima hivyo?

(b) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na Kata ya Ufuluma ambao hawajapata mradi wa *JICA* kama wenzao wa Mabama?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa katika Kata ya Mabama, katika Halmashauri ya Wilaya ya Tabora Vijijini kuna visima virefu viwili vilivyochimbwa na Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la *JICA*. Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza ilihusu upimaji na uchimbaji wa visima vya maji. Wananchi hawakuweza kutumia visima hivyo kwa kuwa mradi haukukamilika.

Awamu ya pili inatekelezwa mwaka huu 2013/2014 ambayo inahusu ujenzi wa miundombinu ya maji na ufungaji wa pampu. Zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi itatangazwa mwezi Novemba, 2013 na ujenzi utaanza mwezi Aprili, 2014. Hivyo inashauriwa wananchi kusubiri hadi mradi utakapokamilika.

(b) Katika Kata ya Ufuluma, Serikali ilipanga kukijengea Kijiji cha Ufuluma mradi wa maji kupitia *JICA*, kama ilivyokuwa kwa Kata ya Mabama. Katika awamu ya kwanza visima viwili vilichimbwa, lakini vyote vilikosa maji. Katika awamu ya pili visima virefu saba vitachimbwa na kufungwa pampu za mkono na wananchi wapatao 1,750 wa kijiji cha Ufuluma watanufaika na mradi huu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sumar, swali la nyongeza.

MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kwa kuwa Serikali inatambua kwamba Kata ya Mabama kuna visima viwili vimepatikana vikiwa na maji safi na salama; na kwa kuwa mradi huo una sasa takriban miaka mitatu na nusu haujaendelezwa: Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwaruhusu wananchi waendeleo kutumia hayo maji ili kupunguza adha ya maji?

Swali la pili; je, Serikali haioni kwamba inawatesa wananchi kwa sababu mradi huu tangu mwaka 2010 haujakamilika na katika Kijiji cha Mabama hakuna kisima hata kimoja chenye maji safi na salama? Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na ukamilishwaji wa mradi huu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mradi huu umechukua muda mrefu, utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2010. Lakini kama nilivyosema mradi huu unafadhiliwa na *JICA*. *JICA* walianza kuutekeleza mwaka 2010 na wote tunafahamu hapa katikati Japan walipata matatizo ya Sunami, kwa hiyo, miradi mingi ilikuwa imesimama. Sasa hivi wamerudi.

Utekelezaji wa mradi huu unaanza mwezi wa Novemba mwaka huu unatangazwa tenda, na wao wenyewe ndio wamepanga kwamba wako tayari kuanza ujenzi mwezi wa nne. Namwomba Mheshimiwa Mbunge afahamu kwamba Serikali inayo miradi mingi na kwa kuwa mradi huu una wafadhili tayari, Serikali inaelekeza nguvu zilizobaki sehemu nyingine ambazo hawana wafadhili. Nimhakikishie kwamba mradi utakamilika na wananchi watapata maji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Bunda wameteseka sana na tatizo la kutopata maji safi na salama na kumekuwa na mradi wa muda mrefu ambao kila siku tumekuwa tukipewa tarehe, utakamilika kesho, keshokutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kwamba Serikali haipeleki fedha za kutosha, mkandarasi naye amekuwa tatizo. Akisikia viongozi wa kisiasa wanaenda, akisikia Waziri anaenda, ndiyo anaenda *site*. Sasa nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini wananchi wa Bunda watapata maji safi na salama ili nao wajione sawa na Watanzania wengine ambao wanapata maji safi na salama?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba mradi ule wa Bunda wa kutoa maji kutoka Ziwa Victoria na kuwapelekea wananchi wa Bunda umechukua muda mrefu. Lakini sababu mojawapo ya kuchukua muda mrefu ilikuwa ni tatizo la upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 tumeuingiza mradi ule kwenye fedha na ulikwishapewa sasa hivi fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji wake. Lakini pia ni kweli kwamba lipo tatizo la mkandarasi, lakini Halmashauri inasimamia, na tumesema tuwasiliane, kama itaonekana ameshindwa, ziko taratibu za manunuzi zinaweza zikatumika kumwondoa ili awekwe mtu mwingine.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mfutakamba.

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti. Nashukuru. Jimbo la Igalula jirani na Tabora Kaskazini, liko bwawa la Goweko ambalo sasa takriban miaka sita limekuwa linafanyiwa upembuzi yakinifu na hilo ni muhimu kwa ajili ya maji ya kutumia wananchi pamoja na kumwagilia mashamba na mifugo. Lini upembuzi yakinifu wa hilo bwawa utakamilika ili lianze ujenzi na tatizo kubwa la maji Jimbo la Igalula katika Kata ya Goweko liweze kutatuliwa pamoja na Kata nyingine kwa kuchimbiwa visima? Nashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, bwawa alilotamka sina jibu la hakika la kusema hapa kwamba naweza nikasema tumeingiza kwenye bajeti, lakini ninachofahamu tumeyapangia mabwawa fedha yote ya kukarabati na kujenga mengine mapya na kwa Mkoa wa Tabora katika fedha za matokeo ya haraka tumewatengea Shilingi bilioni tisa. Kwa hiyo, nitakwenda kuangalia kama katika zile fedha kuna zile ambazo zinakwenda kwa ajili ya ukarabati bwawa ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitamka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Kebwe.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa bwawa la Manchira linasaidia maji katika Mji wa Mugumu kwa asilimia 65 na kwa kuwa Wizara ya Maji walishatembelea katika ufa ambao umejitokeza kwenye tuta ambayo ni hatari, ajali inaweza ikatokea; katika bajeti ya Shilingi milioni 500 ambayo Wizara ilitenga kwa mwaka huu wa fedha, ni kazi gani ambayo imekwishaandaliwa kwa ajili ya kazi hii muhimu kwa ajili ya wakazi wa Mji wa Mugumu?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bwawa la Manchira ambalo limejengwa na linatoa maji kwa ajili ya wananchi wa Mji wa Mugumu lina ufa ambao unatakiwa ukarabatiwe haraka, nami mwenyewe nimefika pale na nimeliona. Huo ndiyo ulikuwa msingi wa kutenga hizo fedha Shilingi milioni 500. Kwa hiyo, fedha hizi zitatumika kukarabati kuhakikisha kwamba ule ufa uliotokea unazibwa na hautokei tena. Hivi ninavyoongea, Wizara yangu inafanya *process* ya kuzipeleka hizo fedha kwa ajili ya kukarabati hilo bwawa.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali linalofuata ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Zedi, Mbunge wa Bukene.

Na. 47

**Ujenzi wa Bomba la Maji Kutoka
Kahama – Tabora**

MHE. SELEMANI J. ZEDI aliuliza:-

Katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Wizara ya Maji imetenga fedha kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu wa mradi wa kujenga bomba la kutoa maji ya Ziwa Victoria Kahama hadi kuyafikisha Tabora Mjini:-

(a) Je, ni vijiji gani vilivyo ndani ya Jimbo la Bukene na Wilaya ya Nzega ambavyo vitafaidika kwa kupata maji hayo mradi utakapokamilika?

(b) Je, ni lini wananchi wa vijiji hivyo wataanza kutumia maji hayo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la maji linalowakabili wananchi wa Jimbo la Bukene na Wilaya ya Nzega. Ili kutatua tatizo hilo, Serikali inatekeleza mradi wa kujenga bomba la kutoa maji ya Ziwa Victoria hadi kufikisha Tabora Mjini. Mradi huu utahusisha Miji ya Tabora, Nzega, Igunga pamoja na vijiji vyote ambavyo vitakuwa na umbali usiozidi kilomita 12 kwa sasa kila upande kutoka kwenye bomba kuu.

Katika kutekeleza mradi huo kwa mwaka 2013/2014 Serikali imetenga fedha kiasi cha Shilingi milioni 450, kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni pamoja na kutathmini athari za kimazingira. Majina ya vijiji vitakavyopata maji, muda wa

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

kuanza ujenzi na kukamilika kwa mradi na wananchi kuanza kunufaika na huduma ya maji, utajulikana baada ya mtaalam mshauri kukamilisha upembuzi yakinifu.

MHE. SELEMANI J. ZEDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Hofu yangu mimi kwenye mradi huu ni kasi ya utekelezaji. Huu ni mwaka wa fedha wa tatu mfululizo ambapo fedha za kufanya kazi ya upembuzi yakinifu zinapangwa, lakini mwaka wa fedha unakwisha kazi haijafanyika. Sasa hivi tuko nusu ya mwaka wa fedha huu tulionao, kwa hiyo, tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie kazi ya upembuzi yakinifu mwaka huu imefikia hatua gani?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri uko tayari kufanya ziara katika maeneo ambayo bomba hili litapita uzungumze na wananchi kuwaeleza mpango ambao Wizara inao kuhusu utekelezaji wa mradi huu ili angalau wananchi wapate imani kwamba mradi huu kweli utatekelezeka kwa sababu sasa hivi wanaanza kupoteza matumaini? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana kwa kufuatilia huu mradi kwa sababu anafahamu umechukua muda mrefu. Tulichelewa kuanza utekelezaji kwa sababu fedha hazikuwepo. Lakini sasa hivi hizi fedha Shilingi milioni 450 zipo na zimetengwa, na yeye mwenyewe ni shahidi, tulipitisha humu ndani Shilingi milioni 184.5 ni kati ya hizi fedha ambazo zinakwenda kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ninavyoongea, mwezi wa Tatu tulishatangaza ili kupata wataalam washauri, tumewashindanisha, mwezi wa Sita tathmini imekamilika. Sasa hivi tunasubiri mshindi aliyepatikana kusaini naye mkataba mwezi huu wa Kumi na mwezi wa Kumi na Moja itaanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na baada ya kukamilika ndipo tutajua mradi huu utapita kwenye maeneo yapi, kwenye vijiji vipi na itakuwa nafuu wakati huo kuwaeleza wananchi kuhusu hilo.

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Kuhusu utayari wa mimi kufanya ziara, niko tayari, lakini kwa sasa hivi kabla usanifu haujamilika ambao utainisha njia ya ule mradi, itakuwa vigumu kuwaambia wananchi kwamba mradi utapita hapa wakati *design* haijasema. Tutawaambia wananchi kwa ujumla kwamba mradi huu utapita ukienda Tabora na vijiji vyote ambavyo vitapitiwa na mradi huu vitapata maji. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan.

MHE. SUSAN A. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Maji ni uhai, na wote tunatambua na kila Mbunge anayesimama hapa anaonesha jinsi ambavyo kuna matatizo makubwa kwenye Jimbo lake au sehemu anayotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Waziri atuambie, Dar es Salaam hususan Wilaya ya Kinondoni kuna tatizo kubwa sana la maji hasa yale mabomba tunayoyaita mabomba ya Mchina. Inatokea kwamba kwa wiki mzima hakuna maji. Je, Mheshimiwa Waziri unatolea tamko gani matatizo ya maji katika Jiji maarufu kama la Dar es Salaam? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Susan kwamba Dar es Salaam ni Jiji kubwa na lina matatizo ya maji na sababu mojawapo ni kwa sababu miundombinu iliyopo ni ya muda mrefu na sababu ya pili ni kwamba uzalishaji wa maji ni kidogo. Serikali imechukua hatua kubwa, sasa hivi tunatekeleza miradi mikubwa mitatu. Mradi wa kwanza ni kutoa maji kutoka Ruvu Chini unaoongeza kutoka lita milioni 182 mpaka 270 na tayari ujenzi wake umeshaanza. Sasa hivi wanalaza mabomba.

Mradi wa pili ni wa kutoa maji Ruvu Juu ambao unaoongeza maji mpaka lita milioni 196 kutoka lita milioni 82;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

na mradi wa tatu ni wa visima vya Kimbiji na Mpera ambao utaongeza maji lita milioni 260.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi yote hii imekwishaanza kutekelezwa. Itakapokamilika, nataka niwahakikishie wananchi wa Dar es Salaam kwamba watapata maji ya kutosha. Kazi ya pili ambayo tayari nayo imeanza kutekelezwa ni kufanya tathmini ya namna ya kupanua mtandao wa maji katika Mji wa Dar es Salaam. Kwa wakati huu tutajitahidi kwamba maji yaliyopo yanayozalishwa lita milioni 300 yagawiwe vizuri ili wananchi waweze kupata maji, na pale kunapokuwa na matatizo ya mgao, basi tuwasiliane tuweze kurekebisha mambo yaende vizuri.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa mradi huu wa kupeleka maji Mkoa wa Tabora kupitia Nzega na Igunga utapita pia Igunga, Waziri anaweza kukubaliana nami kwamba wakati anakuja Nzega pamoja na kule Bukene kama alivyoahidi apite pia Igunga kuzungumza na wananchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Kafumu, amekuwa akifuatilia sana miradi ya maji katika Jimbo lake la Igunga. Ni hivi jana tu amenikumbusha kuhusu matatizo ya maji ya Jimbo lake. Nataka nimwahidi yeye na wananchi wa Igunga kwamba nitafanya ziara kutembelea Jimbo lake na kuwaeleza wananchi mikakati iliyopo ya kutatua tatizo la maji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti katika hatua ya upembuzi yakinifu kumekuwepo tabia ya wakandarasi au hawa

[MHE. E. M. MAIGE]

wataalam kutoshirikisha wananchi. Katika awamu ya kwanza ya ule mradi wa Ziwa Victoria kwenda Kahama na Shinyanga, kuna baadhi ya maeneo ambayo ni vijiji, kwa mfano vijiji vya Makuzuka, Kabondo, Matinze, Izuga-Bubungu ambavyo vimepitiwa kabisa na bomba lakini havikupata maji kwa sababu vililitwa ni vitongoji. Sasa kwenye hii hatua, Mheshimiwa Waziri anatumuhakikishiaje kwamba wananchi watashirikishwa ili kuepusha matatizo yaliyojitokeza kwenye awamu ya kwanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika utekelezaji wa mradi awamu ya kwanza ya kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Kahama na Shinyanga kuna vijiji vililachwa kwa sababu ya kutoshirikishwa.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Maige kwamba sasa hivi Wizara yangu inafuatilia kwa kina kwenye miradi hii mipya ya kuona kwamba sehemu zote ambazo bomba linapita wananchi hawaachwi. Vile vile tumekuwa tukiagiza kwamba pale ambapo yanatoka maji lazima tuhakikishe kwamba wananchi wa ile *source* wapate maji ili nao pia waweze kuwa walenzi wa ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji alivyovitaja, tumeviingiza vile vijiji katika awamu hii ya vijiji 100 na tunaanza na vijiji 40 vya kutoa maji kwenye bomba kuu kuwapatia wananchi na fedha zake zipo tumetenga Shilingi bilioni mbili. Hivi sasa utekelezaji wake umekwishaanza. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tatizo la maji nchi nzima ya Tanzania ndiyo tatizo namba moja na kama kuna agenda ambayo inaondoa uhalali wa Serikali hii ni agenda ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni nchi ya 11 kwa mito mingi duniani. Tanzania ni nchi ambayo ina Ziwa kama

[MHE. D. Z. KAFULILA]

Tanganyika ambalo lina asilimia 17 ya maji ya kunywa duniani. Lakini Watanzania walioko Kigoma mita 100 mita 200 kutoka usawa wa ziwa hilo, hawana huduma ya maji. Hivi Serikali ya CCM ilitaka ipate nchi yenye vyanzo kiasi gani vya maji iweze kuwapatia wananchi maji? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu. Mheshimiwa Wasira.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kutekeleza miradi ya maendeleo na kuweka vipaumbele ni suala la Bunge Zima ambalo ndilo linasimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Katika mpango huo, maji yamewekwa na yamepewa kipaumbele na katika mpango unaoitwa *Big Results Now*, maji ya vijijini yamepewa nafasi kubwa. Bunge hili kwa mwaka jana 2012, ilitenga Shilingi bilioni 184 kwa ajili ya kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka ieleweke ya kwamba Serikali inafanya yake na inajua matatizo haya. Kwa Mji wa Kigoma kwa mfano, tunao mradi mkubwa sana ambao unagharamiwa na Umoja wa Ulaya ambao unakusudia kusambaza na kumaliza tatizo la maji katika Mji wa Kigoma. Vile vile bomba kuu la kutoka Mwanza ambalo linakwenda mpaka Kigoma ni katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambalo tulisema tutafikisha maji Tabora, Nzega na Igunga. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi maeneo hayo kwamba kazi hiyo itafanyika na utekelezaji utafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu majibu yaliyotolewa hapa Bungeni kuhusiana na kuchelewa kwa miradi mingine, ni kweli miradi ya maji mingine imechukua muda mrefu sana. Katika Mji wa Dar es Salaam kwa mfano hatua zinachukuliwa sasa na ahadi ya Serikali ya kuongeza kiwango cha maji katika Jiji la Dar es Salaam utafanyika.

Huko Bunda mradi unaendelea hivi sasa na fedha zimeshatolewa, mabomba yanatengenezwa na mkandarasi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

aliyekuwa anasuasua sasa anasimamiwa kikamilifu na mabomba sasa hivi yako Dar es Salaam, yatapelekwa Bunda na kazi hiyo itamalizika ifikapo Desemba mwaka huu 2013. (Makofi)

Kwa hiyo, kazi inayofuata katika mradi ule ni kupanua na kuweka miundombinu kwa ajili ya maji ya Mji wa Bunda. Kwa hiyo, wasiwasi unaotolewa Bungeni hapa, hauna msingi na kazi inaendelea. (Kicheko/Makofi)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, *order please!* Order please! Mheshimiwa Waziri wasiwasi uko mkubwa sana. Mheshimiwa Haji.

MHE. MUSSA HAJI KOMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa mujibu wa maamuzi ya nchi hii tuliambiwa mwaka 2020 wananchi wa Tanzania watapata maji safi na salama. Kwa kutokana na mawazo kama haya na maswali mbalimbali yanayotokea ndani ya Bunge, ningeiomba Serikali itueleze, bado nia hiyo wanayo au kuna tatizo gani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo nia bado ipo na tunataka kwenda zaidi ya hapo. Tulipanga katika Mpango wa Milenia kwamba ifikapo 2015 tuwapatie Watanzania waishio Vijijini maji kufikia 65%. Tulipoanzisha Mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, tumejiwekea kufikisha 74% mwaka 2015. Kwa hiyo, tunakwenda zaidi ya lengo. Ifikapo 2025, tuwapatie Watanzania 90% waishio vijijini. Mpango huo bado upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipanga kwa Watanzania waishio mijini, katika malengo ya Milenia na Ilani ya Uchaguzi tufikishe 86% ifikapo mwaka 2015. Utekelezaji uliopo sasa hivi, tumekwishafika 88% na tunakaribia kwenye 90%, kwa hiyo, tutavuka lengo. Ifikapo 2025 tumepanga tufikie 95% na zaidi kwa ajili ya maji ya miji mikubwa.

[NAIBU WAZIRI WA MAJI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango hii inatekelezeka na utekelezaji wake umeanza. Mpaka sasa hivi tumeshapeleka maji vijijini zaidi ya vijiji 752 na tunatarajia ifikapo mwaka kesho mwezi wa Sita tuwe na vijiji 1,449 vinavyopata maji ambavyo vitakuwa ni sawasawa na Watanzania 7,100,000 wameongezeka.

Kwa hiyo, malengo yetu ni kwamba, ifikapo mwaka 2015 tutakuwa na Watanzania wanaopata maji milioni 30.6 ambao kwa kweli ni kiasi kikubwa ukilinganisha na idadi ya Watanzania tulionao kwa sasa hivi ambao ni milioni 44.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa, swali la mwisho la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na mawazo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ningependa kujua mpango wa maji ya Ziwa Victoria kutoka Magu kwenda katika Miji ya Sumve, Nyambiti na Malya; mpango huu umefikia wapi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nampongeza Mheshimiwa Ndassa kwa kufuatilia sana mradi huu wa maji ili wananchi wake wa Ngudu, Magu, waweze kupata maji. Huu mpango upo, tunao mradi ambao tayari tulikwishatangaza tenda za kupata Wataalamu Washauri ambao watafanya tathmini, watafanya upembuzi yakinifu na usanifu kuainisha sehemu ya kutoa maji kwenye Ziwa Viktoria na njia ya kupita. Lakini nataka nimhakikishie kwamba miji ya Magu na Ngudu itapata maji kutoka Ziwa Victoria.

MWENYEKITI: Nakushukuru. Sasa tunaendelea na swali na Mheshimiwa Muhammad Sanya, kwa niaba yake Mheshimiwa Hamad Ali Hamad.

Na. 48

Kuanzisha Kiwanda cha Betri za Radio Nchini

MHE. HAMAD ALI HAMAD (K.n.y. MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA) aliuliza:-

Wananchi walio wengi nchini huishi vijijini ambapo njia pekee ya kupata taarifa mbalimbali za masuala yanayowahusu kama kilimo, afya, elimu, uchumi, maendeleo, na kadhalika, ni kupitia matangazo ya redio; na redio hizo hutumia betri ambazo huingizwa kutoka nje ya nchi, lakini zikiwa katika viwango hafifu na zisizodumu kwa muda mrefu:-

Je, Serikali haioni kuwa umefikia wakati wa kutafuta mwekezaji ili kiwepo kiwanda cha kutengeneza betri za redio zenye viwango?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa idadi kubwa ya wananchi wanaoishi vijijini wanapata taarifa mbalimbali kupitia matangazo ya redio ambazo hutumia betri (*Dry Cell Batteries*), hivyo kuwa na betri zenye viwango na zinazodumu ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa bado hakijapatikana kiwanda kingine cha kuzalisha betri kavu nchini, zaidi ya kiwanda cha *Matsushida East Africa*. Kiwanda hiki ambacho sasa kinaitwa *National Panasonic battery (T) Co. Ltd* ambacho kinazalisha betri milioni 100 kwa mwaka, wakati mahitaji ya betri nchini yanakadiriwa kuwa zaidi ya milioni 250 kwa mwaka, mahitaji ambayo hukua kwa 3% kila mwaka.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mahitaji ya betri nchini kuwa makubwa zaidi ya uzalishaji uliopo, kampuni ya *Tiger Head* kutoka China imefanya makubaliano na Kampuni ya Tanzania (*African Logistics*) ya kujenga kiwanda kingine nchini cha kuzalisha betri.

Kampuni hii kwa sasa inaingiza nchini betri aina ya *Tiger Head* kwa lengo la kuziba pengo la mahitaji ya betri nchini. Hivi sasa, Wizara yangu na kituo cha Uwekezaji (*TIC*), tunaendelea kushawishi uwekezaji huo ili makampuni mengine yajitokeze kwa lengo hilo.

MHE. HAMAD ALI HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa uzalishaji wa betri kwa mwaka ni chini ya 50%; na kwa kuwa Watanzania walio wengi wanapata taarifa mbalimbali muhimu kwa njia ya redio zinazotumia betri: Je, ni kwa sababu gani kiwanda hiki kinatengeneza kiwango hiki kidogo cha betri wakati soko lipo?

(b) Kwa kuwa uzalishaji wa betri kwa mwaka ni chini ya 50%; na kwa kuwa, wananchi wa Tanzania wanaendelea kutegemea kupata taarifa kwa njia ya redio zinazotumia betri na hasa kuelekea kipindi hiki cha machakato wa mabadiliko ya Katiba: Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha kwamba, kiwanda hiki kinazalisha katika *full swing* au angalau 75% ya uzalishaji kwa mwaka? Ahsante.

MWENYEKITI: Majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa sababu zinazopelekea uzalishaji kuwa mdogo wakati mahitaji ni makubwa kusema kweli, sehemu kubwa ya sababu hizi ni nguvu ya soko. Nikisema nguvu ya soko nina maana kwamba, ushindani uliopo mkubwa unasababisha uuzaji wa betri

[NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

nyingine kutoka nje. Kwa mfano, kama nilivyosema kwamba kiwanda hiki cha *National Panasonic* wanashindana na *Tiger Head*. Kwa hiyo, ule ushindani unaweza ukaleta uzalishaji kuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna ushuru mkubwa (*Import Duty*) ambao unatozwa katika baadhi ya malighafi ambazo zinatengeneza betri. Ushuru huu umeshakuwa mkubwa kiasi cha 25% na kiasi kikubwa cha ushuru huu kinasababisha bei ya betri kuwa kubwa. Kwa hiyo, wananchi wanashindwa kumudu bei hiyo. Kwa hiyo, uzalishaji unakuwa mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la pili kwamba Serikali ina mkakati gani kuhusu kuhakikisha kuwa angalau uzalishaji wa betri ufikie kiwango kizuri kidogo na kuweza kukidhi mahitaji ambayo yapo, kusema kweli ni kwamba, suala la kuhakikisha kiwanda hiki kinazalisha zaidi ni jukumu la kiwanda chenyewe, siyo jukumu la Serikali.

Kwa hiyo, Wizara yangu imepokea malalamiko kutoka Kampuni ya *National Panasonic* kuhusu ushuru huu mkubwa ambao nimeusema katika jibu langu la msingi kwamba unasababisha bei inakuwa kubwa na wananchi wanashindwa kumudu hiyo. Suala hili linazungumzika, kwa hiyo, nina mpango wa kuongea na Wizara ya Fedha kuangalia ni jinsi gani ambavyo wangeweza kuwasaidia hawa wenzetu wa kiwanda waweze kupata unafuu wa ushuru huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, juhudi zaidi zinafanyika kuweza kudhibiti uingizaji wa betri *fake*, ambayo pia itasaidia kuongeza uzalishaji wa betri za *National Panasonic* hapa nchini. Vilevile naanza kushauri kwamba, kampuni ya *National Panasonic* yenyewe iweze kuingia ubia na wengine ili waweze kusaidia kuongeza uzalishaji. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtutura.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Mara nyingi tumekuwa tukiona bidhaa mbalimbali ambazo zina udhaifu wa ubora zikiangamizwa katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu. Lakini suala la betri Watanzania wote watakuwa mashahidi kwamba, hizi betri ya *Tiger Head* zina ubora wa chini sana, lakini hatujaona hata siku moja betri hizi zikiangamizwa. Je, Mamlaka ya Udhhibiti wa Ubora wameridhika na ubora wa betri hizi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mtutura, nakubaliana naye kwamba, kweli hizi betri zina kemikali ambazo zinaweza zikaleta madhara. Nithibitishe kwamba, *TBS* wameliangalia hili na kuzidi kusisitiza kwamba, wametoa tangazo kama vile tulivyoona kwenye gazeti la Majira la mwezi Mei mwaka huu, 2013, wamezidi kuzuia uingizaji wa betri *fake* hapa nchini zikiwemo betri hizi za *Tiger* ambazo zinaingia na *TBS* imethibitisha kabisa kwamba betri hizi za *Tiger Head* zinazoingia hapa nchini, zimekidhi ubora ambao unaohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wananchi kwamba, hiyo wanayosema kwamba betri za *Tiger* hazina ubora, ni kweli kwamba zimeshathibitishwa zina ubora. Naomba wananchi kwa ujumla kwamba, wanaponunua betri wahakikishe kwamba, betri hizo zina nembo ya *TBS* ile ambayo nimethibitisha kwamba zina ubora.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lema.

MHE. GODBLESS J. LEMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika Jiji la Arusha, kulikuwa na kiwanda cha kutengeneza redio cha *Phillips*. Kiwanda hicho kwa sasa kimekufa na eneo hilo limeanza kuwa pori na majengo yake yameanza kuchakaa. Je, Serikali ina mpango gani na kiwanda hicho ama eneo hilo kwa sasa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kiwanda cha redio cha *Philips* kimekufa muda mrefu sana na ni ukweli kama alivyosema, nami nimhakikishie kwamba, suala hili nitalichukua niweze kuliangalia halafu nilete majibu ambayo yana uhakika hapa Bungeni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamad Rashid.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tunaelewa kwamba Serikali inawahimiza sana wawekezaji katika viwanda, lakini viwanda kama havilindwi, kila siku tutakuwa na tatizo hili kwamba viwanda vipo, havizalishi kwa ukamilifu kwa sababu havina ulinzi kutoka Serikalini. Je, Serikali ina Sera gani juu ya kuvilinda viwanda vya ndani ili viweze kushindana na wale ambao wanaingiza bidhaa, siyo tu hafifu, lakini hata kuingiza bidhaa zenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikupe mfano tu, Marekani wanalinda viwanda vya chuma na huwezi kuingiza chuma Marekani, ni lazima ununue vyuma vinavyozalishwa Marekani. Tumeshindwa nini kutengeneza Sera ambayo inakiwezesha kiwanda kupanuka kutokana na ulinzi unaolindwa na Sera za Viwanda?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ushauri wake wa kuwa na Sera unachukuliwa. Lakini nimhakikishie kwamba, viwanda vya ndani tunavilinda na ndiyo maana Kauli Mbiu yetu ya Wizara ni kwamba, Nunua Bidhaa ya Taifa Hapa Nchini ili Uweze Kujenga Taifa Lako. Nasisitiza kwamba bidhaa ambazo zinazalishwa hapa nchini na zinasindikwa hapa nchini zipewe kipaumbele na wanunuzi wote ambao wanazinunua ili ziweze kusaidia kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama nchi, kama tulivyo sisi Watanzania kwamba sisi ni wanachama wa *WTO – World Trade Organisation* na kuna *standards* ambazo zinaruhusiwa; na kama zinakidhi *standards* ambazo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA]

zinaruhusiwa za Kimataifa hatuna budi tusingitize kwamba, hakuna uwoga wa kuingiza bidhaa hiyo, na kuuza bidhaa hiyo na inaruhusiwa Kisheria kwa sababu, inakidhi matakwa ya *WTO*. Kwa hiyo, ni bora tuzingatie hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Faki?

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, naitwa Mheshimiwa Khatib Said Haji. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, swali moja la nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Uwekezaji wa Zabendo ya Muza ina kiwanda cha betri zinazozalishwa zinazoitwa *Magic Cell*. Kwa bahati mbaya hapa hata Wizara yako... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde.

MWENYEKITI: Hebu Mheshimiwa, kaa kwanza.

Hapa, Spika (Mhe. Anna S. Makinda) Alikalia Kiti

SPIKA: Wataalamu wamekuwa wengi. Kilichotakiwa ni kwamba, Mwenyekiti angeniambia namwachia Kiti Mwenyekiti, kwa hiyo, najua kwamba, tunakuja kuonana. Sasa na Wataalamu wangu wananiambia amesimama-amesimama. Sasa ndiyo hivyo.

Nani alikuwa anasema? Aendelee.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, swali dogo la nyongeza?

Mheshimiwa Spika, kampuni ya kizalendo ya Wazawa Tanzania, *MUZA*, ina kiwanda cha betri na kinachozalisha mabetri aina ya *Magic Cell* na Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa anajibu swali la msingi hakukiweka kiwanda hiki

[MHE. K. S. HAJI]

katika orodha. Kiwanda hiki kimesimamisha uzalishaji kutokana na ushindani usio wa halali unaofanywa nchini na betri la *Tiger Head*. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa kauli gani katika kulinda ushindani wa uhalali wa biashara hasa ukizingatia kwenye soko la betri, ili kiwanda hiki kiweze kurudi kwenye soko?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba, nimevitamka viwanda ambavyo vinazalisha hivi sasa, nimetamka kiwanda cha *Panasonic* ambacho kinazalisha kiwango cha betri kama nilivyataja kadiri ya milioni 100 na nimetamka kiwanda cha *Tiger Head* kwa sababu nacho kinaingiza betri ili kuziba pengo ambalo nimesema lipo. Hiki kiwanda cha *MUZA* ambacho kinazalisha betri za *Magic Cells* sikuweza kukitamka kwa sababu kiwanda hiki kimekuwa hakizalishi hivi sasa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, bado maswali ni mengi na muda umekwisha. Naomba twende Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Abia Nyabakari, aweze kuuliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Kabati.

Na. 49

Madhara ya Nguo za Ndani Zitoazo Rangi

MHE. RITTA E. KABATI (K.n.y. MHE. ABIA M. NYABAKARI)

aliuliza:-

Nguo nyingi za ndani zinazotengenezwa na kuingizwa nchini zinatoa rangi, na utoaji rangi huo hudumu mpaka nguo hizo zinapokwisha:-

(a) Je, Serikali inaweza kutueleza madhara yatokanayo na rangi hizo?

(b) Kama hakuna: Je, Serikali imejiridhishaje kwamba rangi hizo hazina madhara kwa binadamu?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, matumizi ya rangi mbalimbali zinazotumika kutengeneza nguo hudhibitiwa ili kuhakikisha kwamba hazileti madhara kwa mtumiaji wa nguo. Kemikali zinazoengenezea nguo viwandani hazina madhara katika mwili wa binadamu kwa kuwa Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali huzifanyia ukaguzi kabla ya kuanza kutumika.

Aidha, utoaji wa rangi katika nguo mpaka zinapokwisha, yaani kuchakaa, hutokana na teknolojia hafifu au rangi zenye ubora duni zilizotumika kwenye utengenezaji wa nguo. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kupitia Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali, inashauri kuwa endapo ikitokea mtumiaji wa nguo zinazotoa rangi akipata madhara kama kuwashwa, vipele au mzio, yaani *allergy*, mhusika aende kwenye Kituo cha Huduma za Afya kuonana na Daktari kwa uchunguzi na ushauri.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inasimamia na kudhibiti matumizi mbalimbali ya kemikali, zikiwemo rangi zinazotumika katika utengenezaji wa nguo kulingana na Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali, Sura Namba 182 ya mwaka 2003.

Serikali itaendela kufanya ukaguzi wa Kemikali za viwandani, zinazotumika kutengeneza nguo na kutoa ushauri kwa wenye viwanda kabla ya kutumia kemikali hizo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kabati, swali la nyongeza.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa nini Serikali isidhibiti uingizaji wa nguo zenye uhafifu na uduni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa liko pia tatizo la uingizaji holela wa nguo za mitumba nchini ambazo wakati mwingine huleta madhara ya kiafya kwa binadamu: Je, Wizara inadhhibitije suala hili?

SPIKA: Ahsante kwa kuuliza vizuri maswali ya nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, na wewe kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, suala la udhibiti la viwango linasimamiwa na *TBS* na tunazungumza mara nyingi tu kwamba bidhaa zinapoingizwa basi huwa zinapata ukaguzi wa Shirika la Viwango na kuangaliwa juu ya viwango vyake na kuruhusiwa kuingizwa nchini kwa ajili ya matumizi. Katika Wizara yangu tunasimamia usalama wa mali na vifaa pamoja na kemikali zinazotumika katika nguo ili kumhakikishia mtumiaji asiwe amepata madhara katika matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa katika maeneo hayo, uingizaji wa nguo, idadi yake na ni nguo za aina gani kwa hakika ni eneo ambalo limeenda sambamba na mabadiliko ya mfumo wa kiuchumi na maendeleo ya nchi yetu toka tulipoanza miaka yote hiyo mpaka sasa. Pale tutakapokuwa na uwezo wa kuwa za nguo za kutosha ndani katika uzalishaji, tunapokuwa na ubora wa nguo zinazolingizwa udhibiti wake ukiwa imara kama unavyoendelea hivi sasa, naamini hakutakuwa na madhara yanayotokana na uingizaji wa hizo nguo.

SPIKA: Naomba tuendelee na swali linalofuata, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Josephine Genzabuke atauliza swali.

Na. 50

Soko la Mazao ya Alizeti na Ufuta

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Wakulima wengi wa Mkoa wa Kigoma wakiwemo wanawake na vijana wameitikia wito wa kuanzisha kilimo cha mbegu za mafuta zikiwemo Alizeti na Ufuta:-

- (a) Je, Serikali imeandaa mazingira gani kuhusu soko la mazao hayo?
- (b) Je, Serikali inaagiza mafuta ya kula kiasi gani kutoka nje ya nchi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuandaa mazingira ya soko la mazao ya alizeti na ufuta, Serikali itaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kukamua mbegu za alizeti na ufuta kupitia uwekezaji wa viwanda vidogo vya wakulima (*semi refinery*) na viwanda vikubwa (*double refinery*) pamoja na kuondoa kodi na ushuru wa mitambo na mashine za kilimo zikiwemo za kukamulia mbegu za alizeti na ufuta ili kuongeza usindikaji wa mbegu za mafuta na hivyo kuwepo kwa soko la uhakika kwa wakulima wa mbegu za mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeshawahi kueleza humu Bungeni kupitia utekelezaji wa kuendeleza Sekta ya Kilimo, *ASDP*, Halmashauri za Wilaya zikiwemo za Mkoa wa Kigoma zimewezeshwa kujenga viwanda vidogo vidogo na kununua mashine za kukamua mbegu za mafuta na hivyo kuongeza usindikaji wa mbegu za mafuta nchini na kutoa soko la uhakika kwa wakulima.

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu inafanya utafiti wa kujifunza namna ambavyo wakulima wadogo wa Malyasia na Indonesia walivyohusishwa katika mpango uliokuwa na mafanikio makubwa wa kuongeza uzalishaji wa Mawese.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mafuta ya kula nchini sasa hivi yanakuwa kila mwaka lakini katika mwaka huu yanakadiriwa kuwa wastani wa tani 380,000 ambapo uzalishaji wa ndani ni asilimia kama 30 sawa na tani 100,000 na mafuhta yanayoagizwa kutoka nje ni 60% mpaka 70% sawa na tani 280,000 hadi tani 300,000.

SPIKA: Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Swali la kwanza, kwa kuwa sasa wakulima wengi wanazalisha mafuta ya alizeti na ufuta ambayo yana soko zuri ndani na nje ya nchi na wapo watu ambao wanaingiza mafuta ghafi wakidai kwamba yanakuja kusafishwa yanapokuwa yameingia nchini wakati ni mafuta safi ya kula: Je, Serikali ina mpango gani wa kuzuia uingizaji wa mafuta ya kula yanayotoka nje ili mafuta yetu ya alizeti yapate soko zuri? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa Mkoa wa Kigoma wakulima wanalima alizeti na michikichi inayotoa mafuta ya mawese: Je, Serikali iko tayari kuhamasisha wawekezaji kuja kuwekeza kiwanda cha kusindika mafuta ya kula katika Mkoa wa Kigoma? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi, tupo nje ya muda.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema, mafuta yanayoagizwa ni *refined* au *semi refined palm oil*. Ni mafuta kidogo tofauti,

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

siyo mafuta kama haya ya alizeti na ufuta. Kwa maana hiyo, hata kwenye Soko la Dunia mafuta ya alizeti ufuta yana bei kubwa zaidi kuliko yale mafuta ya mawese. Kwa hiyo, tunachohimiza Wizara ya kilimo, siyo kuacha kuzalisha moja au kufanya mengine nasema tuzalishe yote kwa sababu mafuta yetu sisi tunayozalisha alizeti na ufuta yana bei kubwa sana kuliko mafuta mawese na kwa maana hiyo wanaoleta mafuta haya wanaamini unaweza kuleta mafuta ya mawese lakini pia unaweza kuagiza nje mafuta ya alizeti kwa maana ya mambo ya *demand and supply*. Kwa hiyo, tunachosema ni kwamba tutazalisha yote kwa sababu bado soko la dunia linahimili uzalishaji wa mazao yote matatu.

Mheshimiwa Spika, hili la wawekezaji kuja Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya mafuta ya kusindika wawekezaji wengi wameomba na wamependa kuzalisha kwenye Mkoa wa Kigoma lakini pia kwenye Mkoa wa Rukwa na Katavi, mafuta ya mawese na mafuta mengine ya kula. Tatizo ni upatikanaji wa ardhi na ni jambo ambalo tunalzungumza ili wenzetu Wizara ya Ardhi lakini na uongozi wa Mkoa ubaini maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji huu mkubwa wa mafuta ya kula.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimwa Faida Mohammed Bakar.

Na. 51

Sababu za Kufa kwa Zao la Minazi

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR aliuliza:-

Zao la nazi linategemewa sana nchini hususan ukanda wa Pwani na Zanzibar kwa upande wa biashara na chakula, lakini sasa imeonekana minazi mingi kufa (au kupungua).

Je, ni sababu gani zinazosababisha zao la minazi kufa kwa wingi?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, zao la nazi limekuwa likiathiriwa na ugonjwa wa kunyong' onyea minazi unaojulikana kitaalam kama *Coffee Coconut Lethal Disease (CLD)* ambapo hapa nchini mara ya kwanza ulionekana huko Bagamoyo mwaka 1905 na Msimbati Mtwara 1912. Katika kukabiliana na tatizo la kufa kwa minazi Serikali ilianzisha Mpango wa Taifa wa Uendelezaji Minazi, *National Coconut Development Program* wa mwaka 1979.

Mheshimiwa Spika, kupitia utekelezaji wa mpango huo, mwaka 1981 ulifanyika utafiti uliobaini sababu za minazi kufa kwa wingi kuwa ni ugonjwa wa kunyong' onyea *CLD* na madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabia nchi hasa ukame. Utafiti huo ulibaini kwamba ugonjwa huo unasababishwa na vimelea yaani *vector* vinavyojulikana kama *phytoplasma* vinavyosambazwa na mdudu aitwae *Diastrombus mkuranga*. Aidha, kwa sasa Wilaya zilizoathirika zaidi ni Wilaya ya Rufiji, Wilaya ya Kilwa na Wilaya mkuranga.

Mheshimiwa Spika, pamoja na utafiti huo wa muda mrefu ugonjwa huo bado unaendelea kuwa tishio kubwa hapa nchini kutokana na ukweli kwamba magonjwa yanayosababishwa na vimea hivyo vya *phytoplasma* yanahitaji utafiti wa muda mrefu na endelevu. Utafiti uliofanyika hadi sasa unaoneshwa kwamba matokeo ya matumizi ya sayansi na teknolojia kwa maana ya *bio-technology* ambayo yamefikwa kwenye maeneo mengine ya kilimo yanaweza kutumika na yanahitajika kwenye ugonjwa huu wa minazi. Hivyo Wizara yangu itaendelea na utafiti kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo pamoja na kuendelea na kuzalisha mbegu za minazi inayovumilia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

ugonjwa huo na kuhimiza kupanda miche hiyo pamoja na kufuata ushauri wote unaopendekezwa na wataalam wa kilimo kama njia ya kupunguza tatizo hilo.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Faida Bakar, swali la nyongeza.

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa mbali na ugonjwa wa minazi lakini hivi sasa kumejitokeza wimbi kubwa la baadhi ya watu kuikata minazi kwa makusudi; mnazi umekaa miaka 100 pengine au 20 au 30 lakini anaukata kwa siku moja kwa kupata vitale; kwa sisi Wazanzibari na watu wa Pwani tunavijua vitale ni nini. Ni chakula cha kujiburidisha dakika moja tu. Anaukata mnazi kwa dakika moja tu: Je, Mheshimiwa Waziri analijua hili? Kama unalijua, watu hawa wanachukuliwa hatua gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa nazi ni zao la biashara, vile vile ni zao la chakula; na kwa kuwa minazi mingi imeathirika na imepotea kutokana na maradhi ambayo ameyataja Mheshimiwa Waziri: Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwapatia mikopo wakulima wa nazi na miche bure ili waweze kuipanda kwa wingi ili iweze kurudi katika hali yake ya zamani? *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana tuko kwenye muda usiokuwa wa kwetu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, hili la kwanza la kwamba baadhi ya watu wanakata minazi kwa ajili ya vitale na amesema sisi watu wa Pwani wenyewe ndio tunahusika na hilo ni kweli. Hili la vitale na faida najua. Tatizo la vitale ni kwamba inatokana na imani tu kwamba vitale vina viburudisho ambavyo vinaongeza ubora wa miili ya binadamu. *(Kicheko/Makofi)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Kwa hiyo, katika hili tushauriane tu kwamba katika ule mti wa mnazi unafaidika na nazi au unafaidika na kitale? Kwa hiyo, hili linatuhusu sisi wote watu wa Pwani twende tukafanye tathmini hiyo ili tuone kama tunataka kula vitale au tunataka kula nazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la pili kuhusu zao la biashara na zao la chakula, kwa sasa hivi uhai wa mnazi ni miaka kama sabini. Lakini kwa sasa hivi kwa ugonjwa huu, minazi haikai hata miaka mitatu, mine au mitano. Kwa hiyo, tulichofanya, Wizara ya Kilimo ni kwamba tumebaini minazi namna kama kumi, kumi na tano ambayo inaweza ikahimili kama miaka 20. Tunataka tugawe miche hii kwa kujua kwamba itakaa miaka 20 tu lakini itawasaidia wakulima.

Kwa hiyo, tunaomba tuhimizane sisi na watafiti na wakulima pia waridhie kwamba tutatoa minazi hiyo lakini uhai wake hautakuwa uhai mrefu kama ile miche ya zamani ile *East African tall* iliyokuwa inakaa miaka 70, hii itakaa kama miaka 20 hivi, lakini bado itakuwa na faida kubwa kwa uchumi wa wananchi wa Mikoa ya Pwani. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Tunaingia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kilufi atauliza swali linalofuata.

Na. 52

Migogoro Kati ya Wakulima na Wafugaji

MHE. MODESTUS D. KILUFI aliuliza:-

Migogoro kati ya wakulima na wafugaji ni tatizo kubwa nchini linalopelekea kupoteza maisha ya watu:-

(a) Je, ni lini Serikali itatenga maeneo ya wafugaji kama ilivyotenga maeneo ya wanyamapori?

(b) Je, kwa nini Serikali isiimarisha Soko la Mifugo na Mazao ya Mifugo na kutoa elimu kwa wafugaji juu ya matumizi bora ya mifugo?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 ambayo inalenga kutenga ardhi kwa ajili ya makundi mbalimbali, Serikali imeandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi yenye vijiji 479 kati ya Wilaya 69 kwenye Mkoa 21. Katika vijiji hivyo 479, jumla ya hekta 1,284,011.88 za maeneo ya malisho zimetengwa. Maeneo haya yaliyopimwa na kutengwa yanalindwa kisheria kupitia Sheria ya Maeneo ya Malisho na Rasilmali za Vyakula vya Mifugo namba 13 ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya mifugo kupitia mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Wilaya hizo na Wilaya nyingine kulingana na upatikanaji wa fedha. Maeneo haya hutengwa kulingana na mahitaji ya wafugaji na ni tofauti na utengaji wa maeneo ya wanyamapori ambapo mara nyingi maeneo hayo hutengwa kutokana na kuwepo kwa idadi fulani ya wanyama hao na kwa shughuli nyingine za kibinadamu kukatazwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, (b) ili kuimarisha na kuendeleza biashara ya mifugo hapa nchini Serikali imejenga jumla ya minada 322. Minada hi ni ya aina tatu ambayo ni minada ya awali 300, minada ya upili 12 na minada ya mipakani 10. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi nchini imeendelea kuimarisha biashara ya mazao yatokanayo na mifugo hususan nyama kwa kujenga viwanda, machinjio takribani saba za kati za kuchinja na kusindika nyama na bidhaa zake.

Aidha, viwanda 67 vya maziwa na vingine saba vinajengwa viwili vya ngozi vinajengwa hapa nchini.

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVU]

Kutokana na matumizi ya miundombinu hiyo, nchi yetu inaweza kufanya biashara ambapo kiasi cha tani 126,000.2 za nyama ya ng'ombe tani 667 za nyama ya mbuzi na tani 88.4 nyama ya kondoo zenye thamani ya Shilingi bilioni 28.8 ziliuzwa nje ya nchi katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi inaendelea kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa kisasa wenye tija ili wafugaji wanufaike kutokana na mifugo yao pamoja na mazao ya mifugo.

SPIKA: Mheshimiwa Kilufi, swali la nyongeza.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kama kweli yanayozungumzwa hapa kwamba kuna maeneo yametengwa, inakuwaje sasa hivi migogoro ya wafugaji inazidi kuongezeka? Lakini vile vile upo ushahidi kwamba wafugaji wamekosa maeneo yaliyoboreshwa na miundombinu na hivyo kuvamia maeneo ya wakulima kwa ajili ya kutafuta maji. Je, Mheshimiwa Waziri anatumie nini juu ya mgogoro unaoendelea kwa sasa kutokana na majibu ambayo ameyatoa na ni vijiji vipi na Wilaya zipi ambavyo vimetengewa maeneo haya anayoyataja?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVU:

Mheshimiwa Spika, maeneo haya kama nilivyoieleza, maeneo haya yanatengwa kutokana na upatikanaji wa fedha. Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi imetenga na inaendelea kutenga kutokana na upatikanaji wa fedha. Lakini niseme kwamba katika Halmashauri zote, Halmashauri ndizo ambazo zinatakiwa kufanya tathmini na kuonesha maeneo, kubainisha maeneo, kuyapima na kuyakabidhi kwa wafugaji na kuwawekea miundombinu ya mifugo ili waweze kutulia katika maeneo hayo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVU]

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ndizo ambazo zinaonesha uhitaji huo kwa kuona idadi ya mifugo ambayo wanayo na kushirikiana na Wizara yangu kutoa utaalumu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mifugo, lakini Wizara ya Ardhi ndiyo ambayo hasa yenye ardhi ya kutakiwa kupima na kuweka maeneo hayo ili wafugaji waweze kukabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mikoa ambayo imetengwa maeneo hayo ninayo hapa nitamkabidhi Mheshimiwa Mbunge pamoja na maeneo na Wilaya ambazo zimetengwa pamoja na idadi ya maeneo hayo ninazo nitamkabidhi Mheshimiwa Mbunge kwa rejea.

SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, muda umekwenda kabisa mpaka saa 5.00 na maswali yanapaswa kwisha saa 4.30 lakini tumefilka saa 5.00.

Kwa hiyo, naomba niwatambue baadhi ya wageni waliopo humu ndani. Kuna wanavikundi kumi wa kikundi cha Ngoga Mboga cha Dar es Salaam, hebu wasimame hao, mpo watatu tu! Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 120 na Mwalimu wao kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Dar es Salaam. Naomba wasimame walipo. Ahsante, karibuni. Kuna wanachuo 45 pamoja na wakufunzi wawili kutoka Chuo cha Ualimu cha *Mountesori* cha Mwanza, wasimame walipo. Ahsante, karibuni. Safari ndefu! *(Makofi)*

Wanafunzi 45 wanaosoma Udaktari kutoka Chuo cha *Saint Francis* cha Ifakara Morogoro. Naomba Madaktari hao wasimame walipo. Nafikiri wamekosa nafasi, watatuunga mkono baadaye. *(Makofi)*

Kuna wanamichezo 27 wanaoshiriki mashindano ya Halmashauri hapa Dodoma ambao ni watumishi kutoka Wilaya ya Misungwi. Naomba wasimame hawa wanamichezo. Ahsante, karibuni. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Tuna wanamichezo 44 wanaoshiriki mashindano hayo kutoka Wilaya ya Manyoni. Naomba wasimame. Ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanamichezo 28 ambao ni watumishi kutoka Halmashuri ya Uyui. Wasimame walipo. Ahsante, nawatakieni michezo miema. *(Makofi)*

Karibuni wengine ambao hatukuwataja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba wakutane, sijui kama leo saa 5.00 katika Ukumbi wa Pius Msekwa 'B', wamepeva ruhusa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji - Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.00 watakutana *Basement* hapo chini.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini - Mheshimiwa Mwambalasa, anaomba niwatangazie Wajumbe kwamba saa 7.15 watakutana katika Ukumbi wa Pius Msekwa, nadhani ziko kumbi nyingi, mtajua ni wapi; huyu hakusema ni upi.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa Shah, anaomba Wajumbe wa Kamati yao wakutane saa 7.15 wakutane katika Ukumbi Na. 227.

Halafu kutoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* - Mheshimiwa Iddi Azzan anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 2 kutokuwa na mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya timu ya Waheshimiwa Wabunge, *Bunge Sports Club* na timu ya *Trevo Port* kutoka Dar es Salaam. Mchezo huu utafanyika katika uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 10.00 jioni. Aidha,

[SPIKA]

mshindi wa mchezo huo atakabidhiwa kikombe na medali. Mechi hii ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki itakayofanyika mwezi Desemba nchini Uganda.

Hivyo hivyo kesho timu ya *netball* ya Bunge itacheza na timu ya Makonda kutoka Zanzibar siku hiyo hiyo Jumamosi, sijui ni wakati gani, hawakutaja. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kwenda kuisindikiza timu yenu. Katibu.

HOJA YA KUAHIRISHA SHUGHULI ILI KUJADILI MAMBO MUHIMU YA DHARURA

Maelezo ya Serikali kuhusu migogoro kati ya wafugaji na wakulima, Hifadhi na Wawekezaji; na maelezo ya Serikali kuhusu Operesheni Tokomeza Ujangili

SPIKA: Naomba nirudie maelezo niliyotoa mwanzoni kwamba tarehe 30 Oktoba, 2013, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Kigola, kwa kuzingatia kanuni ya 47 na kanuni ya 55 ya kanuni za kudumu za Bunge, toleo la 2013 waliomba Bunge liahirishe shughuli zake ili lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma. Uamuzi wangu katika hoja hizo mbili ilikuwa kwamba Serikali ikazifanyie kazi na kuleta maelezo hapa Bungeni ili hatimaye Waheshimiwa Wabunge waweze kupata fursa ya kujadili hoja za Waheshimiwa Wabunge hao.

Kwa hiyo, tunachokifanya sasa ni kwamba Waziri wa Maliasili na Utalii atatoa maelezo, na Waziri wa Mifugo naye atatoa maelezo halafu tutaruhusu mjadala. Tutaendelea na mjadala mpaka saa 7.00, hatua nyingine tutaieleza kadri tunavyokwenda. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Kagasheki.

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwa utangulizi wa taarifa hii ya awali kuhusu Operesheni Tokomeza, niliruhusu nitaje yafuatayo:-

[WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye idadi kubwa ya tembo duniani kama tunavyosema sisi huku Bara na Zanzibar wanavyosema ndovu. Katika Afrika ni nchi ya pili kuwa na idadi ya tembo licha ya tembo wake kupungua. Katika miaka ya 1960, idadi ya tembo ilikuwa kati ya 250,000 na 300,000. Wingi wa tembo nchini ulichangiwa na juhudi za uhifadhi wa wanyamapori zilizotokana na kutenga maeneo makubwa kama hifadhi pamoja na ulinzi wa maeneo hayo. Takriban asilimia 80 ya tembo wa Tanzania wanapatikana katika maeneo yaliyohifadhiwa *co-protected areas* ambayo ni Hifadhi za Taifa (*National Parks*), Eneo la Hifadhi la Ngorongoro (*Ngorongoro Conservation Area*) na Mapori ya Akiba (*Game Reserves*). Asilimia 20 iliyobaki inapatikana kwenye Misitu ya Hifadhi (*Forest Reserves*), Mapori Tengefu (*Game Control Areas*), Maeneo ya Wazi (*General Land*) na kwenye ardhi za vijiji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za uhifadhi, kumekuwa na changamoto zinazotishia uhai wa maliasili zetu. Moja ya changamoto hizo ni ujangili wa tembo ambapo katika vipindi tofauti wamekabiliwa na tishio la kutoweka. Tukio la kwanza kubwa ni lile la miaka 1970 na 1980 ambapo idadi ya wanyama hao ilipungua kwa asilimia 72 kutoka 203,000 mwaka 1977 hadi 57,334 mwaka 1991. Maeneo yote yaliyohifadhiwa yaliathirika kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Pori la Akiba *Saleou* lililokuwa na tembo wengi zaidi lilipoteza asilimia 50 ya tembo wake na hifadhi ya Taifa ya Serengeti ilibaki na asilimia 20 tu.

Katika kipindi hiki Tanzania ilipoteza zaidi ya asilimia 90 ya Faru, mnyama mwingine mkubwa ambaye amekuwa akiwindwa kwa sababu ya pembe yake. Kufuatia janga hili, mwisho wa mwaka 1980 Serikali ilitangaza operesheni kubwa iliyojulikana kama Operesheni Uhai iliyojumuisha vyombo vya dola likiwemo Jeshi la Wananchi na Askari wa Wanyamapori. Tatizo la ujangili lilidhibitiwa kwa kiwango kikubwa na tangu wakati huo idadi ya tembo ikaanza kuongezeka tena. Idadi iliyoongezeka kufikia 130,000 mwaka 2002. Tatizo kubwa la ujangili limejitokeza tena miaka ya karibuni ambapo mwaka 2009 idadi ya tembo ilishuka hadi 109,000. Hii inaondoa kabisa

[WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

matumaini ya ongezeko la wanyama hao na inatishia kutoweka kwa kiumbe huyo nchini kama hatua madhubuti hazitochukuliwa kudhibiti tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko kubwa la ujangili nchini, Waheshimiwa Wabunge, wasomi, wananchi kwa ujumla, wanaharakati walitaka Serikali kutumia Jeshi kukomesha janga hili la ujangili. Wabunge ndani ya Bunge na nje ya Bunge mara kadhaa wameshauri na kusisitiza kwamba Jeshi la Wananchi ndiyo tegemeo kubwa katika kupambana na ujangili hapa nchini. Ilidhihirika wazi kwamba wanyama hawa watatoweka na lawama zitajitokeza kutoka vizazi vijavyo. Vivutio vya Tanzania ni pamoja na tembo, ikifahamika kwamba kutokana na vivutio hivi Tanzania inayo nafasi kubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua kadhaa kudhibiti tatizo la ujangili wa tembo na wanyama wengine nchini. Hata hivyo, katika miaka ya karibuni, tatizo la ujangili wa tembo limeongezeka kutokana na kuwepo kwa soko kubwa katika nchi za Mashariki ya mbali. Aidha, uchache wa watumishi katika Sekta ya Maliasili, kushuka kwa maadili miongoni mwa watumishi wa Serikali na raia wengine wimbi la wageni wengi kutoka katika mataifa yenye maeneo ya tembo pamoja na urahisi wa kufika kwenye maeneo yenyewe yenye tembo kulitokana na kuimarika kwa miundombinu na urahisi wa mawasiliano kama simu za kiganjani kumechangia kuongezeka kwa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, hali halisi, imetulazimu tufanye operesheni nyingine ambayo inajulikana kwa jina la Operesheni Tokomeza. Hii Operesheni ilianza tarehe 4 Oktoba, 2013, uhalali wa Operesheni Tokomeza unatokana na sababu nyingi zikiwemo:-

- (i) Ulazima au umuhimu wa kunusuru uchumi wa nchi kwa kuathiri Sekta ya Utalii;
- (ii) Umuhimu wa kutunza na kuendeleza ikolojia ya maeneo yaliyohifadhiwa;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

- (iii) Umuhimu wa kutunza fursa za kisayansi na kitaalam zinazotokana na wanyamapori na viumbe hai wengine;
- (iv) Umuhimu wa kulinda heshima ya Taifa letu mbele ya jumuiya ya Kitaifa kwa kuuthibitishia ulimwengu kuwa tuna nia ya dhati ya kupambana na ujangili hapa nchini; na
- (v) Umuhimu wa wito, wawakilishi wa wananchi kuitaka Serikali itumie uwezo wake kukomesha na kutokomeza ujangili.

Makao Makuu ya Operesheni Tokomeza yako katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi na nchini hapa imegawanywa katika kanda 12 za utekelezaji kama ifuatavyo:-

- (i) Saleou, Mikumi, Udzungwa, Lukwika, Lumesule, na Liparamba;
- (ii) Buringi - Biharamulo, Ibanda – Rumanyika, na Rubondo;
- (iii) Moyowosi, Ugala na Luganzu;
- (iv) Serengeti, Loliondo, Maswa, Ikorongo na Kijereshi;
- (v) Kilimanjaro, Arusha, Mkomazi, Umba, Simanjiro na Longido;
- (vi) Tarangire - Manyara, Karatu - Ngorongoro, Swagaswaga na Mkungunero;
- (vii) Rungwa, Ruaha, Mpanga, Kipengele;
- (viii) Rukwa, Lukwati - Katavi, Lwafi, Piti na Wembere;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

- (ix) Mahale na Gombe;
- (x) Saadan na kwenye maeneo yenye misitu ya mikoko;
- (xi) Pori Tengefu la Handeni, Kilindi na Mkinga; na
- (xii) Msitu wa Kazi Mzumbwi, Kisarawe, Rufiji na Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi kumekuwa na mafanikio ya kukamata vitu mbalimbali katika operesheni hii kama ifuatavyo:-

Yamekamatwa meno ya tembo, bunduki za kijeshi, bunduki za kiraia, risasi aina mbalimbali, watuhumiwa; ng'ombe, meno ya ngiri, mikia ya wanyama mbalimbali, ngozi za wanyama mbalimbali, pembe za swala tomi, mkaa, mbao, magogo, misumeno, mitengo ya wanyama, baiskeli, pikipiki na magari. Kwa kuwa taarifa hii ni ya awali, taarifa rasmi itatoa idadi kamili ya vitu vilivyokamatwa kwa tarakimu zake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii operesheni ni kubwa na ya Kitaifa, yapo yanayosemekana kutendeka ambayo hayakubaliki kama vile uonevu, unyang'anyi, mateso, uuwaji na hao watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa napokea taarifa kwa wananchi na bado nasisitiza tuzidi kuletewa taarifa ili tuzifanyie kazi na Serikali haitasita kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika siku chache za majadiliano ndani ya Bunge hili, Waheshimiwa Wabunge wameleta kilio kizito kuhusu mwenendo wa Operesheni Tokomezwa. Nafurahi kuona hakuna aliyeipinga operesheni, wengi walichokikataa ni mwenendo wa operesheni yenyewe. *(Makofi)*

Kutokana na kilio hicho, Serikali inatamka yafuatayo:-

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]

(i) Hapa Bungeni naomba nirejee agizo kwa Kamanda wa Operesheni lililotolewa mwezi Oktoba, 2013 kwamba mifugo yote iliyokamatwa ndani ya hifadhi kabla ya operesheni tokemeza haijaanza na mwanzo wa operesheni iachiwe na wenye mifugo yao wapewe bila malipo yoyote au adhabu yoyote. *(Makofi)*

Hakuna tunachokiomba, wakishaachiwa hao ng'ombe hakuna kurudi tena katika hifadhi.

(ii) Mifugo ambayo imekamatwa ndani ya hifadhi na bado imo ndani ya hifadhi, iachiliwe mara moja, lakini hakuna kurudi tena ndani ya hifadhi. *(Makofi)*

(iii) Wale wote ambao mifugo yao imepigwa risasi na wana vielelezo, wanilettee na tutachukua hatua kwa sababu nimeambiwa kwamba vielelezo vipo ingawaje mimi sijaviona. *(Makofi)*

(iv) Litakuwa jambo la busara kufanya tathmini ya Operesheni Tokomezi. Tutafanya tathmini hii tuweze kupata picha kubwa ya operesheni nzima kwa kutembelea maeneo mbalimbali na kusikiliza kauli za wananchi na kushuhudia yaliyotokea katika maeneo huko kwa wananchi.

Kwa kuwa yako malalamiko mengi kutoka kwa Wabunge kuhusu mwenendo mzima wa operesheni hii, ni lazima hatua stahiki zichukuliwe kwa wote waliokiuka utaratibu na maagizo ya operesheni. Hatuna jinsi, lazima tathmini ifanyike. Naomba Waheshimiwa Wabunge wawe na imani kwamba tathmini hii itafanyika na itakabidhiwa Bungeni, kupitia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, Operesheni Tokomeza itasitishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante, sasa namwita Waziri wa Mifugo na Uvuvi.

WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya Bunge, namba 49(1)(2) ya kanuni za kudumu za Bunge toleo la 2007, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo ya Serikali kuhusiana na migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, siku ya Jumatano, tarehe 30 Oktoba, 2013, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, alisimama kwa kutumia kanuni 55(3)(e) iliyosomwa pamoja na kanuni 47(1)(2)(3) akikuomba wewe Mheshimiwa Spika kuahirisha shughuli za Bunge zilizokuwa zikiendelea ili kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma. Jambo hilo ni migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi inayoendelea sehemu nyingi nchini pamoja na athari zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Nkumba kutoa hoja yake, uliagiza Serikali ikafanyie kazi masuala hayo na kuyatolea maelezo hapa katika Mkutano huu wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa maelezo ya Serikali kuhusu wafugaji kuhamahama na adha mbalimbali zinazowakumba wakati wa kuhama wanapotafuta malisho na maji.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya wafugaji yamekuwa yakipungua mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, idadi ya mifugo, wanyamapori, kilimo na mahitaji mengine ya ardhi. Maeneo mengi ya wafugaji hususan yale yaliyokuwa yakitumika kama kimbilio wakati wa ukame, yamebadilishwa matumizi na mengine yamegeuzwa kuwa hifadhi, Mbunga za wanyama, makazi ya watu, kilimo na miundombinu. Hivyo, kubadilishwa kwa matumizi ya maeneo mbalimbali yaliyokuwa yakitumika kwa ajili ya ufugaji, pamoja na mabadiliko ya tabia nchi, vimechangia

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVU]

migogoro mingi kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 2005 hadi 2013, nchi yetu imekumbwa na vipindi kadhaa vya ukame vilivyoathiri sana ufugaji kutokana na kukosekana kwa maji na malisho. Mikoa iliyoathirika zaidi ni pamoja na Mkoa wa Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara, Arusha, Manyara, Morogoro, Singida, Dodoma, Tabora na Kilimanjaro. Ili kuinusuru mifugo yao, wafugaji walihamia Mikoa mingine, au Wilaya nyingine za Mkoa huo huo zilizokuwa na unafuu katika upatikanaji wa maji na malisho. Uhamiaji huo ulisababisha uharibifu wa mazingira kwenye maeneo ambayo ni vyanzo vya maji na hifadhi za Taifa.

Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na hifadhi ya wanyama pori la Burigi, Maswa, Meatu, Bonde la Usangu hasa eneo la lhefu na bonde la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uharibifu huo wa mazingira kuanzia mwaka 2006 na 2013, Serikali imetopa matamko mbalimbali ya kuondoa mifugo iliyoingia katika Vijiji na maeneo tengefu katika Mikoa ya Mbeya, Rukwa, Morogoro, Kagera, Simiyu, Shinyanga na Kigoma kinyume cha taratibu zilizowekwa na sheria za kuhamisha na kusafirisha mifugo kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine, zikiwemo sheria zifuatazo:-

Sheria ya Magonjwa ya Mifugo ya Wanyama Sura namba 156; Sheria ya Hifadhi za Mazingira ya Mwaka 1994; Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974 ambayo imefanyiwa *revision* mwaka 2008; Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999; Sheria ya Mipango ya Matumizi bora ya Ardhi ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kumefanyika *operation* mbalimbali nchini zenye majina tofauti. Operesheni hizi ni pamoja na Operesheni ya lhefu, Operesheni ya Ondoa Mifugo Morogoro na Rukwa, Operesheni Kimbunga na Operesheni Tokomezwa Ujangili.

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]

Utekelezaji wa Operesheni umefuatia matamko na mikakati mbalimbali iliyotolewa na Serikali. Hata hivyo, wakati wa kutekeleza maelekezo hayo ya Serikali katika maeneo mbalimbali nchini, yamejitokeza malalamiko mengi kutoka kwa mfugaji mmoja mmoja, kupitia kwa Waheshimiwa Wabunge hapa Bungeni na kwa kupitia umoja wa wafugaji, wakidai kwamba Operesheni hizo kutofanyika vizuri.

Baadhi ya maeneo yaliyolalamikiwa ni pamoja na utozaji wa *fine* za viwango tofauti, zinazodaiwa kuwa ni kubwa na kuhoji uhalali wa misingi ya viwango hivyo kisheria. Vilevile yamekuwepo malalamiko ya unyanyasaji, uombaji wa rushwa na dhuluma na kutopewa nafasi ya kujitetea.

Mheshimiwa Spika, wafugaji kuhama kutoka eneo moja kwenda lingine, ni mbinu mojawapo ya kunusuru mifugo yao kutokana na ukame, milipuko ya magonjwa, migogoro ama kubadilisha mazingira. Kuhamisha mifugo ni mkakati wa kufuatilia rasilimali za maji na malisho pamoja na chumvi chumvi, ambazo hazipatikani maeneo yote kwa wakati wote na huduma muhimu za watu na mifugo. Jambo hili linafanyika kwa kuzingatia ibara ya 17 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayotoa haki kwa raia yeyote wa Tanzania kwenda kuishi mahali popote nchini bila kuvunja sherai za nchi.

Hata hivyo, matatizo kadhaa yanaweza kutokea wakati wa kuhama, ikiwa ni pamoja na kutokea kwa migogoro kati ya wafugaji, wakulima na kusambaza magonjwa ya mifugo na mifugo kufa kutokana na kutozoea mazingira mapya.

Mheshimiwa Spika, ni kinyume cha taratibu kwa mfugaji kuhamisha mifugo yake kwenda Mkoa, Wilaya, Tarafa, Kata au Kijiji kingine pasipo na kibali cha maandishi cha kukubaliwa toka Mkoani, Wilayani, na Kijiji anachohamia. Pia, waraka wa Rais Na. (1) wa mwaka 2002, juu ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo, umetoa taratibu za wafugaji kuhamisha mifugo yao kutoka sehemu moja ya nchi kwenda sehemu nyingine ndani au nje ya Mkoa, Wilaya na Kijiji.

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVU]

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa mifugo katika kukuza uchumi wa Taifa letu, Serikali imeendaa Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, ambayo pamoja na mambo mengine, inatoa matamko ya kisera kuhusu kumwendeleza mfugaji, kuendeleza mifugo, kuboresha rasilimali za nyanda za malisho na miundombinu. Sera hii inatekelezwa kupitia *program* ya kuendeleza Sekta ya Mifugo na kusimamiwa na Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Rasilimali za Malisho na Vyakula vya Mifugo Sura Na. 180 na Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Sura Na. 156.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi za Serikali zinalenga kupunguza uhamaji kwa kuboresha mazingira ya ufugaji hususan miundombinu ya uzalishaji na masoko, maji, malisho, elimu kwa wafugaji, kosafu, nambari za mifugo, kinga dhidi ya magonjwa ya wanyama na kuendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, pametokea migogoro mikubwa kati ya wafugaji na wakulima katika maeneo mbalimbali hapa nchini hususan katika Wilaya ya Kilosa, Mvomero, Kilombero, Chunya, Kondo, Kisarawe, Bagamoyo, Babati, Igunga, Chato, Biharamulo, Maswa, Geita, Bukombe, Uvinza na maeneo mengine hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kinachoonekana kuendeleza migogoro hiyo, hususan katika baadhi ya Wilaya nilizozitaja, ni wafugaji kuendelea kupeleka mifugo yao kutoka maeneo mengine wakielewa kuwa kuna maeneo ambayo yako wazi na ya malisho na maji ya kutosha kwa ajili ya mifugo yao. Aidha, baadhi ya watendaji wanaruhusu wafugaji kuhamisha mifugo yao bila kujali kama inakohamishiwa mifugo bado kuna maeneo ya kutosha kupokea mifugo. Kadhalika, baadhi ya viongozi wa vijiji wanaruhusu mifugo kuingia katika maeneo yao bila kuzingatia kwamba, idadi iliyopo ya mifugo inalingana na uwezo wa maeneo ya malisho waliyopo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara yangu kutoa maelekezo kwa Mikoa na Wilaya kuzingatia taratibu za kuhamisha mifugo, na pia kutoa taaarifa kwa umma kupitia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVU]

vyombo vya habari, jambo ambalo nililifanya Juni, 2012, bado tatizo la kuhamisha mifugo kiholela ni kubwa na sababu kubwa ya migogoro kati ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya aina ya pili ni ile iliyotokea kati ya Wafugaji na maeneo ya hifadhi na mbunga za Wanyama na maeneo mengine tengefufu. Kama tunavyofahamu maeneo haya yanasimamiwa na sheria mbalimbali ili kuyalinda na kuyahifadhi. Hata hivyo, kutokana na sababu nilizozieleza awali za kuhamisha mifugo, wafugaji mara nyingi hukimbilia huko ili kunusuru mifugo yao kutokana na ukosefu wa malisho na maji. Kwa bahati mbaya sana, na pengine bila kuelewa, baadhi ya watendaji wamewaondoa wafugaji katika maeneo hayo kwa kutumia nguvu za ziada hata kufikia kuwajeruhi wafugaji na mifugo yao. Kwa vyovyote vile, jambo hili sio jema na Serikali inalikemea jambo hili maana Serikali yetu inaendeshwa kwa sheria. Kwa hiyo, tunatarajia ukiukwaji wowote wa Sheria utashughulikiwa kwa ustaarabu kulingana na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuwapa pole na kuwaomba radhi wale wote waliopata usumbufu kwa namna moja au nyingine, hususan katika kupoteza mifugo yao, mazao yao ama kujeruhiwa kutokana na *operation* hizo. Aidha, Serikali inaendelea na itaendelea kuchukulia hatua watendaji walijihusisha na watakaojihusisha na vitendo hivyo viovu.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali za kukabiliana na tatizo la wafugaji kuhamahama, miundombinu imeendelezwa kwa kuchimba jumla ya malambo 1,378 na visima virefu 85,000. Aidha, katika mikakati ya kuendeleza malisho, jumla ya hekta milioni 1.2 zimepimwa na kutengwa kwa ajili ya malisho katika vijiji 479 vya Halmashauri 69, Mikoa 21 na zoezi hili ni endelevu kutokana na upatikanaji wa fedha. Pia, Serikali kwa mwaka 2013, imepanga kuchimba malambo na kuweka miundombinu ya mifugo katika maeneo inakohamia mifugo katika Wilaya za Chunya, Lindi na Rufiji na Wilaya zenye mifugo mingi yaani Kilindi, Kiteto, Maswa na Same.

[WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI]

Mheshimiwa Spika, mpango huu utakuwa endelevu kwa kuzishirikisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ili hatimaye wafugaji watulie sehemu moja yenye maji na malisho ya kutosha na hivyo kuondokana na kuhama hama.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wanahamizwa na kukumbushwa kuzingatia kufuga mifugo kulingana na maeneo yaliyopo na ambayo yatakuwa yameanishwa, ili yaendelezwe kama ilivyoainishwa kisheria na Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 pamoja na Sheria ya Rasilimali za Malisho Vyakula vya Mifugo Sura Na. 180. Serikali itaendeleza jitihada zake za kutoa elimu bora ya ufugaji na kusambaza mbegu bora za mifugo kwa wafugaji kwa kutumia uhimilishaji ili wafugaji wawe na mifugo bora na kuanisha kutenga na kupima maeneo kwa ajili ya ufugaji.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni ongezeko la idadi ya mifugo ikilinganishwa na kasi ya uvunaji. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali inaendelea kuhamasisha na kuhimiza sekta binafsi, kujenga viwanda vya kusindika nyama na mazao yake ili kuwapatia wafugaji soko la uhakika. Hadi hivi sasa kuna viwanda saba hapa nchini vya kusindika nyama na bidhaa zake. Aidha, Wizara inawapongeza wawekezaji waliojitokeza kuanzisha viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya Shinyanga na Mwanza na kutoa wito kwa wawekezaji wengine kujitokeza zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuchukua nafasi kukushuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kuwasilisha maelezo haya ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante. Tumesikia maelezo kwa Wizara hizi mbili. Kabla sijaita mchangiaji wa kwanza, naomba nitangaze kwanza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala
- Mheshimiwa Pindi Chana, anaomba Kamati yake saa 7.00

[SPIKA]

mchana wakutane katika Ukumbi Na. 219. Naomba Makatibu wenu walete matangazo mapema na siyo baada ya hapo.

Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji mko zaidi ya mia moja na kitu. Kwa sababu suala hili, hapa tunapozungumza sasa hivi ni kujaribu ku-*air our views* kidogo, lakini bado kazi inaendelea. Kwa sababu bado itabidi turudie, kama hili suala la Operesheni Tokomezwa itabidi lirudiwe kwa undani zaidi na hilo lingine nalo itabidi lifanyiwe kazi kwa undani zaidi. Kwa hiyo, hapa nitatumia saa moja na nusu tu, mpaka saa 7.00 tunaahirisha.

Kwa hiyo, nitaita kwa Vyama halafu basi tena. Yaani nitakwenda kwa *portion* za Vyama, kwa sababu bado tutarudia kwa ukamilifu zaidi. Hapa sasa hivi bado tunajaribu kuunga mkono dharura walizozileta wale wenzetu.

Halafu lingine naomba niseme, wale walioomba tuahirishe Bunge, hoja yao ilikuwa ni kuomba tuahirishe Bunge ili tujadili suala la dharula. Hawakuwa na hoja zaidi ya hiyo. Kwa hiyo, hakuna wa kufunga hapa, ndiyo kanuni zinavyosema.

Kwa hiyo, nitamwita kwanza Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, atafuatiwa na Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Dkt. Titus M. Kamani, halafu Mheshimiwa Said A. Arfi na wengine wachache nitawataja baadaye. Dakika ni kumi.

MWENYEKITI WA KAMATIYA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa shukurani kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika suala hili zima la migogoro ambayo imedumu kwa muda mrefu kati ya wafugaji na wakulima. Migogoro kati ya wafugaji na wakulima imedumu kwa muda mrefu, kuanzia miaka ya 1960 na imeendelea mpaka sasa.

Kadri ya idadi ya watu ilivyokuwa inaongezeka na idadi ya mifugo kiongezeka, migogoro hii nayo vile vile

[MWENYEKITI WA KAMATIYA KILIMO, MIFUGO NA MAJI]

imeongezeka. Lakini tatizo limezidi kuwa kubwa zaidi, kuanzia Desemba, 2008, ambapo Serikali iliagiza kwamba mifugo iliyokuwa katika sehemu za vyanzo vya maji, sehemu tengefu na maeneo mengine, hususan katika Mikoa ya Morogoro na Rukwa na maeneo mbalimbali sehemu za Pwani, kwamba ihamishwe na kupelekwa mahali pengine.

Baada ya agizo hilo la Serikali, utekelezaji wa agizo hilo ulianza kutekelezwa mara moja. Kwa bahati mbaya sana, utekelezaji wa suala hili haukuwa umepangwa vizuri, na hivyo ulileta matatizo mbalimbali kwa makundi mbalimbali ya wafugaji. Haya matukio tumekuwa tukiyasikia katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu; yalianza katika sehemu chache na katika siku za hivi karibuni yamekuwa katika sehemu nyingi sana.

Tukio la sasa; tarehe 29 na 30 Oktoba, 2013, makundi tofauti ya wafugaji kutoka sehemu mbalimbali hapa nchini yalifika hapa Dodoma kwa lengo la kuwaona Wabunge na vilevile kwa lengo la kumwona Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi Taifa - Mheshimiwa Kinana, ili kueleza matatizo ambayo amekuwa akikumbana nayo katika zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine.

Mikutano iliofanywa ilifanywa tarehe 29 na 30 Oktoba, 2013 na baadhi ya Wabunge walihidhuria. Wafugaji walieleza kwa masikitiko makubwa matukio mbalimbali ambayo walikumbana nayo katika kutekeleza haya, katika zoezi la kuwahamisha wafugaji kutoka eneo mojawapo na kwenda katika eneo lingine.

Kubwa walilosikitishwa nalo ni kwamba zoezi la kuhamisha, wafugaji kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine lilianza wakati agizo hilo lilikuwa limesitishwa kuanzia tarehe 30 Aprili, 2009; wakati Serikali ilisema ilikuwa inazidi kutafakari utekelezaji wa jambo hilo baada ya malalamiko mbalimbali. Sasa mambo ambayo yamewakera sana wafugaji na ambayo yaliwafanya baadhi ya viongozi, Waheshimiwa Wabunge kuleta hoja ya kuomba Bunge

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI WA KAMATIYA KILIMO, MIFUGO NA MAJI]

liahirishe shughuli zake na kujadili jambo la dharura ni mambo yafuatayo:-

Kwanza, wafugaji wanasema matayarisho ya zoezi ya kuwahamisha wafugaji kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine hayakuwa na matayarisho ya kutosha na utekelezaji wake haukuwa makini. Wafugaji waliambiwa ondokeni kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine na kule ambako walikuwa wanakwenda hawakujua kama kulikuwa na matayarisho kwa maana ya malisho, maji, miundombinu na huduma nyingine za afya. Baadhi ya wafugaji hawakufika kule walikotakiwa kwenda, kwa sababu kulikuwa hakuna msimamizi yeyote katika shughuli hiyo.

Pili, migogoro hii kama walivyoeleza Mawaziri waliotoa kauli, ilihusisha makundi mabalimbali, nisingetaka kuyarudia lakini husasan kati ya wafugaji na wakulima. Lakini kumekuweko na athari mbalimbali za uvunjifu wa amani, uharibifu wa mali za wafugaji na wakulima kwa maana ya mifugo na mazao na kwa nyakati tofauti, baadhi ya wananchi wamepoteza maisha yao na hasa katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga, Mbeya, Rukwa, Katavi, Tabora na Kagera.

Tatu, mifugo mingi imekamatwa katika maeneo mbalimbali, na wale waliokuwa wanasimamia Operesheni na kufungiwa katika mazizi. Ili uweze kukomboa mifugo yao, ilibidi walipe *fine*. *Fine* hiyo kwa ng'ombe ilikuwa kati ya Sh. 10,000/= mpaka Sh. 50,000/= na kwa mifugo midogo kama mbuzi na kondoo, tozo yake ilikuwa kati ya Sh. 5,000/= na Sh. 10,000/=. Wafugaji wengi wana mifugo mingi sana.

Mheshimiwa Spika, kama mtu mmoja anaweza kulipa Sh. 50,000/= kwa ng'ombe na uchukue mathalani ng'ombe 300 tu, *fine* aliyokuwa analipa ilikuwa ni kubwa sana. Watu hawa wamekuja na wameleta risiti walizokatiwa na mamlaka mbalimbali zilizokuwa zinasimamia zoezi hili. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P.M. MSOLLA]

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafugaji wengi walikuwa hawana fedha za kukomboa mifugo yao ambayo ilikuwa inatozwa kwa gharama kubwa sana, wengi wao wallazimika kuuza mifugo yao kwa bei ya kutupwa, bei ya chini kabisa ili kusudi angalau waweze kukomboa mifugo yao michache. Wanasema, katika zoezi lile kulikuwa na wanunuzi tayari kama vile walikuwa wamepangwa, kwamba wanaposema uza mifugo yako, kuna mtu wa kununua yuko hapohapo na ananunua kwa bei nafuu kabisa, ili kusudi waweze kulipia baadhi ya mifugo waweze kuondoka nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, mifugo iliyoziidi kukaa kwenye mazizi ya Serikali ambapo mwenye mifugo alikuwa bado anatafuta fedha ilibidi kulipa tozo kwa kila siku ya ng'ombe au mfugo wake ulioendelea kulala katika zizi lile. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa kwa wafugaji walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wafugaji kama walivyosema wazungumzaji wengine, hawakupewa nafasi ya kujitetea kwamba wao kabla ya oparesheni hiyo walikuwa pale na walikuwa wanaishi kihalali.

Mheshimiwa Spika, kuna madai ya jumla ya unyanyasaji, kupigwa, kutishiwa, kutukanwa na kuporwa mali. Katika sehemu nyingi, waliamuriwa waondoke na wanaambiwa rudini kwenu. Hawa ni Watanzania, wanachojiuliza kwao ni wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa ni Watanzania, wanaruhusiwa kisheria kuishi mahali popote ili mradi wamefuata taratibu. Sasa wanasema tukimbilie wapi, ndiyo maana wamerudi kukimbilia kwa watetezi wao Wabunge ili kusudi waweze kuliona jambo hilo kwa upana. Aidha, kwa nyakati tofauti, mifugo imechinjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hayo yaliyotokea na kwa kuzingatia kwamba migogoro kati ya wakulima na wafugaji imedumu kwa muda mrefu bila ufumbuzi na kwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P.M. MSOLLA]

kuwa suala hili ni la kisera na linahusisha Wizara mbalimbali na ili kudumisha amani na utulivu katika jamii yetu, ninakusudia kuleta hoja ya kuunda Kamati Teule chini ya Kanuni ya 120(2)(a) ambayo itamruhusu Katibu ili apange nafasi kwa mujibu wa Kanuni 30(4) ili kusudi Bunge liweze kujadili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema hamtaweza kuchangia wote, mko wengi mno, kama tukikubaliana hoja hii, tutarudia tena kujadili. Mheshimiwa Nkumba!

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia fursa hii. Kwanza kabisa, naendelea kuwapa pole Watanzania wote waliokumbwa na kadhia hii mbaya, lakini naomba niweke msimamo wangu kwamba haiwezekani mpaka mambo yanakuwa makubwa kiasi hiki, watu wanaathirika huko, mali zao zinaathirika, uhai wa wananchi unapotea, ndiyo Serikali inakuja hapa kutoa maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba kazi ya Serikali ilikuwa kuendelea na hili zoezi walilokuwa nalo, mambo yameharibika, sasa naomba Bunge lichukue nafasi yake kama alivyotoa maelezo Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo. Ni vizuri Bunge hili likaunda Kamati ambayo kwa kweli itakwenda kufanya kazi ya uchunguzi kwa kina halafu baadaye ndiyo Serikali ije ilifanyie kazi jambo hilo. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. J. NKUMBA]

Mheshimiwa Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji nchini hapa ni ya muda mrefu na Serikali kila wakati imekuwa inatueleza hapa suala la upangaji wa matumizi bora ya ardhi. Haya yameendelea kuwa mambo ambayo yako kwenye makaratasi, lakini huko vijijini kuna matatizo chungu nzima. Wakulima na wafugaji hawaelewani na migogoro hiyo inaendelea kila wakati. Mambo haya yanafika mahali Serikali badala ya kutatua tatizo, kila siku Serikali imekuwa inakwenda kutatua ugomvi wa wakulima na wafugaji kwa kutumia bunduki, kwa kutumia mabomu, hatuwezi kuendelea na utaratibu wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wetu wamepata athari kubwa sana katika maeneo mbalimbali nchini. Ng'ombe wamepigwa risasi, mali zimepotea na wananchi wamekufa. Mbaya sana hawa waliokuwa wanafanya operesheni hii, wamekuwa wakitumia maneno mabaya, wanasema sisi hatuwezi kuhojiwa na mtu yeyote, tumetumwa na Ikulu, tumetumwa na uongozi wa juu. Nataka niulize, hawa watu walitumwa kweli na Mheshimiwa Rais kutumia utaratibu wa namna hii? Walitumwa kweli na Serikali? *(Makofi)*

Halafu ninyi viongozi, Mawaziri mnaosimamia sekta hizi mmewaacha hawa watu wanakwenda kufanya vurugu, wanakwenda kuondoa hali ya amani na utulivu wa wananchi wetu, wanakwenda kuuu mifugo, wanakwenda kuuu watu!

MBUNGE FULANI: Shame!

MHE. SAID J. NKUMBA: Leo hapa mnatuletea taarifa, mimi sikubaliani na taarifa hii ya Serikali. *(Makofi)*

WABUNGE FULANI: Waongo!

MBUNGE FULANI: Waondoke.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Maliasili na Utalii, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nataka niseme, mnazo hoja za kujibu kwenye Chama chenu na wote mnatoka CCM, mna hoja za kujibu kwenye Chama chenu Chama cha Mapinduzi. Vilevile mnazo hoja za kujibu kwa aliyewateua, aliyewatuma, Mheshimiwa Rais, hakuwatuma mambo myaache yaharibike kiasi hiki. Nataka niseme ndugu zangu, wananchi wamekasirika sana na sisi Wabunge hapa kwa sababu tunasimamia maslahi ya wananchi, kwa kweli katika jambo hili, hatuko pamoja na viongozi ambao kwa kweli wanazembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu, kwa kweli, nimekasirika sana na ukikasirika hata ile nidhamu ya kuzungumza inaweza ikakosekana.

MBUNGE FULANI: Sawasawa!

MHE. SAID J. NKUMBA: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie, katika maeneo mbalimbali nchini, wananchi wamepoteza mali zao, lakini wapo ambao kwa kweli wameshiriki kusababisha uharibifu mkubwa wa mali, lakini vilevile baadhi ya wananchi wetu kupoteza maisha. Nataka niseme kwamba imekuwa ni mazoea, haya maelezo yanayotolewa hapa, hawa waliohusika watachukuliwa hatua za kisheria, baadaye mambo yakishapoa, yamepoa. Naomba niweke kwenye rekodi kwamba jambo hili kama ambavyo Serikali imeji-*commit* hapa, kwamba watakaobainika watachuliwa hatua, tunataka tupate taarifa ni akina nani waliochukuliwa hatua juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, hii operesheni iliyokuwa inaendelea ya kusaka majangili, napenda vilevile Serikali baadaye ije itupe taarifa kwamba majangili wakubwa ambao kwa kweli ndiyo wanaofanya biashara hii, ni majangili wangapi waliokamatwa. Maana operesheni kubwa hii imekwenda kuwasumbua wanavijiji huko ambao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. J. NKUMBA]

kwa kweli wanajishughulisha na shughuli zao za kiuchumi za kila siku lakini watu wanaohusika kununua pembe za ndovu kwenda kuuza nje, hawakuguswa katika jambo hili muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, kwa heshima kubwa na unyenyekevu mkubwa, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Lugola!

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kabla sijasahau, hizi taarifa mbili za Mawaziri wawili, zimetokana na shinikizo la Bunge lako Tukufu. Katika mazingira ambapo taarifa inatolewa kwa shinikizo, taarifa hizo zinakuwa zimejaa maneno matamu, ya kudanganya Bunge na ya kudanganya Watanzania. Taarifa hizi sizihitaji na wala sikubaliani na maelezo yote kwa ujumla wake yaliyotolewa na Mawaziri hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema sikubaliani nao, Mheshimiwa Waziri wa Mifugo, taarifa yako umeisoma yote, unasema unawapa pole wale waliopata usumbufu. Watu wamekufa, wewe unaita usumbufu! Mtu amekufa wewe unaita usumbufu! Taarifa gani ya namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wabunge sasa mnisikilize ili mjue ukubwa wa tatizo hili linalowakabili wafugaji katika nchi yetu. Tatizo hili halikuanza kutokana na hiii Operesheni ya Tokomeza Ujangili au Kimbunga, limeanza kwa muda mrefu, wafugaji wamekuwa wakilia, wanakosa mahali pa kupeleka kilio chao kwa sababu wamekuwa wakipuuzwa na Mawaziri wanaohusika na wafugaji hao. Leo unasema Operesheni Tokomeza Ujangili kumbe ni Operesheni Tokomeza Ufugaji! Ni operesheni ambapo ni miradi ya watu kujipatia utajiri. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

Mheshimiwa Spika, Mawaziri hawa wataponea wapi kama damu ya Dasu Rutaligura ambaye alikufa kule Kilombero haitaanguka juu yao? Mawaziri hawa wataponea wapi, kama damu ya Madirisha Luchagula aliyekufa kule Mlele, haitakuwa juu yao? Mawaziri hawa wataponea wapi kama Ndugu Baya Tambi wa Ulanga aliyekufa kwa kupigwa haitakuwa juu yao? Mawaziri hawa wataponea wapi kama damu iliyomwagika ya wafugaji watano kule Mtimbila Ulanga haitakuwa juu yao. Mawaziri hawa wataponea wapi kama wafugaji waliopata vilema vya kudumu, akiwemo Ruhende wa Kilema, akiwemo Afisa Tarafa wa Mpimbwe na Diwani Majimoto, ambao walipigwa na kujeruhiwa vibaya wakiwa wamekwenda kwenye msiba wa mfugaji huyu wa Mlele aliyeuwawa. Mawaziri hawa wataponea wapi kama wafugaji watano wa Mtimbila waliojeruhiwa na wakapata vilema kutokana na vitendo wanavyofanyiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Ihefu, wafugaji walikaomatwa na ng'ombe zao, wakawa wananyeshwa maji ya moto, maji ya pilipili na kulazimishwa kulalia mchanga uliochemshwa, Mawaziri hawa, Ulinzi, Maliasili na Utalii, Mambo ya Ndani pamoja na Mifugo na Uvuvi, wataponea wapi kutokana na vitendo hivi? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mkono wangu umesheheni *book* lenye vielelezo, kuna picha za ng'ombe walikuwa wanapigwa risasi. Zaidi ya ng'ombe 500 katika nchi hii wamepigwa risasi kuwashinikiza wafugaji watoe fedha ambazo hazistahili, Mawaziri hawa wataponea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushahidi uko hapa, hivyo vibali anavyovisema Waziri wa Mifugo na Uvuvi, wafugaji wamekuwa na vibali kusafirisha mifugo yao, lakini vielelezo viko humu, bado ng'ombe wao walikamatwa na wengine kupigwa risasi, Mawaziri hawa wataponea wapi?

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Bunda, eneo la Kawanga Tengefu, wawekezaji ambao wana kiburi, ambao

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

wameonekana wako juu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao wameonekana hakuna mtu anayewakemea, wakachukua ng'ombe 150 na kuwatumbukiza kwenye Mto Rubana, ng'ombe wote wakaenda mpaka Ziwa Victoria, Mawaziri hawa mtaponea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu litakubali maelezo ya Serikali kwamba Serikali ikatathmini, haiwezekani Serikali ambayo vyombo vyake, Jeshi la Wananchi, ushahidi upo hapa, wameua watu, Maaskari wa Wanyamapori, ushahidi upo wameua watu, pamoja na wawekezaji, haiwezi kutathmini watu ambao wamewashindwa kwa muda mrefu, kazi hii lazima ifanywe na Kamati Teule ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wafugaji hawa walikuja Dodoma kuonana na Wabunge wao, kutoa kilio chao baada ya Mawaziri hawa kushindwa kuwatekelezea yale ambayo yalikuwa yanawasibu. Hata hivyo, bado Waziri wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi anasema wafugaji hawa ni matapeli, wafugaji hawa tuwaogope, maana yake ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lazima Bunge hili lijadili mambo haya kwa upana wake ili tujue ni watu wangapi wamekwisha kufa mpaka sasa, ni ng'ombe wangapi ambao wamepigwa risasi, ni ng'ombe wangapi ambao wametozwa faini ambazo hazistahili na ni wananchi wangapi wana vilema, wananchi wangapi wamechomewa nyumba zao, wananchi wangapi wamebakwa katika operesheni hizi? Kamati Teule ndiyo italeta majibu ili Bunge lako Tukufu liweze kutoa maazimio stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati namalizia, najisikia vibaya sana, Mawaziri hawa kuendelea kutoa lugha zilezile, maelezo yaleyale kwenye Bunge hili, wakati matukio haya ni ya muda mrefu. Nina wasiwasi, kama hoja hizi zisingetolewa na Wabunge kwenye Bunge lako Tukufu, haya waliyoyaleta leo wangeyaleta lini? Mpaka sasa hakuna jangili hata mmoja

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

ambaye amebakwa, ambaye amepigwa risasi, ambaye nyumba yake imechomwa moto. Hakuna jangili hata mmoja ambaye amenyeshwa maji ya pilipili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndiyo sababu nikasema, kama si Mawaziri wenyewe wanaohusika katika mambo haya ya miradi hii ambayo ni operesheni ya kukamata ng'ombe na kupora, lazima wahusika wote wangekuwa wamekamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niwaombe Wabunge wenzangu, katika jambo hili tusimame imara, tushikamane ili tuweze kutatua kero hii ambayo ni ya muda mrefu ili wafugaji hawa tunaowahitaji na wana sekta muhimu, sekta ya ufugaji, lakini nashangaa Waziri anayehusika na sekta hii ameipuuza na ndiyo sababu hata mchango wake kwenye pato la Taifa ni wa kusuasua. Lazima tufike mahali Waheshimiwa Wabunge tusikubali maneno yaliyotolewa humu, maneno matamu, yaliyojaa kutuhadaa, lazima sisi wenyewe Wabunge twende *on the ground*, twende tuangalie nini kinatokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, nitaomba niwasilisha kitabu hiki kilichosheheni ushahidi na vitendo viovu na vichafu ambavyo vimekuwa vikifanywa. Jeshi la Wananchi, Askari wa Wanyamapori, pamoja na wawekezaji katika nchi yetu. Halafu nina barua nyingine nyingi ambazo wamekuwa wakiziandika kwenda kwa Wizara husika na zenyewe nitaziwasilisha. Kitabu hiki kimejaa pamoja na stakabadhi ambazo wamekuwa wakitozwa fedha nyingi, wakati mwingine wameshindwa, ng'ombe wao wamechukuliwa. Kuna vibali vya kusafirishia mifugo, viko humu, kuna picha za ng'ombe waliouawa kwa risasi.

Mheshimiwa Spika, nisikitike, juzi wakati tunaomba kujadili jambo hili kwamba ni la dharura, hukulipa umuhimu wa udharura na matokeo yake, vitendo hivyo viliendelea na ng'ombe wengine waliendelea kuuzwa, 330 kwa kumbukumbu tulizo nazo. Kwa hiyo, nakuomba, katika

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. N. LUGOLA]

masuala ambayo Wabunge tunasema ni ya dharura, yachukuliwe kwa udharura wake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Nakubali yote uliyosema isipokuwa taratibu inabidi zifuatwe.

Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Halima Mdee mta-share dakika 10.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi nchangie katika hoja hii iliyoko mbele yetu. Niwape pole Watanzania wote ambao wameathirika dhidi ya zoezi hili la kutokomeza majangili, lakini maisha yao yakatolewa chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali hii ambayo siyo sikivu.

Mheshimiwa Spika, haya yanayojiri siyo mapya, leo Bunge linatibu majeraha. Kauli hizi za kunyanyasa Watanzania zilianza kutolewa hapa Bungeni. Mheshimiwa Waziri Mkuu alinukuliwa katika Bunge hili akisema hawa watu ni kupigwa tu, lakini Mheshimiwa Kagasheki alizungumza akiwa Arusha na akaripotiwa na vyombo vya habari, kwamba hawa majangili mkikutana nao huko mmalizane nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachoendelea Mheshimiwa Waziri Kagasheki amesema leo kwamba wameanzisha magereza mbalimbali *(Guantanamo Bay)* na kwa kanda yetu ya Kaskazini wameanzisha katika Hifadhi ya Ngorongoro. Wameanzisha kwenye Kituo cha Polisi, wananchi wasiokuwa na hatia wanachukuliwa, wanapelekwa kule, wanatandikwa mpaka kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali hii naifahamu, ukiachilia mbali hawa wafugaji ambao ng'ombe wao wamepigwa risasi, nimejuliza sana, hivi Bunge hili ni lini tumetunga sheria ya kuuha wahalifu ambao hawajasikilizwa? Umetuhumiwa tu, unapigwa risasi, ni lini Bunge hili limetunga sheria kama hiyo?

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

Mheshimiwa Spika, naomba nisipoteze mada hii, ni kwamba kuanzia Waziri Mkuu afute kauli yake, Mheshimiwa Kagasheki ufute kauli yako na hawa Mawaziri waliohusika, kuanzia Waziri Mkuu na Mawaziri wake wote, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete awawajibishe, vinginevyo hatuwezi kuendelea katika hali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Babati waliathirika. Alifuatwa baba mmoja anaitwa Kibuga katika familia yake, akapelekwa Kituo cha Minjingu, akapelekwa Ngorongoro amekuta wenziwe wamefungwa vyuma, wananyanyaswa, wamevuliwa nguo, unageuzwa kichwa chini miguu juu, wanakupiga kwato, wanakuvunjavunja mpaka unapoteza maisha. Yule baba haikuishia hapo, mke wake akafuatwa kwenye familia.

Mheshimiwa Spika, akina mama wa Mkoa wa Manyara, akina mama wa Babati wanauliza, nawapongeza waliandamana siku ya tarehe 17 siku kifo cha mwanamama mwenzao kilipotokea, tangu lini wanawake wa Mkoa wa Manyara wanawinda tembo? Kwa sababu yule mama Emiliana ambaye hivi ninavyoongea ni wiki ya tatu yuko mochwari, wananchi wamekataa kuzika kwa sababu alifuatwa kwenye kazi zake za kuuza mboga, akapelekwa kwenye Hifadhi ya Tarangire, akapigwa, akavunjwawunjwa. Hivi ninavyoongea, mwili wake uko mochwari ya hospitali ya Mrara Babati, ametobolewa macho, ameumizwa, amechunwa ngozi na Maaskari wa Operesheni Tokomeza Majangili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini Waziri Mkuu na Mawaziri wake wanaohusika katika hizi sekta wasiondoke? Nawapongeza wananchi wa Mkoa wa Manyara, Babati na Galapo, wamekataa kumzika yule mama kwa sababu hakuhusika na uwindaji wa tembo, wala hajui kinachoendelea ni kutokana na kauli ya Mheshimiwa Kagasheki kwamba kila anayekamatwa akasulubiwe mpaka kufa. Hatuna sababu ya kukaa na hawa Mawaziri humu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. P. P. GEKUL]

ndani wakati Watanzania wasiokuwa na hatia wanapoteza maisha yao, mifugo wanauawa, wanaswagwa kwenye mito wafe.

Mheshimiwa Spika, tumeona hata Kigoma, mtu ambaye ana *block* yake ya mifugo (*ranch*), amelipa shilingi milioni 10 lakini kaandikiwa risiti ya shilingi milioni moja...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Bahati mbaya dakika zako tano zimeisha, Mheshimiwa Mdee!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza niseme kwamba katika maelekezo ama Maazimio ama hotuba ya Mheshimiwa Waziri, naomba Mawaziri wote wawili waongeze, wale watu wote ambao walihusika na mauaji ya wafugaji wakamatwe, fedha zote zirejeshwe. Kwa sababu mtu anatozwa faini kwa ng'ombe mmoja kwa siku moja kati ya Sh.80,000 mpaka Sh.150,000. Ng'ombe mmoja kwa siku moja. Sasa majibu ya haya mengine mnayo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, viongozi wanakwepa tatizo. Waziri wa Mifugo, Waziri wa Maliasili na Utalii, wanajua chanzo cha migogoro ya wafugaji na wakulima na hifadhi, ni hatuna mipango bora ya matumizi ya ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili suala hatujaanza kulizungumza leo, tumezungumza miaka mitano iliyopita. Ukirejea hotuba zetu, tumezungumza yote. Miaka 52 baada ya Uhuru, Waziri wa Mifugo kwenye kikao alichofanya na wafugaji kwa maneno yake ukurasa wa nne kwamba tatizo ni kutokutengwa kwa ardhi kwa ajili ya kuendeleza ufugaji na kutokuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi kunakosababisha adha kubwa kwa wafugaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo anakuja kutuambia hapa eti kuna hekta milioni 1.5 kwenye wakati anajibu swali asubuhi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. H. J. MDEE]

zimetengwa kwa ajili ya wafugaji, zipi? Kwa nini haya masuala hukuyaeleza wakati unazungumza na wafugaji? Ama ndio katika utaratibu uleule mkiwa mnatujibu hoja zetu mnapiga sanaa hapo wakati mnajua ukweli sio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, miaka 52 baada ya Uhuru, unaambiwa katika vijiji 12,000, ni vijiji 1300 tu vyenye mipango ya matumizi bora ya ardhi, asilimia 11 ya vijiji, miaka 52 ya Uhuru. Miji Mikuu ya Mikoa ni asilimia 10 tu, Miji Mikuu ya Wilaya, ni Wilaya 20 tu kati ya Wilaya zote. Tumetoa Hoja Binafsi, tuitake Wizara ya Ardhi ikafanye tathmini, tujue katika nchi hii kiwango cha ardhi wanacho wawekezaji, kipi kiko kwenye hifadhi, kipi kiko Serikalini ili tupange matumizi bora, hoja hiyo tuliitoa mwaka jana. Lengo lilikuwa kutafuta suluhu ya migogoro ya wafugaji ambao wamegeuka wakimbizi ndani ya nchi yao. Tunazungumzia Botswana ambao wana mifugo milioni mbili ambayo ndiyo inaendesha uchumi, sisi tuna mifugo zaidi ya milioni 40.

Mheshimiwa Spika, majibu ya hoja ile hayajaletwa, Spika ukaagiza mwezi wa nne umepita, ukaagiza Bunge la mwezi wa nane umepita, limeagizwa Bunge hili la mwezi wa 11, linapita, kwa nini? Kwa sababu Serikali na Wizara haijui ina ardhi kiwango gani ambayo inatumika kwa matumizi gani, hatujui. Sasa kama hatujui, hivi tuna uhalali wa kuongoza? Kama Serikali ambayo ina *network* ya kiusalama na kitaalam mpaka katika ngazi ya kitongoji, inahitaji mwaka mzima kupata takwimu ya kiwango gani cha ardhi; hiyo ni Serikali mfu...

MBUNGE FULANI: *A dead government.*

MHE. HALIMA J. MDEE: *You are dead. (Kicheko)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Kamani na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia suala hili la migogoro na operesheni. Naungana na mawazo ya wenzangu waliochangia na kwa sababu mimi si kashenamboni, sikuwaona wale waliochunwa au kutoswa kwenye maji, naomba nitoe mawazo yangu juu ya uendeshaji wa operesheni, imenisikitisha kweli yaani hapa nilipo nina hali mbaya. Uwezo wa Serikali yetu kuendesha *operation* ni wa hali ya chini mno. Haihitaji mtu kumchuna ngozi ili ujue kwamba yeye anauza pembe, pembe si zinauzwa Singapore? Sasa kama mtu anauza mchicha, halafu unamhusisha na Singapore, inaonyesha weledi mdogo wa kuendesha *operation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, zitaundwa Kamati sina wasiwasi, ninachotaka kuiambia Serikali yangu, kwa sababu nina mashaka, mimi nilisoma *operation* kwa nadharia, sikuchuna ngozi lakini nilisoma *stage* zote za *operation*. Andaeni watu wa kufanya *operation*, muwape maadili. Mimi kwetu imepigwa Operesheni Kimbunga lakini walifikia hatua kumuangalia mtu urefu wa pua, unamuuliza mtu kwa nini pua yako iko hivi. Sasa watu wa kwetu bahati mbaya hawashirikiani na Mungu kuumba mtu, lakini hiyo mimi niliiona kwamba ni upungufu wa wataalamu wa Serikali na nilimwambia rafiki yangu mmoja Waziri wa Mambo ya Ulinzi kwamba andaeni watu wa *operation* katika mafunzo yao na muwasambaze nchi nzima na itakapofika wakati mnaita *operation*, muwaite watu hao kusudi waje wafanye shughuli hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri maelezo yalipotolewa na Waheshimiwa Mawaziri, sheria zetu hazikidhi. Nimesikitika sana niliposikia rafiki yangu Waziri anasema tuliwaambia watendaji mifugo isihame lakini ikawa inahama; sasa kama Waziri huwezi kuwaambia walioko chini yako wakatekeleza, daah, inakuwa ni shida. Hata hivyo, inaonekana kama sheria hazipo lakini watu wameuana. Nyie mnazungumza haya ya ndugu kwa ndugu, mimi kwangu ni kilio. Juzi imepigwa Operesheni Kimbunga, wale jamaa zangu ninaogombana nao wala hawakuulizwa, nasikia Askari wa Kimbunga

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. J. MWIJAGE]

walikuwa wanafika kwenye mazizi fulani, wakiona mtu anafanana na fulani wanapiga saluti halafu jamaa anadondosha makaratasi mekundu. Nilimueleza kiongozi wangu mmoja kwamba Kimbunga kwetu haitafanikiwa na watu wale wa Kimbunga waliokuwa wanatafutwa, wale wahasimu hasa, wakawa wanafanya kazi ya kuwaumiza wananchi wazawa mpaka jana nimekwenda kuripoti Serikalini, watu wanalia. Hata hivyo, inapomhusu Ngosha, Ngosha anapigwa mpaka afe, inapowahusu wale rafiki zangu, hao wanaachwa, sasa inakuwa ni kizunguzungu mpaka unashindwa kuelewa ufanye nini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niishauri Serikali yangu, mimi katika mtazamo wangu, tembo wanauawa, atafutwe mchawi anayeua tembo, hivi kweli na akili zetu sisi wauaji wa tembo na wauza tembo hatuwajui?

MHE. ANNE K. MALECELA: Nashangaa!

MHE. CHARLES J. MWIJAGE: Atafutwe huyo mtu na namna ya kujisafisha ni kuwaleta wale wahusika tuwashughulikie kiuhalisia. Halafu tukubaliane, kama mifugo haina malisho lakini mifugo tunaihitaji, mnatueleza hizi lugha za kiutaalam, tufanyeje sasa ili kusudi haya makundi yasiendelee kuhasimiana. Inaonekana hatuna utaratibu, kama vile ambavyo hatujui kuendesha *operation*, hatujui hata ku-*manage* hizi *departments*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine linalonisikitisha, tumepewa taarifa kwamba kuna watu hawana maadili lakini wako ofisini, kwa hiyo makosa yanafanyika kwa sababu watu hawana maadili. Kama hii ingekuwa *paper* za kusahihisha, daah, nashukuru Mwenyezi Mungu sikuwa *Lecturer*, hawa watu wangeshindwa kabla ya kufanya mtihani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anakuwaje Mtendaji, amepewa mamlaka na nilisema jana kwenye redio, mtu amepewa mamlaka, amepewa majukumu halafu hawajibiki? Kwa hiyo, naiambia Serikali Kuu tubadilike sasa, nenda katika utaratibu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. J. MWIJAGE]

ambapo mtu atapewa ofisi, ataambiwa afanye nini na atapewa mamlaka, asipofanya hivyo aondoke asubuhi. Kinyume cha hapo, utamwambia mtu atakataa kutii na asipotii majanga yatatokea kama haya na mtu utawajibishwa kwa kosa ambalo hukufanya. Unapita mtaani watu wanakuambia ulichuna mtu ngozi wakati hata mtu mwenyewe humjui.

Mheshimiwa Spika, haya ni matatizo makubwa na lazima tuchukue hatua. Naungana na wenzangu tuchukue hatua ili kusudi wananchi wajue kwamba Serikali imechukua hatua. Mfugaji afuge, mkulima alime na tembo waendeleo kuzaliana lakini kwangu mimi tembo ni kiama. Baada ya wale ndugu zangu wale ambao sitaki kuwasema kusudi *East Africa* isife; wamehamia Kimisi na Burigi, mbona hawajaondolewa? Sasa wanafukuza tembo, tembo wanakuja Rutoro. Tembo wamekuja vijijini wanakula mazao ya wananchi kwa sababu wale jamaa ambao hawataki kuguswa wamekwenda Kimisi na Burigi. Mbona hiyo Operesheni Tokomeza haijawakamata wale, si mngeanzia kule? Mimi nashindwa kutetea mtu, nashindwa kuelewa kinachofanyika. Hapa tunakwenda ndivyo sivyo turudushe utengenezaji wetu wa taratibu katika misingi.

Mheshimiwa Spika, siwezi kuendelea zaidi, hili suala ni tete na ningewaomba wote tulijadili kwa malengo na maslahi mapana ya Taifa letu. Nauunga mkono utengenezaji wa Kamati Teule ili ishughulikie suala hili. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Kamani!

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwanza labda ni *declare interest* maana yake wakati mwingine unapooonga kwa uchungu watu hawajui ni nini. Mimi kwa taaluma ni Daktari wa Mifugo lakini ni mfugaji. Vilevile kwa taaluma ni Mhifadhi. Kwa hiyo, haya mambo ninapooona yanaenda kwa namna ya kusikitisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. T. M. KAMANI]

namna hii, inaniuma sana kwa sababu sivyo vile tulivyofundishwa.

Mheshimiwa Spika, zamani kulikuwa na ugonjwa wa mifugo uliokuwa unaopwa sana, unaitwa Sotoka. Nchi nyingi ziliungana, mataifa yote kupambana na Sotoka hatimaye ikatokomezwa na Waziri wa Maendeleo ya Mifugo alitoa taarifa hapa ya kupongeza watu walichangia katika kutokomeza ugonjwa huo katika nchi yetu. Hata hivyo, sasa hivi Sotoka imerudi na Serikali ndiyo Sotoka ya mifugo katika nchi hii. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli inasikitisha sana, Polisi, Mahakimu wamekuwa Sotoka wa mifugo katika nchi hii. Ng'ombe waliouawa katika nchi hii, kwa kweli inatia uchungu. Rasilimali za nchi yetu ambapo kwa kudura ya Mwenyezi Mungu iko, kuwa na ng'ombe wengi imegeuka kuwa mateso na majanga. Utaratibu wa *operation* umefanyika visivyo kabisa.

Mheshimiwa Spika, tuliwahi kuona *operation* mbalimbali katika Taifa hili enzi za Mwalimu; *operation* inaandaliwa, watu wanapewa elimu ili wafahamu madhara na matokeo ya *operation* ile. Viongozi wanashirikishwa, wanafundishwa na wananchi wanaelimishwa lakini *operation* hii imefanyika kinamna yake. Kwa sekta ya mifugo, mimi kwa kweli nasema Wizara Mifugo imepoteza uhalali wake. Rais aliianzisha kwa nia njema kwa kutambua kwamba mifugo inaweza kuwa sekta ya kuwaondolea watu umaskini na kujenga utajiri kwa Taifa, lakini sicho hicho ambacho nafikiri Rais alikitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika *operation* hii, kokote mifugo ambako imeuawa, sijaona Waziri, wala Katibu Mkuu, wala Mkurugenzi wa Mifugo ambaye ametoa kauli. Mimi nafikiri hata Madaktari wa Mifugo katika nchi hii, wamepoteza sana heshima yao kwa sababu kila Mkoa ambako *operation* imefanyika yuko Daktari wa Mifugo wa Mkoa na Wilaya, lakini hawajasema chochote. Huwa tunakula kiapo cha kulinda uhai wa wanyama wakati tunapopewa digrii zetu lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. T. M. KAMANJ]

hakuna Daktari au Mtaalam yeyote aliyekemea jambo hili; wanyama hawapaswi kufa kwa namna hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kawaida hata jambazi anapokamatwa, akishawekwa kwenye mikono ya sheria, hateswi tena, hata hukumu ikitolewa akafungwa gerezeni, hateswi tena na anapewa chakula. Hata hivyo, sisi katika *operation* hii, mifugo imekamatwa, imefungiwa kwenye mazizi kwa siku hadi tano, haipewi chakula wala maji. Mifugo inadondoka kwa njaa. Mfugo haujipeleki wenyewe kwenye pori, mifugo inapelekwa na watu, badala ya kushughulika na watu wale kwa sheria na taratibu, unaadhibu mifugo, unasema una akili timamu? Nasema hawa watu kwa kweli wamekiuka kabisa misingi ya ubinadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa taaluma tunafundishwa kwamba kwa sababu mifugo ni sekta muhimu, iko duniani na inatajirisha mataifa; Botswana, ukiondoa almasi, shughuli nyingine muhimu ni mifugo, inaliingizia taifa pesa nyingi. Hivyo hivyo na kwa mataifa mengine makubwa yaliyoendelea, Marekani wanafuga tena wana *ranch* kubwa, Kusini ya Marekani ni *ranching*, New Zealand na Australia. Tunafundishwa kwamba lazima utenge maeneo ya malisho na maji, uweke miundombinu lakini katika nchi yetu, hakuna.

Mheshimiwa Spika, nimeona kile kitabu cha Mipango, ukurasa wa 37 na kwenye hii taarifa ya Waziri anasema wanaweka miundombinu kule Kilindi, Kiteto, Kishapu, Maswa na Same halafu na Chunya, Lindi na Rufiji. Maeneo ambayo yameshambuliwa, ambayo yamepata matatizo makubwa ni maeneo yanayozunguka maeneo ya hifadhi, sijasikia akitaja Itilima, Busega, Bariadi na Meatu. Kama mnaweka miundombinu kule ambako hakuna matatizo, ninyi akili yenu inakuwaje katika upangaji wa mambo? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, katika taaluma tunafundishwa uboreshaji wa mbegu ya mifugo, vituo vya uzalishaji wa mbegu za mifugo haviendelezwi, vimeachwa vinasambaratika, kiko kule Mabuki, kilianzishwa enzi za zamani, suala hilo halipo. Kuna suala la masoko, juzi juzi hapa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. DKT. T. M. KAMANI]

wale Mahujaji kule Saud Arabia walikuwa wanahitaji mbuzi kulisha Mahujaji. Tanzania tuna mbuzi milioni 16 lakini tumeshindwa kulitumia soko lile kwa sababu hatuna mipango iliyokaa sawa lakini watu wanawahi kwenda kushambulia mifugo kule na kupiga risasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa magonjwa, usimamizi (*management*) lazima kuwe na *management*, wataalam wetu wako ofisini, hata hii mifugo iliyoshambuliwa hakuna aliyeangalia. Kwa kweli, inasikitisha sana. Mifugo ingeweza kuwa mtaji mkubwa kwa Serikali kwa kuingiza fedha ya kigeni, ingekuwa chanzo kikubwa cha mapato kwa Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kuna haja ya Serikali kujiangalia upya kwa sababu kwa kila tatizo kuna *solutions* zaidi ya 1,000, hebu tuzitafute hizo *solutions*. Haiwezekani wafugaji ndio ikawa taabu, labda tujue kama ni chuki tu kwamba kuna mifugo basi inakuwa chuki. Mifugo hii ni mtaji mkubwa ambapo Serikali ni vema ikautumia. Wanyamapori wakishambulia maeneo ya wananchi, Askari huwa wanaenda na baruti, wanawapiga, wanawatisha wanarudi kwenye Hifadhi. Wanyama hawauwawi, wanarudishwa. Inakuwaje ng'ombe wakienda porini, wanaenda kupigwa risasi? Kwa kweli kitu hiki tumevuka misingi ya ubinadamu na ni lazima tuangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna namna nyingi ya kutumia wataalam waliopo kuhakikisha sekta hii ya mifugo inatajirisha taifa letu. Viwanda siyo viwanda vidogo vidogo, tuna ng'ombe milioni 22 za ngo'ombe, Tanzania ni nchi ya pili, hawa siyo ng'ombe wa kiwanda kimoja, wanahitaji viwanda vingi, inatakiwa elimu ya kutosha, Wagani wetu wako wapi kule kwenye mifugo? Wagani wamemaliza kozi miaka miwili iliyopita lakini mpaka sasa hawajaajiriwa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ester Bulaya, atafutia Mheshimiwa James Mbatia na Mheshimiwa Sakaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa na mimi niseme natoka katika Mkoa ambao una wafugaji, Mkoa wa Mara. Napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wafugaji wote, ndugu na jamaa ambao ndugu zao wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, mimi labda niwaulize Wabunge wenzangu, hivi ninyi mlitarajia ripoti ya namna gani kwa matukio ambayo yameanza kutokea, watu wameuwawa, ng'ombe wanauwawa, tunaanza Bunge, Mawaziri husika hakuna hatua yoyote waliyoichukua, mlitegemea ripoti gani zaidi ya hii ambayo imetolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashangaa na nimesikitika sana, eti mafanikio ya *operation* hii ni kukamata ng'ombe, kukamata magari, ni kukamata meno ya tembo lakini majangili hakuna hata mmoja aliyekamatwa, tunaambiwa ni mafanikio, kweli? Kama Bunge ni lazima tufanye kazi yetu na naunga mkono hoja ya kuanzishwa Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtandao huu wa ujangili ni mkubwa. Mawaziri wanaohusika na hizi Wizara wamekuwa wakilalamika tu lakini hakuna Mpango Mkakati wa kukabiliana na suala hili la ujangili. Naomba nitoe mfano mmoja. Kuna kesi ilikuwa inamkabili mshtakiwa mmoja nguli wa ugangili linalojulikana, akafungwa, lakini mtandao ulivyokuwa mkubwa, watu wali-*lobby* kuhakikisha anatoka kwa Msamaha wa Rais, ni aibu ya namna gani? Baada ya kugundulika na Mheshimiwa Rais kutoa maagizo, suala hili lilishughulikiwa, yule mshtakiwa akakamatwa akawekwa ndani lakini jinsi mtandao huo ulivyo mkubwa, leo hii yuko nje anapeta. Leo tunapewa taarifa mafanikio ni kukamata ng'ombe na kutokomeza nguvu za wafugaji katika taifa letu. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. A. BULAYA]

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Bunda tu peke yake, tunapozungumza matatizo ya wananchi, nawaomba Mawaziri muache kusema habari hizo hazina msingi kwani tunapewa taarifa na wananchi na wengine tunapewa taarifa na viongozi wetu wa chama. Kwa hiyo, tunapoleta taarifa hapa mzizingatie na mjue tuko makini na wala hatutishiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bunda peke yake, Jimbo la Bunda, ng'ombe 120 wamekamatwa, watu zaidi ya 50 wamepigwa na mpaka sasa hivi ng'ombe wako Ndabaka. Kata ambazo zimedhurika na zoezi hili ni Nyamatoke, Kunzugu, Unyari, Mgeta, Mcharo na maeneo mengine. Sasa hatuwezi kuacha kuzungumzia matatizo yanayohusu wananchi, hatuwezi! Siwezi kuacha kuzungumzia matatizo niliyopewa na kiongozi wangu wa chama, haiwezekani! *(Makofi)*

MBUNGE FULANI: Ahsante!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, tunaomba haya mambo yafanyiwe kazi. Tunaomba matatizo ya wananchi Wabunge tunapoyaleta hapa yashughulikiwe na zisiletwe danadana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la wafugaji kunyanyaswa, halijaanza leo. Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola amezungumzia suala la Kawangwa. Huyu mwekezaji Grumet amekuwa kama ni 'Mungu Mtu' katika Wilaya ya Bunda. Suala hili alianza kulishughulikia Mama Shamsi Mwangunga, likamshinda, kwa sababu badala ya kwenda kwa wananchi alikwenda kwa mwekezaji. Nimetoka Bunda, niliitwa na Wazee, nikaenda kwenye vijiji vya Kunzugu, Nyamatoke, Unyari, Kihumbu na Mgeta, kote huko nimefika. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wale wameniambia matatizo yao na walitaka kuja Bungeni, nikawa muungwana, hata Waziri nilimwambia, nililifikisha kwenye Kamati na picha ambazo Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola, amezileta.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. A. BULAYA]

Sasa tufanye *research* ya namna gani ili Wabunge tueleweke? Hilo pori hata ubadilishaji wake wa matumizi, ni wa utata. Alinukuliwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bunda anasema hana nyaraka za kubadilishwa kwa pori hilo kutoka kuwa matumizi ya wananchi na kuwa Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, wananchi wanavyonyanyaswa, ukisikia mzee wa miaka 70 na zaidi anazungumzia suala la kumwaga damu kutokana na manyanyaso ya kukamatwa mifugo yao na kuzamishwa Mto Rubana ni hatari. Bibi wa miaka 75 anafungwa, haiwezekani tukaacha kuzungumzia mazungumzo kama haya ambayo yanawahusu wananchi wetu. Wananchi wanalalamika, Viongozi wa vyama wanalalamika halafu tuache kuja kuyasema katika Bunge lako Tukufu, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, katika pori hilo ambalo lilikuwa la wananchi, wananchi kule kuna makaburi yao, tunajua tamaduni za Afrika, wakienda kuhani wanakamatwa, wanapigwa wanauliwa. Leo hii mwekezaji Grumet ametengeneza zizi, anakamata mifugo anaiweka kule anaifuga inakuwa ni yake. Haiwezekani tukaacha kuongea matatizo ya msingi kama haya yanayolihusu taifa letu, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kutatua tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji na wawekezaji kama tusiposhughulikia mipaka yetu kikamilifu. Kama tusipotenga maeneo ya wakulima na wafugaji, hatutaweza kushughulikia tatizo hili. Hatuwezi kushughulikia matatizo haya kwa maneno au kwa *pressure* ya Bunge, kila mmoja atimize wajibu wake. Hilo ndilo jambo la msingi. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: *Yes!*

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Saidi Nkumba amesema mpaka watu wa-*react*, waumie, ndiyo wahusika waanze kuchukua hatua, siyo vizuri. Haya mambo yametokea maeneo mengi tu, Mheshimiwa Lukuvi, ndugu yake kapigwa na wala siyo jangili, basi kwa sababu yuko

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. E. A. BULAYA]

kwenye nafasi yake hawezi kusema, hatuwezi kufumbia macho masuala kama haya. Kwa hiyo, ni lazima waje na mipango madhubuti, waje na hiyo ripoti ya kueleweka na wote ambao wamesababisha matatizo haya na *crisis* kwa wananchi, wachukuliwe hatua na hilo ndiyo jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi naunga mkono. Tunaiomba Serikali ichukue hatua ipasavyo. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Mbatia atafuatiwa na Mheshimiwa Sakaya.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, uhai wa mwanadamu haununuliki kwa gharama yoyote ile. Jambo tunalolizungumzia limeshasababisha mauaji kwenye Taifa letu, chuki ni kubwa na yote haya yamesababishwa kwa kiasi kikubwa niseme na uzembe. Uzembe huu unatokana na kutofanya maamuzi kwa wakati sahihi. Tatizo linapotokea, Serikali inaelezwa, Serikali inakuwa na urasimu wa kufanya maamuzi, ndiyo yamefikisha Taifa hili hapa tulipofikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja kwa kielelezo, ukienda Mkoa wa Kigoma, kwa mfano Wilaya ya Kasulu, mauaji yametokea kule Rongwe mpya na Rushingo. Vita vimetokea, chuki kati ya Wasukuma na Waha kule Kagerankanda. Uvinza chuki imetokea Kati ya Waha na Wasukuma. Leo tunajenga chuki ya makabila kwa makabila kwa sababu ya Serikali kutokufanya maamuzi kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina kilometa za mraba 945,903 ni eneo kubwa tu, ambalo linatosha ukiwa na mipango thabiti, ambayo umejipangia vizuri. Leo hii inatokea chuki, wakulima hawa, wafugaji hawa, ufugaji wetu huu ni utajiri lakini leo imeonekana ni kero. Leo hii wakulima wanawaona wafugaji ni tatizo. Wafugaji wanaona wakulima ni tatizo, tunajenga chuki.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. F. MBATIA]

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano. Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, mwaka 2012 mwezi wa Desemba, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mheshimiwa John M. Cheyo, tulichangishana kwa pamoja kuangalia tatizo la ufugaji katika Mkoa wa Morogoro. Tulituma Mwakili kule. Unapokuta Jeshi la Polisi wanaposhika mifugo, wao ndiyo wanakuwa wachungaji wa mifugo na kila Askari anatakiwa alipwe Sh.7,000/= kila siku, hivi Serikali iko wapi, *let us be sincere*. Unapona kwamba mfugo au ng'ombe mmoja anapigwa faini ya Sh.59,000/= unaongea na Mkuu wa Mkoa ana viwango vyake, *District Commissioner* ana viwango vyake, *DAS* ana viwango vyake, maamuzi yako wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano chuki ninayoisema kwa pale Kasulu, unapona Mkuu wa Wilaya, Waha wa Kasulu wanasema huyu ni Msukuma, *DAS* ni Msukuma, Afisa Usalama ni Msukuma, kwa hiyo linaonekana ni genge la Wasukuma dhidi ya Waha kuleta uharibifu katika jamii yao. Sasa tunapojenga chuki kila siku, taarifa zinapelekwa Serikalini na Mheshimiwa Waziri Mkuu tulishazungumza na wewe kuhusu hili, lakini maamuzi hayafanyiki, sasa tunapofika kwenye hatua za namna hii kwa kweli inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi tulipozungumza naye kuhusu tatizo hili, unamweleza matatizo yanayotokea, anakuambia hana habari. Maeneo ya wafugaji yako wapi, hana habari! Sasa Serikali iko wapi, wajibu wa Waziri uko wapi? *(Makofi)*

Operesheni Tokomeza, ukienda Arusha leo, kule Mbauda na Minjingu, watu wamewekwa *lockup* pale Minjingu zaidi ya wiki mbili, wamepigwa, wamenyanyaswa kweli na hawapeleki Mahakamani, haki iko wapi? Sasa tukiendelea na utaratibu huu wa kutokuwajibika kwa pamoja, kwa sababu hili ni suala la kuwajibika kwa pamoja, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara nyinginezo, TAMISEMI nayo iko ndani yake lakini unakuta

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. F. MBATIA]

hakuna uwajibikaji wa pamoja na ndiyo maana unaweza ukakuta Waziri huyu analalamika, Waziri huyu analalamika, Mbunge alalamike, Waziri alalamike, sasa ni nani amfungue paka kengele. Serikali isisubiri kuwa *reactive* mpaka tatizo litoke ndiyo tuanze kujibizana hapa kwa shinikizo, Serikali *must be pro-active* ndiyo maana ya Serikali, unaona kesho itatokea nini, unakuwa na *mitigations measures* leo kabla ya tatizo halijatokea. Leo hii tatizo limekuwa ni kubwa, mauaji yanatokea kwenye taifa letu, sasa tufanyeje? Mwaka 2015 lengo la Saba la Melenia kuhusu *sustainability and environmental protection*, tutajeleza namna gani?

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hali tuliyofikia leo hii, hata elimu yenyewe ya ufugaji katika Taifa letu ni tatizo kubwa. Elimu hata ya ukulima yenyewe ni tatizo kubwa. Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi amezungumzi suala la Sera ya mwaka 2006. Je, ni *viable* mpaka leo hii, inatumika namna gani leo hii?

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Serikali isijaribu kuja na majibu mepesi kwa matatizo magumu kwelikweli kwa Taifa hili. Kwa sababu tunasema hii ni nchi ya amani na utulivu lakini vita vipo, mauaji kila siku yanatokea. Mama Celina Kombani kwako kuna matatizo makubwa sana kuhusu mambo ya ufugaji na wakulima hapa. *Let us be sincere*, hili ni tatizo la Taifa zima. Sasa tunapokuja na majibu mepesi, kwa nini tufikie hatua hii? Kusipofanyika maamuzi magumu sasa bila kuoneana aibu, wanasema ukitaka kumpiga nyani wala usimwangelie usoni, hatuwezi tukavuka hapa tulipofikia. Kwa sababu unaweza ukawa na vyombo lakini kama vyombo hivi havifanyi maamuzi kwa wakati wake, unapopata *crisis* kama hii kitaalam, unapofanya *classification* zake, unashindwa ku-*come up* na *mitigation measures immediately*, kwa kitaalam na wakati unaofaa, inakuwa ni tatizo zaidi.

Mheshimiwa Spika, niombe tu na labda nisiombe kwa sababu wajibu wa kwanza wa Bunge ni kuisimamia Serikali. Muda huu tulioupata ni mfupi. Mimi naunga mkono kabisa Kamati Teule ya Bunge makini iliangelie jambo hili kwa undani

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. F. MBATIA]

na ndiyo wajibu wa Bunge lako Mheshimiwa Spika, itakuwa imechukua nafasi ya kuisimamia vizuri Serikali kwa kuwa Serikali imeshindwa kutekeleza wajuu wake wa kusimamia ulinzi na amani wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1648, *Democratic Principle* ilianzishwa wakati wa ukabaila, fujo zilitokea sana kule Ulaya, kwenye mambo ya ardhi, wanatoka kwenye ukabaila wanaenda kwenye ubepari. Wakaanzisha *Democratic Principle*, inayosema, *no representation no taxation*. Hakuna uwakilishi makini kama wa Bunge hili dhidi ya Serikali, hakuna kulipa kodi. Je, Wabunge wawaambie Watanzania wasilipe kodi kwa sababu wanakosa Serikali makini ya kusimamia kodi zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hatutaki tufike huko kwa sababu Taifa hili ni letu sote. Malengo yetu tunalitakia mema Taifa letu. Mivurugano iliyopo nje ya mipaka yetu ni mikubwa sana, hebu humu ndani basi tuwe makini, tuwe *serious*, tushirikiane kwa pamoja, tuwe Taifa makini ambalo kweli linaweza likaongoza Bara hili la Afrika. Kwenye mifugo ni migogoro, kwa wakulima ni migogoro, kwenye siasa ni migogoro, kwa majirani zetu ni migogoro, tutakuwa tuna-*deal* na migogoro, migogoro. Wanasema *great mind discuss ideals simple minds discuss events*. Hatuwezi tukaendesha Taifa kwa matukio, ni lazima tuendeshe Taifa hili kwa hoja makini ambapo tunataka tulitoke hapa, tuone kweli 2025 tunafika kwenye hali ambayo unasema kweli Tanzania hii na rasilimali tulinazo, migogoro ya gesi huko na wapi, hapana, iwe ni neema kwa Taifa na isiwe ni balaa.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema kwamba wakulima waonekane kwamba wana haki ndani ya Taifa hili, wafugaji wana haki ndani ya Taifa hili, mifugo tuliyo nayo iwe ni neema na utajiri kwa Taifa isiwe ni balaa kwa Taifa na wale wote waliozembea mpaka uhai wa binadamu ukatoweka, hatuwezi tukarudisha maisha ya binadamu, wawajibike ipasavyo bila kuoneana aibu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Sakaya!

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo kwenye hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naungana na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba upo umuhimu mkubwa sana wa Bunge lako kuingilia kati ili wafugaji waweze kupata neema na wakulima wa Tanzania waweze kupata neema katika nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni ukweli unaodhihirika kwamba Serikali iliyoko madarakani imeshindwa kabisa kusimamia suala la migogoro ya wafugaji Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *operation* ambazo zimetamkwa kwenye Taarifa ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, za majina mbalimbali, Operesheni Ihefu, Operesheni Ondoa Mifugo Morogoro, Rukwa, Tabora za mwaka 2009, Operesheni Kimbunga, Operesheni Tokomeza Ujangili, zote zimekuwa na madhara makubwa sana kwa Taifa, kwa wafugaji na kwa rasilimali ya mifugo ambayo tunategemea kwa ajili ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Operesheni ya Ihefu, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Tume kwa ajili ya kuangalia madhara yaliyotokea, utaratibu haukufuatwa, maandalizi hayakuwepo, tukategemea italetwa taarifa lakini mpaka leo Watanzania hatujui kilichoendelea. Operesheni Hamisha Mifugo Tabora, Morogoro na Rukwa watu walijinufaisha kwa ng'ombe za wafugaji, watu walikuwa matajiri kwa kutegemea ng'ombe za wafugaji. Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2009 aliunda Tume na akatuambia hapa Bungeni kwamba atatuletea taarifa lakini mpaka leo hakuna taarifa inayohusiana na suala hilo.

Mheshimiwa Spika, leo tunakuja kushuhudia tena matatizo mengine ndani ya wafugaji haohao, inasikitisha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

sana. Serikali kuanzia mwaka 2008 mpaka leo 2013, kweli, wameshindwa kuwaambia Watanzania ni kwa nini matatizo ya mifugo yanatokea? Ni kwa nini wafugaji wamekuwa wakimbizi ndani ya nchi yao? Inaumiza!

Mheshimiwa Spika, wakati nafuatilia suala la mifugo zaidi ya 6,000 mwaka 2011 waliokamatwa kutoka Kijiji cha Shela Usinge wakafungiwa ndani ya Ofisi ya Kata Usinge Mjini, nilipokutana na lile tatizo kwanza nilimpigia Mheshimiwa Waziri wa Maliasili aliyekuwepo wakati huo na Mheshimiwa Waziri wa Usalama, nikawaeleza hali halisi kwamba lipo tatizo kubwa hapa, mifugo inakufa, iko siku sita hapa, hawana chakula wala maji lakini hakuna aliyechukua hatua yoyote. Walichoona cha msingi, tumchukue Sakaya, tumweke ndani, tumnyamasishe, badala ya ku-*dea*/na tatizo lililokuwepo wakati huo. Kuanzia mwaka 2011 pamoja na kuwa nimekwenda ndani nimekaa siku zote hizo, nimeumwa na mbu mpaka leo kwa nini angalau hawakwenda kuangalia lile tatizo? Hata hivyo, nashukuru Mungu nilikaa ndani tarehe 30, mifugo imefungiwa ndani siku sita na tarehe 31 imetoka ile mifugo bila maandishi yoyote, bila faini yoyote na bila maelezo yoyote mpaka leo. Inasikitisha kwamba hata Mawaziri ambao tumewapa dhamana, kwa kweli wanapoona tatizo hawalipi umuhimu unaostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wafugaji wamekuwa wanatumwiwa kama vitega uchumi kwa watendaji wa Serikali kwa maeneo mengi, sana! Watendaji wa Serikali wakiwemo Maafisa Game, wanakwenda kuwachukua ng'ombe kwenye maeneo ya wafugaji, wanawaswaga wanawapeleka kwenye Hifadhi, wakifika kule wanaanza kuwaambia tunataka milioni kadhaa za pesa, milioni tano mpaka milioni ishirini, wafugaji wanasema hatuna, wanaanza kushindana kwamba lete kumi au kumi na mbili, wakiona hawana kabisa ng'ombe wale wanapiga mnada. Polisi wanaitwa, wanaitwa na wanunuzi wanawapiga mnada wa chini ya thamani. Inaumiza kuona ng'ombe wa shilingi milioni moja, anauzwa kwa shilingi 60,000/= mpaka 100,000/=, leo tunasema kwamba hatuna pesa Watanzania. Rasilimali hii

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

ambayo ni nchi ya pili duniani kuwa na wanyama wengi, tumeshindwa kuitumia, tunalia uchumi ni mbaya, tunalia hakuna fedha za miradi ya maendeleo, tunazipata wapi?

Mheshimiwa Spika, hivi juzi tarehe 30 mwezi huu, katika Wilaya ya Kaliua, Kijiji cha Kangeme, ng'ombe 2,700 wamepigwa mnada. Tulivyokuwa tunaomba hapa kwamba tusitishwe, tujadili kwa dharura, kule walikuwa wanapiga mnada. Kwa hiyo, pengine siku ile kama zoezi lingesitishwa wale ng'ombe wangeokoka. Leo ng'ombe wale wamepigwa mnada, wafugaji wamekuwa maskini, ukiuliza bei iliyozwa ng'ombe utalia machozi, mbuzi Sh.5,000/= hata bei ya kifaranga cha kuku huwezi kupata kwa bei hiyo. Tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, Wabunge tunapoongea hapa Bungeni, tunaleta matatizo, Serikali iyafuatilie, isichukulie kama ni Sakaya, wengine ilifikia hatua wanasema Sakaya anatafuta umaarufu wa kisiasa, leo yako wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo yapo, tunapokwenda kule tunayaona, tunapotembea kwenye ziara tunayaona, tunayaleta Serikalini ili yafanyiwe kazi, matokeo yake dharau, leo tupo hapa, wafugaji wanauawa na ng'ombe wanauawa, hivi kweli ng'ombe wa Sh.1,000,000/= wanapangwa mstari, ng'ombe 10 wanapigwa risasi na Askari anayevaa kombati, viatu, soksi, kofia kwa pesa za Watanzania. Kwa kweli naomba sana Bunge lako liingilie kati kwani Serikali imeshindwa na imeshindwa kwa sababu taarifa za kuanzia mwaka 2008, zipo wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka nijue, nimewahi kumuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo muda mrefu kwamba ng'ombe wakikamatwa wanaweka faini zao, unaambiwa ng'ombe mmoja Sh.180,000/=, mtu ana ng'ombe 800 mpaka 1,000, unamwambia faini ya Sh.180,000/=, nataka nijue ni sheria gani ambayo inaruhusu mtu kujiwekea utaratibu wa faini kwa ng'ombe mmoja Sh.180,000/=, wafugaji wakishindwa kulipa faini hiyo ng'ombe wao wanapigwa mnada na ndivyo inavyokuwa. Wafugaji wamekuwa maskini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)
[MHE. M. H. SAKAYA]

na wengine wamepoteza maisha, hata sheria za nchi tumeshindwa kuzifuata matokeo yake tupo hapa tulipo leo.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya hifadhi, kwenye hifadhi zetu nyingi na hasa *Game Reserves* na hasa maeneo mengi ya Tabora, Kaliua na Urambo hayajaa inishwa kikamilifu. Nimewahi kusema muda mrefu hapa Bungeni na hata kwenye Kamati ya Maliasili ambayo nimekuwa mjumbe, Serikali itenge pesa, iainishe maeneo haya ili mfugaji akiwa anafuga hapa ajue pale ni hifadhini. Hayo hayafanyiki, fedha haitengwi na kinachofanyika ni operesheni tu, hakuna maandalizi wala usimamizi na wanaoteseka ni wafugaji ambao wako ndani ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya mifugo, tumekuwa tunasema hapa Bungeni lazima tutenge maeneo, wafugaji wameuana mara ngapi? Wameandamana mara ngapi? Wakulima wameandamana mara ngapi? Tutenge maeneo kwenye Serikali za Mitaa na kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya wafugaji na wakulima. Leo hapa Bungeni nimeshuhudia Mheshimiwa Waziri wa Mifugo anasema suala la kutenga maeneo ya mifugo ni la Halmashauri kama wataona kuna ulazima huo. Halmashauri tunajua kweli ni ngazi ya chini ya Serikali lakini fedha ya kutenga maeneo ya mifugo Halmashauri zinayo? Serikali Kuu inahusikaje? Imetoa mwongozo na fedha? Hatuwezi kusema kwa maneno wakati tunaona watu wanakufa. Serikali Kuu imetenga fedha ikasema kwamba leo Kaliua chukueni milioni kadhaa, mna ng'ombe kadhaa tengeni maeneo kadhaa, mmefanya hivyo? Siyo maneno tu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali iwajibike kwa hili, wahusika wawajibike kwa hili wala hakuna *discussion* kwa sababu damu za watu wasiokuwa na hatia zimemwagika chini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo mafupi, nasisitiza tena kwamba Serikali imeshindwa kusimamia masuala haya,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. SAKAYA]

naomba Bunge lako Tukufu tuingilie kati, tuwe na Kamati tena yenye nguvu, ipite nchi nzima, ianishe matatizo ya wakulima na wafugaji ili waweze kukaa salama ndani ya nchi yao. Wote waliohusika kuanzia Operesheni ya lhefu mpaka mwaka 2009, waliojitajirisha kwa ng'ombe za wafugaji, wachukuliwe hatua kwa sababu taarifa zipo zimekaliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Arfi atagawana dakika tanotano na Mheshimiwa Shibuda.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na niseme tu kwamba wananchi wanajua ni nani amewafikisha hapo na matatizo waliyokuwa nayo leo na ni nani waende wakamlilie. Haifurahishi na wala haipendezi hata kidogo kwenye Taifa ambalo karne ya 21 linaendelea kuuwa watu wake, wafugaji wapatao zaidi ya 21 wameuawa Mpanda. Jambo hili si dogo hata kidogo, achilia mbali mifugo kadhaa ambayo ilipigwa risasi. Maelezo na vielezo vipo.

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nataka kusema hapa mahsusi pamoja na maelezo ya Serikali kujikita kwenye mifugo, kwamba mifugo iliyopo iachiliwe na kadhalika, naomba maelezo ya Serikali, nyumba zilizochomwa moto mnafanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napoongea sasa hivi, wananchi wapatao 9,000 kwa maana ya kaya 923 za kijiji cha Kabage ambacho kilisajiliwa tarehe 1/9/2012 na kikapewa hati ya kijiji namba KTKIJ namba 47, kijiji hiki kimechomwa moto chote!

WABUNGE FULANI: Eeeh!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. SAID A. ARFI: Kaya 923, wananchi wapatao 9,000 hawana makazi, familia, akina mama na watoto hivi sasa wanaishi chini ya miti katika viwanja vya mpira katika Kijiji cha Mwamkulu na katika viwanja vya Shule ya Mwamkulu. Hawana chakula kwani chakula chao kimechomwa, Serikali ina maelezo gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mtendaji wa Kijiji hicho alimwandikia *DC* wa Mpanda barua tarehe 30, akimwelezea hali halisi na mahitaji ya wananchi hawa, angalau huduma za msingi za kibinadamu wapelekewe kwa maana ya mahema, chakula na dawa lakini mpaka dakika hii hakuna chochote Serikali hii imewafanyia watu wake. Ni Watanzania na ni wakulima na si wafugaji. Kijiji chao kipo kilomita 26 mpaka kwenye mpaka wa hifadhi, mmeviacha vijiji ambavyo mita 500 kutoka kwenye mpaka wa hifadhi, mmefuata kijiji kilomita 26 kutoka kwenye mpaka wa hifadhi, mmekwenda kuchoma moto, kwa maelekezo ya nani? Kwa maagizo ya nani? Kijiji hiki kimesajiliwa na kinatambulika rasmi na kina hati, wananchi hawa wanateseka.

Mheshimiwa Spika, nataka nipate maelezo ya Serikali juu ya wananchi wa Kijiji cha Kabage Mpanda kutoka na hii Operesheni Tokomezwa, hakuna hata mkia wa tembo uliokamatwa, hakuna hata pembe hata moja ya ndovu waliyokamata, hakuna nyara yoyote waliyokamata katika kijiji cha wakulima lakini wamekwenda kuwachomea nyumba zao, ubinadamu gani? Serikali ya Chama cha Mapinduzi dhambi hii iko juu ya shingo yenu. Hamwezi kukwepa kwa kusema hapa kwa uchungu na kwa kauli kalikali, hii dhambi iko kwenu na Mungu atawahukumu kwa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Shibuda!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. JOHN P. M. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kupata fursa hii ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, mficha maradhi hufichuliwa na kifo. Nasikitika sana kwa haya nitakayoyasema. Wafugaji hivi sasa wamekuwa sawasawa na mbuzi. Mbuzi katika Mahakama ya Fisi hana haki zaidi ya kuliwa tu. Kwa hiyo, inasikitisha sana kwa yale yanayotendeka. Mdai haki daima kwa mdaiwa huambiwa ni mtu mbaya. Naomba haya nitakayoyasema yatambulike kwamba nina dhana kukosoana ni kuimarishana na siyo namsonta mtu kwa ajili ya kumsema vibaya.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, Wizara ya Mifugo haina sikio sikivu na siyo kimbilio na ina tabia ya kifuniko kwa kasoro na matatizo ya wafugaji. Ingekuwa ni sikio na ni kimbilio la wafugaji hapa leo tusingekuwepo wangukuwa wameshaieleza Serikali. Kwa hiyo, Wizara hii kwa kweli ni Wizara hasi kwa maslahi ya wafugaji.

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI vilevile ndiyo jiko la dhuluma na ndiyo jiko vilevile la mikakati hasi dhidi ya wafugaji. Kwa hiyo, napenda kusema kwamba sheria zilizo hivi sasa, zilizozaa dhuluma zote hizi, naomba Kamati utakazounda uhakikishe zinapitia sheria zote za mizozo katika Halmashauri zote na sheria gandamizi zifutwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali imezua mbegu ya kubaguana, TAMISEMI ndiyo jiko la kuzaa kubaguana, wafugaji tunaitwa wahamiaji haramu na wavamizi haramu kama Idd Amin ndiyo maana kuna Operesheni Tokomeza. Hata hivyo, TAMISEMI ni nani? Mlezi wa TAMISEMI ni Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna taarifa za kiintelijensia, je, hupati? Magazeti yameandika, je, hupati taarifa hizo? Kwa nini unakaa kimya Watanzania wanaambiwa ni wafugaji haramu na TAMISEMI ambao ni Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Ma-DED. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa CCM mnaposema mnawataka kuwauliza Mawaziri, anzeni kumwuliza Waziri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. P. M. SHIBUDA]

Mkuu, anawajibika vipi kwa azimio tulichoazimia katika Bunge hili mwaka 2009 na kasoro ni zilezile zinajirudia. Naomba hilo mmulize Waziri Mkuu ili aweze kutoa sababu za kwa nini anakaa kimya wakati Watanzania wafugaji anaona wanateketea na hasemi jambo lolote mpaka jambo lije kuibuliwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, kila kitu azungumze Mheshimwa Rais na je, kwa nini Mheshimiwa Rais jina lake linatumika kwamba kaagiza, je, Rais anaagiza vyombo vya dola viue wananchi na mifugo? Naomba Serikali ikanushe kama kweli Rais hakutoa kauli hiyo na kama alitoa kauli hiyo basi CCM mumulize Rais kwa nini anavunja Katiba yake ya CCM na utumishi wa siasa za CCM na matakwa na nguzo kuu za kudai uhuru wa Tanganyika ya TANU na AFROSHIRAZ.

Mheshimiwa Spika, sasa imethibitishwa kuna ongezeko la mifugo na ongezeko la wanyamapori na hao wote malisho yao yako sawia, kwa nini Serikali inashindwa kuongeza maeneo kwa wafugaji inaongeza kwa mifugo? Hii maana yake nini? Tunaomba Serikali ijielekeze na nasikitika, naomba nimwambie Mheshimiwa Rais na watani zetu wote mliopo humu ndani, mtambue ya kwamba 90% ya watu wanaooneka ni watani zenu Wasukuma ambao wana tatizo na kasoro ya kutokuwa na elimu hata ya kudai haki zao. Hivi ingekuwa ni watu ambao wana uhusiano na makabila ya viongozi humu, mngekuwa mnakaa kimya? Mngekuwa mnakaa kimya? Tunaomba mtuokoe kama kweli ninyi ni Serikali ya ukombozi. Baba wa Taifa alikomboa Bara la Afrika, Siasa ya TANU ilikuwa ya kukomboa Bara la Afrika na CCM pamoja na AFROSHIRAZ, inakuwaje sasa kuna mrejeo wa ubeberu, umangimeza na ukaburu dhidi ya wafugaji? Naomba suala hili lieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikitika kusema kwamba hivi sasa TAMISEMI utumishi wake pamoja na utumishi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ndiyo unaozaa migogoro hii. Nasema hivyo bila kusita kabisa na ingekuwa ni kumwomba mtu kujiuzuru ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu ... *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, natamani wote msembe lakini mko zaidi ya mia, kwa hiyo haiwezekani. Pia mkumbuke kwamba hii ilikuwa ni namna ya kupata tuchukue hatua gani ya kimatendo na sio tuendeleo kuongea. Kwa hiyo, kwa maana hiyo, mjadala huu tumeufunga lakini maagizo yangu ni kwamba suala la Operesheni Tokomeza Ujangili kwa sababu wameanza karibuni, yote haya makubwa yametokea, tulipokaa Kamati ya Uongozi tukasema kwamba hili tunaiachia Kamati ya Maliasili na Utalii kuona kwamba mipango waliyoifanya Serikali mpaka imeleta mauaji hayo ni ipi? Kwa hiyo, tunaigiza Serikali mara moja itoe taarifa yote halafu Kamati yangu itapita humo mote walipopita ili kusudi waweze kuleta maelezo.

Waheshimiwa Wabunge, mchana tunarudi, kwa mujibu wa Kanuni ya 120, tunakuja kuunda Kamati Teule kuhusu tatizo la wakulima na wafugaji. Kwa hiyo, tutarudi mchana kufanya kazi hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kuna mambo mawili ambayo naomba mzingatie, Operesheni Tokomeza Majangili itashughulikiwa na Kamati yetu ya Maliasili na wao tutawapa nafasi ya kupita na kuona vyote vile ambavyo vinazungumzwa na wananchi na tunawaomba wananchi pia wajitokeze, yote haya kama ni hasara na kadhalika Kamati yetu itabidi isikilize.

La pili ni hili la wakulima na wafugaji, tunaliundia Kamati Teule mchana tukirudi kwa sababu inaonekana limeungwa mkono lakini itabidi iletwe hoja mahsusi.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa
Mpaka Saa 11.00 jioni)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunasitisha shughuli za Bunge asubuhi, tulikuwa tumepewa taarifa kwamba, kungekuwepo na mjadala kuhusu Kamati Teule. Kwa hiyo, sasa nitamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla. *(Makofi)*

Kamati Teule ya Kushughulikia Migogoro Kati ya Wakulima, Wafugaji na Hifadhi Nchini

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa niliyoitoa leo asubuhi wakati tunachangia Hoja ya Kuahirisha Shughuli ili kujadili mambo muhimu ya dharura, inayohusu maelezo ya Serikali kuhusu Mgogoro kati ya Wafugaji na Wakulima, Hifadhi na Uwekezaji, nilieleza kusudio langu la kutoa Hoja ya Kuundwa Kamati Teule ya Bunge chini ya masharti ya Kanuni ya 120(2).

Naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kuunda Kamati Teule ya Kuchunguza na Kuchambua Sera mbalimbali zinazohusu masuala ya Ardhi, Kilimo, Mifugo, Maji, Wanyamapori na Uwekezaji ili kubaini kasoro zilizomo katika matumizi ya ardhi na hatimaye kuleta mapendekezo Bungeni, ambayo yakitekelezwa na Serikali, yatapunguza na kuondoa migogoro ya muda mrefu inayoendelea kati ya wafugaji na wakulima na hifadhi, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule itakuwa na kazi zifuatazo:-

Moja, kuchambua Sera mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi ili kubainisha kasoro zilizomo kwenye Sera hizo;

Mbili, kuchunguza mikakati ya utekelezaji wa Sera hizo iliyowekwa na Serikali;

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P. M. MSOLLA]

Tatu, kuchambua mikakati yote ya Serikali ya kusuluhisha migogoro ya wakulima na wafugaji;

Nne, kuchambua mikakati ya kulinda vyanzo vya maji pamoja na uharibifu wa mazingira;

Tano, kutoa mapendekezo yatakayoondoa migogoro iliyopo na kudumisha uhusiano mzuri na utengamano kati ya wafugaji na wakulima; na

Sita, mambo mengine yoyote ambayo Kamati itaona yanafaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja litolewa iamuliwe)

SPIKA: Ahsante. Hoja hiyo imeungwa mkono, sasa tuiamue. Mheshimiwa Mnyika, naona umesimama wa kwanza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, naomba kupendekeza kwamba, hoja hii ijadiliwe kwa maana ya kuboresha hadidu rejea za kufanywa na Kamati Teule hii. Kwa hiyo, kama nitapewa nafasi ya kuchangia...

SPIKA: Ndiyo tunajadili hivyo, hoja imeshaungwa mkono ndiyo tunajadili hivyo. Wewe si ndiyo msemaji wa kwanza?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Pia na Mheshimiwa Mtutura.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ningeomba pia mwongozo wako kuhusu muda wa kuchangia.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Dakika tano.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Spika, mtoa hoja ameeleza hadidu rejea za Kamati na zimejikita katika uchambuzi wa Sera, uchambuzi wa utekelezaji wa mikakati na kutoa mapendekezo na kushughulikia mambo mengine. Hata hivyo, tunatambua kwamba, nchi hii imekwishawahi kuunda Tume na Kamati mbalimbali zilizoshughulikia masuala ya ardhi na Kamati au Tume mojawapo ikiwa ni ile iliyoongozwa na Prof. Issa Shivji, pamoja na vyombo vingine ambavyo vimeundwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependekeza kwamba, katika hadidu rejea za kazi ya Kamati hii Teule, Kamati hii ipewe kazi ya kufanya mapitio ya Taarifa nyingine za Kamati na Tume zilizoundwa huko nyuma kushughulikia jambo hilihili ili kuepusha Kamati kurudia kufanya kazi pale ambapo tayari kazi ilishafanyika ila utekelezaji wa mapendekezo ndiyo umesuasua. Kwa hiyo, ili jambo hili liweze kutokea ni muhimu katika hadidu rejea za Kamati suala la kupitia taarifa nyingine likatajwa bayana.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni muhimu sana kwa sababu kumekuwa na kawaida ya kuundwa kwa Tume mbalimbali, lakini Ripoti zake zinafanywa kuwa siri na utekelezaji wa mapendekezo yake haufanyiki kwa ukamilifu. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kwanza ambalo ni muhimu likaongezwa kwenye hadidu rejea za Kamati.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Kamati imesema kwa ujumla kwamba, itatoa mapendekezo baada ya kuwa imefanya mapitio ya kisera, lakini katika mjadala wa Waheshimiwa Wabunge, uliophelekea kutolewa hoja ya kuundwa kwa Kamati hii Teule, Waheshimiwa Wabunge wametaka uwajibikaji pale ambapo kasoro za utekelezaji wa kisera zimetokana na udhaifu wa kiuongozi na utendaji.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

Mheshimiwa Spika, katika hadidu rejea hizi zilizo hivi sasa haijitokezi bayana iwapo Kamati hii vilevile itashughulikia, maana msingi wa Kamati ni kushughulikia masuala ya Sera, kama inashughulikia Sera ni muhimu vilevile ikashughulikia uwajibikaji pale ambapo kuna kasoro za kiutendaji ili azma iliyozungumzwa na Wabunge kwa lugha ya ukali sana ya kutaka uwajibikaji wa waliohusika kutufikisha hapa tulipofika iweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nalo ni muhimu likajitokeza katika hadidu rejea za Kamati ili Kamati itakapokwenda kufanya kazi yake na kutoa taarifa kwa Bunge, jambo hili lisipojitokeza ionekane bayana kwamba, Kamati Teule imekwepa kulishughulikia kwa sababu kwa namna mapendekezo yalivyo, hili halitafanyika kwa ufanisi kama halijajitokeza.

Mheshimiwa Spika, nikimalizia niseme kwamba, Kamati imezungumzia utekelezaji wa mikakati na tafsiri ya mikakati ya Serikali inafinya wigo wa Kamati kushughulikia masuala ambayo yatatupatia suluhisho la kudumu. Nimepitia Mpango wetu wa miaka kumi, hapa nazungumzia Mpango, sizungumzii Mikakati; ni wazi kwamba, Mpango wetu wa Maendeleo iwapo ungetekelezwa kwa kutengewa bajeti ya kutosha kama ilivyoainishwa katika Mpango wenyewe, tusingefika hapa tulipofika. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile pamoja na mikakati Kamati Teule ipewe kazi vilevile ya kupitia Mipango.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kupata ufafanuzi kutoka katika Meza yako, hili ni nje ya hadidu rejea. Wachangiaji waliochangia walikumbusha vilevile maamuzi yaliyofanywa na Bunge kufuatia hoja binafsi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Halima Mdee, nayo kimsingi yalihu suala hili hili la matumizi bora ya ardhi na masuala ya uendelevu katika matumizi ya ardhi. Taarifa ile Serikali ilipaswa iwasilishe mrejesho wa utekelezaji Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni muhimu basi kabla Kamati hii ya Bunge Teule haijaanza kazi yake, Bunge hili

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MNYIKA]

Tukufu lipewe taarifa ya utekelezaji wa Serikali kufuatia hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee, ili yatakayojiri kutokana na mjadala huo nayo yakafanyiwe kazi na Kamati Teule ya Bunge kwa kadiri itakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista.

MHE. MTUTURA A. MTUTURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza, niunge mkono kabisa, uundwaji wa Kamati Teule na niseme tu kwamba, hapa tulipofikia ni baada ya kutokea kwa vifo vya watu. Suala la vifo vya watu ndilo lililogusa zaidi hisia za Wabunge mpaka wakaona kwamba, kuna haja ya kuunda Kamati Teule ya Bunge. Pamoja na ng'ombe kuuawa kwa risasi, kitu ambacho ni aghalabu kwa nchi yoyote duniani hapa kwa sababu hakuna asiyefahamu katika dunia hii kwamba, miongoni mwa wanyama wanaofugwa mnyama mpole sana ni Kondoo na Ng'ombe. Leo ng'ombe anauawa kwa risasi eti tu amekula nyasi za Serikali, jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa na mtu yeyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe, hata kwenye *Hansard* ipo, haya yote ambayo Wabunge wamezungumza leo, mimi niliyazungumza katika Bunge la Bajeti. Yote haya nimeyazungumza, lakini kwa kuwa waliofanyiwa vile ni Watu wa Tunduru mpakani na Msumbiji, hakuna aliyeguswa na hakuna Mbunge hata mmoja ambaye aliunga mkono yale niliyoyazungumza. Leo wameuawa wale ambao wanaonekana kwamba wana damu ya kibinadamu, nadhani Bunge zima limetikisika.

Mimi namshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa sababu yale yote niliyoyazungumza kwenye Bunge la Bajeti leo yamedhirishwa hapa. Kwa hiyo, siyo sahihi na siungi mkono Tume hii kushughulikia masuala ya ng'ombe na wakulima peke yake bila kuhusisha damu ya Watanzania

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. A. MTUTURA]

iliyomwagika eti tu kwa sababu ya kivuli cha kulinda Tembo, haiwezekani! (Makofi)

Siyo sahihi kabisa, naomba suala hili la watu kuuawa ambalo kwa bahati nzuri hata majina kwenye Jimbo langu niliyafikisha kwako Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, nashauri kwamba, pamoja na hadidu za rejea ambazo zimetamkwa na Mwenyekiti, ziongezwe hadidu za rejea zinazohusu kuuawa kwa watu kwa kisingizio kwamba, tunalinda Tembo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili limeifedhehesha nchi yetu na Serikali yetu. Kama yale niliyoyazungumza mwaka jana yangeweza kufanyiwa kazi, leo tusingefika hapa. Nimeomba mara chungu nzima Serikali ije Tunduru, ijaribu kutathmini ile operesheni, maana yake operesheni hii ya wenzetu ninyi ni ya kwanza, lakini sisi Tunduru hii ni ya pili na mambo yaliyofanyika katika operesheni ya kwanza ni ya hatari zaidi kuliko haya. Nimesema hapa Bungeni nikaonekana mimi ni jangili, nikaanza kushambuliwa kwenye magazeti, naandikwa sijui nina bunduki tatu, sijui hizo bunduki tatu aliniuzia nani!

Mheshimiwa Spika, udhalimu mkubwa sana umefanywa ambao hauwezi kuvumiliwa. Naunga mkono yale yote aliyoyazungumza Mheshimiwa Mnyika yaongezwe na hili suala la kuchunguza idadi ya watu walioteswa na waliouawa nayo iingizwe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Jenista Mhagama.

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Mheshimiwa Prof. Msolla na nimpongeze kwa kutuletea hoja hii Bungeni, ambayo itatusaidia kufikia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

hitimisho la mgogoro huu mkubwa ambao upo katika nchi yetu kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa nataka kusema, kwa utangulizi kabla sijasema yale niliyokusudia kuyaongeza, nilikuwa nasema katika msingi wa maendeleo ya Taifa letu ukiutazama kwa ujumla wote tunatambua kwamba, Taifa hili la Watanzania haliwezi kusema kwamba lina uwezo wa kupiga hatua za maendeleo bila kujali Sekta ya Kilimo. Hata hivyo, Sekta ya Kilimo si kwa maana ya kilimo peke yake, bali ni kwa maana ya kilimo na ufugaji kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi ni Sekta mbili ambazo huwezi kuzitenganisha kwani zinakwenda sambasamba. Kwa hiyo, kama kukiwa na jaribio lolote lile la kuharibu Sekta mojawapo kati ya sekta hizi mbili, hakika ni lazima tukubaliane kama Watanzania tutakapokwenda kuangukia ni kuyumba kwa uchumi wa nchi yetu na ndiyo maana unaona Mheshimiwa Spika, ninaanza kwa kusisitiza kwamba, hoja hii ni ya msingi kwa sababu itakwenda kuweka uwanda mzuri wa kupunguza migogoro na kuiondoa kabisa kama itawezekana, migogoro hii mikubwa baina ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wameuawa lakini na wakulima nao wameuawa katika hatua nyingine tofauti. Wafugaji mifugo yao imepata madhara makubwa, ng'ombe wamepigwa risasi na wamekufa, ni maumivu makali sana. Kwa upande mwingine, mashamba makubwa ya wakulima katika nchi hii yameteketee kabisa. Watu walichukua mikopo mikubwa wakawekeza kwenye ekari nyingi sana za mashamba yao wakitumaini kuvuna mazao mengi sana, lakini kwa kuwa hatukuwa na utaratibu maalum wa kujijali sekta hizi mbili kama ni sekta za kuleta maendeleo kwenye uchumi wetu, ulikuta maeneo mengine mashamba makubwa ya Wananchi yameteketee na wameishia kwenye hasara ya mikopo mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hali ya namna hii, unaangalia upande wa kushoto unakuta kuna tatizo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

kubwa la wakulima. Unaangalia mkono wa kulia unakuta kuna tatizo kubwa la wafugaji. Wafugaji wamehangaika, wameuawa na wamepoteza mifugo yao. Wakulima wamehangaika, wameuawa na wamepoteza mali na mashamba yao makubwa. Katika hilo sisi kama Wawakilishi wa Wananchi hatuna budi kusimama na kuhakikisha tunaungana na hoja hii ili kuweka nafasi nzuri sasa ya kutafuta mwafaka. Hawa wote wafugaji na wakulima ni Raia wa Tanzania na wanatakiwa kuchangia mchango mkubwa sana katika kuleta maendeleo ya Taifa letu la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, nilikuwa nafikiri mambo mawili au matatu, yangefanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nilifikiri Kamati hii ingepewa muda maalum wa kufanya kazi. Kwa sababu mtoa hoja amekwenda tu, sijui Kiti chako kitatuongoza, lakini sidhani kama tuiache tu Kamati hii ifanye kazi kwa mujibu wa hoja yake? Nadhani tungepeana muda maalum suala hili lifanyiwe kazi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu leo Serikali imetoa kauli ya kusimamisha hizo operesheni zote, nini kinakwenda kufanyika kuwafanya hawa wafugaji na wakulima wakae watulie wawe katika hali ya amani na wasiingiliane katika hayo majukumu yao tena? Mwingine asiumizwe huku na mwingine asiumizwe kwa upande huu wa kushoto, kulia na kushoto kote kubaki na amani kukisubiri maamuzi mazito yatakapopendekezwa.

Kwa hiyo, nadhani kuna umuhimu wa suala hili kufanyiwa kazi kwa haraka kadiri iwezekanavyo, lakini kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kingine nilichokuwa nataka kupendekeza ni kwamba, kwa kuwa tumeshapata taarifa na tunafahamu Tume nyingi zimeshaundwa kushughulikia masuala haya, lakini hatujaona matokeo ya Tume hizo katika utekelezaji wake. Nadhani tukubaliane kwamba,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. J. MHAGAMA]

haya yatakayokwenda kufanywa sasa hivi kama ni Tume, maazimio au utekelezaji, uwe ni wa mwisho, usitoe nafasi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda umekwisha, ninaomba niseme kwamba, ninaunga mkono hoja hii na nishauri Wabunge waunge mkono hoja twende kuunda hiyo Tume.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Ninamwita Mheshimiwa Moses Machali.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nami kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia juu ya hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba niungane na Mheshimiwa Prof. Msolla, kwa mawazo yake ambayo ameyatoa, isipokuwa ningependa pengine na mimi niweze kuongeza jambo moja katika hadidu za rejea.

Mheshimiwa Spika, moja ni kwamba, kwa sehemu kubwa ukiangalia wachangiaji wengi walijikita kwenye kuangalia matatizo ambayo yamewakuta wafugaji wa ng'ombe pamoja na mifugo yao. Ni kweli kwamba, kitendo kilichofanywa na maafisa ambao wanahusika na operesheni hizo ni zaidi ya ugaidi wa kawaida na jambo hilo halikubaliki. (*Makofi*)

Watu hao wanapaswa wachunguzwe vizuri na ikiwezekana pengine twende mbali, tuweze kuwapima akili zao, kwa sababu haingii akilini unatumia risasi kwenda kupiga ng'ombe. Hiki ni kitu ambacho kiasi fulani hakiingii akilini kwa mtu yeyote ambaye ana akili timamu.

Mheshimiwa Spika, ningependa niongeze jambo moja. Suala hili liende sambamba katika hadidu za rejea, kwenye kwenda kuangalia wakulima ambao nao waliondolewa katika maeneo ambayo Serikali imekuja ku-*claim* baadaye kwamba ni hifadhi. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J. MACHALI]

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo yametajwa ni Hifadhi na Serikali, lakini wakulima wamekuwa wanalima kwa zaidi ya miaka thelathini na kuendelea kwa miaka mingi sana. Haya yamejitokeza hata kule kwetu, Serikali ikasema inafanya operesheni, baadhi ya watu wamekamatwa, wamenyang'anywa rasilimali zao, vyombo vya usafiri kama pikipiki, baiskeli na wengine wamechomewa majumba kwenye Wilaya zetu za Kasulu na hata kule Uvinza hali kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili isijekuwa ni kwenda kuangalia tu ng'ombe waliouwawa, twende mpaka tukaangalie wakulima na wengine leo hii wamefunguliwa kesi na wamefungwa vifungo visivyopungua miezi sita wako gerezani. Sasa kwa kuwa dhamira ya Serikali imeonesha kuwa hawa ng'ombe waliokuwa wamekamatwa sasa waachiwe. Ningependa hili suala tuliangalie ni vipi hawa watu ambao Serikali wamesema walikuwa kwenye Hifadhi wakilima kwa zaidi ya miaka thelathini, kama kule kwetu Kigoma ambao wamekamatwa na wamehukumiwa kwa maagizo ya baadhi ya Viongozi wa Serikali, akiwemo Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, ambaye ndiye alikuwa kinara katika kuongoza suala hili.

Naomba suala hili liangaliwe, hii *aspect* ya wakulima ambao wameondolewa kule nao tuangalie suala hili tunalifanyaje.

La mwisho, ningependa katika kushughulikia uchunguzi wa masuala haya, Kamati yako ambayo pengine utakwenda kuiunda baadaye, uhakikishe unaweka watu ambao watakuwa imara ambao hawataweza kumwonea aibu mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru ninaomba kuishia hapa. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Injini Mnyaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Kakoso!

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, kwa nia ya kuunga hoja ya Mheshimiwa Profesa Msolla ya kuundwa *Select Committee*. Kitendo tutakachokifanya au Bunge hili likiunda Kamati Teule, tutakuwa tumetimiza viapo vyetu tulivyoapa hapa Bungeni kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Toleo la Mwaka 1977, Ibara ya 18 (a), (b), (c) na (d), ambazo zote zinazungumzia namna ya Haki za Binadamu na kulinda masilahi ya binadamu, ambayo yameonekana kuvunjwa kwa kiasi kikubwa.

Siyo Ibara ya 18 tu, Ibara ya 24 ambayo inataka mtu alindwe na mali zake, katika matukio haya kuna watu wamenyang'anywa mali zao. Hata lile tukio la Mchungaji wa Katavi aliyekimbia vishindo hivi akaacha Biblia yake na shilingi laki nane ndani, baada ya kurudi siku ya pili yake akarejeshewa Biblia lakini shilingi laki nane hazikuwepo. Kwa hiyo, watu wamenyang'nywa mali zao.

Siyo hilo tu, zimetumika lugha za ugaidi, watu kusingiziwa ugaidi. Waliosingiziwa ugaidi na wale waliosingizia kuwa hawa ni magaidi, inafaa hadidu za rejea ziende mbali sana kuthibitisha ugaidi wao au kutokuwa magaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna watu Kanda ya Ziwa wasiopungua thelathini ambao wameuwawa na wengine ni walemavu, ambao wanatoka Muleba, wanaotoka maeneo ya Geita, wanaotoka maeneo ya Chato na ikafika *stage* kuna watu binafsi wakalalamika wakaanza kufanya *research* wakamwandikia barua Mkuu wa Mkoa wa Geita na Mkuu wa Mkoa wa Geita akajibu barua hiyo tarehe 21 Juni, yenye kielelezo *GTA/CA/20/6/17* kuthibitisha amepokea na suala hili ni zito mauaji yamefanyika.

Sasa kuundwa kwa Kamati Teule kutasaidia pia na hawa watu ambao walijitolea wenyewe binafsi kabla ya kuundwa Kamati Teule, wakaweza kufanya hiyo kazi na Mkuu wa Mkoa wa Geita mpaka leo ameshindwa kujibu na amethibitisha matukio mengi yametokea ila uchunguzi

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. H. J. MNYAA]

ufanywe zaidi. Kwa hiyo, hili litasaidia na kuona kuwa haki za wale watu zitendeke kwa sababu maiti zimepatikana zilizookotwa katika Ziwa Victoria, lakini badala ya kufanyiwa *postmortem* zimekwenda kuzikwa *direct* hata uchunguzi wa kawaida wa maiti zile haukufanyika; kulikuwa kunafichwa nini?

Kulikuwa na mipango mingi na watu kusingiziana na mambo ya ajabu, kiasi kwamba, ilikuwa ni tishio na hali ya kutisha kwamba Haki za Binadamu zilikuwa zimevunjwa kwa hali ya juu.

Bunge litakapounda Kamati Teule, itakuwa tumerejesha au tumetunza, tumetii Kiapo chetu na kulinda haki za Watanzania hawa ambao wamedhulumika, aidha kwa mali zao, kwa maisha yao na wengine walemavu. Hawa walemavu itafutwe namna ya kuwawezesha kuendelea kuishi baada ya kutiwa ulemavu ambao hauna sababu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Laizer!

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Profesa Msolla. Ninaafiki kabisa mapendekezo yake ambayo yametolewa.

Mheshimiwa Spika, hali ya operesheni iliyofanyika katika nchi nzima, imekiuka maadili ya utu wa nchi hii. Mambo ambayo wamefanyiwa Wananchi yanahuzunisha sana, yanasikitisha kiasi kwamba, hata kuyaeleza unaona aibu kuwa Serikali hii ambayo imechaguliwa na Wananchi, lakini kitu ambacho wanawafanyia Wananchi ni tofauti sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. S. KAKOSO]

Eneo la Kijiji cha Kabage kumechomwa Kijiji kizima. Ninapozungumza hivi sasa, Wananchi hawana mahala pa kuishi, karibu kaya 950 zimechomwa na zaidi ya Wananchi 10,000 hawana mahala pa kuishi. Kijiji hicho ni Kijiji halali ambacho Serikali inakitambua. Kijiji hicho kina usajili ulio halali lakini inasikitisha kuona, Serikali kwa makusudi inawahadaa Wananchi ambao iliwaidhinisha waishi katika maeneo hayo na kwenda kuwachomea, ikiwa ni pamoja na kuchoma vyakula ambavyo wao wanategemea katika kuendesha shughuli zao za maisha pamoja na watoto wao.

Mheshimiwa Spika, Kijiji kingine ni Kijiji cha Nkungwi, Kitongoji cha Rutuba, kimechomwa moto na operesheni ambayo kimsingi ninashindwa kuelewa nini vigezo vilivyotumika kwenda kuwachomea Wananchi ambao hawana hatia ya aina yoyote na wala hakuna majangili ambao walikuwa wanafuatwa katika maeneo hayo. Eneo hili bila kuangalia utu wa ubinadamu, ninaomba Serikali ipeleke msaada haraka wa kuwasaidia wale Wananchi ambao hawana mahala pa kuishi na hawana chakula kwa sababu Serikali imewachomea.

Eneo lingine ni la Kitongoji cha Mnyamazi, Serikali imeenda kuwachomea Wananchi ambao wanakaa zaidi ya miaka ishirini wako pale, eti kwa kisingizio wanaishi katika maeneo ambayo ni hifadhi wakati siyo kweli. Eneo hilo Serikali inalitambua, wamekuwa wakifanya shughuli zote za Kiserikali muda wote, lakini Serikali imeamua kwenda kufanya vitendo ambavyo ni vya aibu, vitendo vya ubakaji vimefanyika katika eneo hilo, kiasi kwamba unashindwa kuamini wale walioenda kufanya operesheni ndiyo kweli walitumwa na Serikali waende wakabake watu, waende wakachome nyumba za watu!

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iteue Tume ambayo itakuwa makini kuangalia hali halisi; vinginevyo, mkituma watu ambao hawatafuatilia kwa ukaribu zaidi itakuwa siyo haki. Ninaomba sana Serikali ifanye kile ambacho kitawasaidia Wananchi. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

SPIKA: Muda wako umeisha.

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba sasa mmeanza kujadili, ninaomba mjadili hadidu za rejea, bado mtahitajika kutoa ushahidi kwa Kamati hii kwa mengi mliyonayo, kwa sababu mtaisadia Kamati kufanya kazi zake.

Mheshimiwa Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Mangungu, halafu Mheshimiwa Kiwanga.

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nieleze maeneo machache ambayo nilitaka yaongezwe katika hadidu za rejea.

Kwanza, ninaungana na Wabunge wote walioongea. Ninataka itafutwe ni kwa nini operesheni hii imegeuzwa badala ya kutafuta majangili wakaanza kuwapiga wafugaji na kuua mifugo; ni nani aliyewatuma wafanye kazi hiyo? Hizi ni kazi mbili tofauti, kitafutwe kiini kwa sababu ujangii na kuua mifugo ni vitu viwili tofauti.

Nikirejea yaliyosemwa na Mawaziri asubuhi, kuna maeneo ambayo yanastahili kutafutiwa ufumbuzi wake; Waziri wa Mifugo alisema asubuhi kuwa, maeneo ya ufugaji yamekuwa yakipungua mwaka hadi mwaka kwa ajili ya idadi ya watu, mifugo, wanyamapori, kilimo; ni kweli ndivyo ilivyo; sasa je ni nini kifanyike ili hili tatizo lisitokee tena? Suala hili la kuua mifugo ndiyo ufumbuzi?

Jambo lingine tuambiwe hekari zilizopimwa milioni moja laki mbili na themanini na nne elfu, mia mbili na nane ambazo zimepimwa kwa ajili ya ufugaji; hivi ni mimi tu ndiyo sifahamu eneo hilo liko wapi? Kwa sababu eneo ambalo ametuambia hakuna eneo linalofahamika kama Hifadhi ya Serengeti, Hifadhi ya Tarangire na maeneo mengine. Kama kuna maeneo ambayo yanaeleweka kabisa hili ni kwa ajili ya ufugaji lisingiliwe, hilo lifahamike.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. L. LAIZER]

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Serikali itazame mapori ambayo hayana wanyama tena, lakini bado yanalindwa; na kama yapo maeneo kama hayo, basi hayo yawe maeneo mengine ya kupimwa kwa ajili ya mifugo. Mimi nilitaka kuongezea maeneo hayo kwa sababu siyo mjadala ni maeneo ya kwenda kutazamwa, nataka yatazamwe.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mangungu, Mheshimiwa Kiwanga na Mheshimiwa Kalogeris atakuwa wa mwisho.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Nianze kwa kuunga mkono hoja hii ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Profesa Msolla. Ningependa katika nyongeza ya hadidu za rejea ambazo zimewekwa, moja kati ya wahanga ambao wameathirika na operesheni hii ni Wakazi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini katika maeneo ya Mitole, Njinjo, Kandawale pamoja na Miguruwe na kwa upande wa Kilwa Kusini ni Nanjilinjji.

Mimi nitapenda pia pamoja na mambo mengine, Kamati utakayoiunda itakayothibitishwa na Bunge hili, pia ifanye tathmini jinsi gani ambavyo Wananchi wameathirika na uhaini huu uliofanyika na unyama uliofanyika dhidi ya binadamu. Pia iangaliwe namna ya kuweza kuwafidia; wapo watu ambao wametumia gharama kubwa kwenda kujitibia hospitalini, wengine wamepata ulemavu wa kudumu, wengine wameathirika na mpaka sasa tunavyozungumza, watu wanaishi maporini na watakosa chakula kwa sababu hiki ndicho kipindi cha kuandaa mashamba na kipindi ambacho watu walitakiwa wawe wamekwenda kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo kwenye hoja ambayo imewasilishwa asubuhi na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ukisoma ameanisha kuwa, sababu za kuwepo kwa operesheni hii ilikuwa ni pamoja na umuhimu wa kulinda

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. A. MANGUNGU]

heshima ya Taifa letu mbele ya Jumuiya ya Kimataifa kwa kuthibitishia Ulimwengu kuwa tuna nia ya dhati ya kupambana na janga la ujangili.

Nilitaka kuuliza hii Jumuiya ya Kimataifa inaangaliaje pale ambapo vyombo hivi vinakwenda kuwaumiza Wananchi wasiokuwa na hatia na wanahukumiwa kinyume kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 13(6)(e), ambayo inasema ni marufuku kwa mtu yeyote kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha?

Hili jambo tusilichukulie tu kwa ushabiki wa kisiasa, watu wamepoteza roho zao, watu wameumizwa, kwahiyo, kama alivyosema Mheshimiwa Mhagama, ninaungana naye, lazima kuwe na *time frame*. Hili tangazo ambalo Mheshimiwa Waziri leo amekiri hapa na kusimamisha hii operesheni, basi itamkwe na hiyo operesheni isimame mara moja mpaka pale Tume hii itakapokamilisha utaratibu wake na kuwekwa mambo sawa.

Vilevile yamekuwepo maeneo na tafsiri nyingi sana, wapo watu wa Tabora na Mikoa yote ya Lindi na Mtwara, haya maeneo yameainishwa kuwa ni Hifadhi tangu mwaka 1952 mpaka leo mipaka hii haieleweki. Kila mara ambapo watu wanaamua kwenda kulima au wanapoonza kuwa hili ni eneo letu la kulima, wanaambiwa wapo kwenye Hifadhi basi hata eneo hili la Bunge linaweza kuja kutafsirika kuwa ni eneo la Hifadhi pia. Tume hii ifanye uainishaji wa maeneo hayo. *(Kicheko)*

La mwisho kabisa, lazima ichunguze na iangalie ni kwa nini wanatumia jina la Mheshimiwa Rais vibaya. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Ninamwita Mheshimiwa Kalogeris, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Kiwanga wa mwisho.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MHE. INNOCENT E. KALOGERIS: Mheshimiwa Spika, nami ninashukuru kupata nafasi kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Sina tatizo na ninaunga mkono hoja ya Mwenyekiti wa Kamati kwa kuanzisha Tume Maalum ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika, ninadhani Bunge lako Tukufu lina wajibu sasa baada ya kilio hiki cha wafugaji, lakini kubwa zaidi; matatizo ya wakulima na wafugaji Bunge lako lingetambua kuwa ni Janga la Kitaifa. Katika hili ninaomba Serikali vilevile itambue kuwa, migogoro ya wakulima na wafugaji nchini ni Janga la Kitaifa, ambalo linatakiwa kufanyiwa kazi ya ziada na kazi kubwa kuhakikisha Wananchi wanaishi kwa amani na utulivu katika maeneo yao.

Pamoja na hadidu rejea ambazo zimeundwa, wengi waliozungumza ninaamini wanatoka maeneo ya wafugaji, mimi ninatoka katika maeneo ya wakulima Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro ni Mkoa wa Wakulima, Wakulima wananyanyasika sana na wao vilevile na wanateseka sana, hawana uhuru na hawana raha katika nchi yao. Wakulima wamefika mahali kwa uchache wa sauti yao au kwa unyonge wao wa kukosa fedha, inaonekana Serikali kama vile haiwasikilizi. Leo hii Wafugaji katika *style* ileile wamefika mahali wamelifanya Bunge mpaka tunataka kuunda Kamati Teule. Morogoro wakulima wamelala barabarani, wamechomewa nyumba zao, lakini hakuna kitu kilichofanyika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, pamoja na Kamati hiyo, mimi mchango wangu ni mfupi tu; nikuombe katika Kamati hiyo tafadhali Wajumbe wa Kamati watoke katika maeneo husika hasa Mkoa wa Morogoro Wabunge wawepo ili walau Kamati ikawasikilize wakulima, wananyanyasika vipi katika nchi hii na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, wakulima wanashindwa kulima, wanashindwa kujiongezea kipato kwa kazi yao ya kilimo kwa sababu ukilima wafugaji wanakuja wanakula mazao,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. I. E. KALOGERIS]

ukileta ubishi unapigwa na unanyanyasika. Moja katika hadidu rejea ambayo ninaomba Kamati yako, wapo wafugaji wakorofi ambao wanajulikana hawako kihalali katika vijiji husika, wameendelea kuwa ndiyo wao wakubwa wa kambi za mateso kwa wakulima wetu. Ninaomba katika hadidu rejea wafugaji hao waorodheshwe, wahojiwe, Wananchi watoe majina ya wafugaji hao na ikiwezekana hatua za Kisheria zichukuliwe dhidi yao. *(Makofi)*

Inaumiza na inasononesha, wenzetu wanazungumza hapa, wanazungumza kwa dhamira ya wapiga kura wao, lakini na sisi kule kama wapiga kura wetu wakiamua ni kwamba, CCM haipo madarakani. CCM haitakuwa madarakani na huu ni mtego na bomu kwa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mimi ni Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Morogoro, lakini ninadhani hata uchaguzi ujao, kwa kero hii wafugaji wanavyowanyanyasa wakulima kule, nina uhakika kuwa hatutopata viti. *(Makofi)*

Naomba sana Kamati hii Teule itakayoundwa na kama ombi langu utalisikiliza, ikajadili kwa kina tupate suluhisho la kudumu la migogoro ya wakulima na wafugaji. Kila mtu atimize wajibu wake katika kuendeleza nchi hii, apate kipato chake na familia yake, tuondoe umaskini, tuondoe ujinga na tupate kipato cha kutosheleza Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Kiwanga, msemaji wetu wa mwisho!

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, naunga mkono asilimia 101 kwenye hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Profesa Msolla.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. L. A. KIWANGA]

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maliasili, lakini tumezungumzia zaidi kuhusu wanyamapori na operesheni zilizokuwa kule. Mkoa wa Morogoro hususan Wilaya ya Kilombero na Ulanga na Kilosa, operesheni hii siyo ya mwanzo. Kama mliyokuwa mnasikia kwenye vyombo vya habari, operesheni zimekuwa karibu mwaka mzima au miaka yote, lakini unajuliza ni nani aliyewaruhusu wafugaji waingie ndani ya Mkoa wa Morogoro bila kuwawekea miundombinu ya kufuga vizuri ili wasilete ugomvi na wakulima? Ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi!

Nani anayefanya wafugaji haramu waingie na kugombana na wafugaji halali? Ni Watendaji wa Vijiji, Wenyeviti wa Vijiji wanaotokana na Chama cha Mapinduzi na Watendaji wa Kata; hilo halina ubishi. Nadhani wakienda huko kama watakuwa wakweli wataona na watapewa na ushahidi, ni rushwa iliyokithiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba katika hadidu za rejea hebu wakaangalie, kuna Kesi Namba 212 ya mwaka 2012 kati ya wafugaji wameungana na wakulima; ndiyo mara ya kwanza nimeona hiyo Wilaya ya Ulanga na Kilombero, wameungana wakulima na wafugaji, wanaishitaki Wizara ya Maliasili kwa kuweka mkuruzo bila kushirikisha wanavijiji mpaka vijiji vingine vimeingia katika hiyo Hifadhi.

Sasa ni vyema wakaenda, naongeza hiyo, wakachunguze kwa makini na watuletee usuluhishi. Mahakama ya Ardhi ilishatoa mrejesho kwa Wizara na kwa wakulima na wafugaji mwezi Agosti, 2013. Hata wenyewe Maliasili wanakiri kwamba, kweli wameenda kuweka ule mkuruzo mpaka kati ya hifadhi na wakulima na wafugaji hawakuwashirikisha na zoezi lilikuwa baya, lakini tangu mwezi Agosti walivyopewa hiyo taarifa na Mahakama ilivyoamua wakae pamoja wakashiriki kuweka mpaka, mpaka sasa watu wanaanza kulima, Maliasili, Serikali imekaa kimya wala haiendi. Sasa hivi watu wanaenda kulima na *order* ya Mahakama imetoka, lakini bado wanadharau na ushahidi upo. Serikali imeidharau Mahakama, ushahidi upo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. L. A. KIWANGA]

Mheshimiwa Spika, sasa waende wakachunguze watuletee majibu hapa. Hiki kiburi wamekipata wapi cha kudharau Mahakama, Mhimili mmoja kudharau Mhimili mwingine? Tatizo liko wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakulima sasa hivi wamekamatiwa matrekta yao. *Operation* zilivyokuwa zinaenda huko ushahidi upo, watu wamechomewa ndani ya nyumba zao, watoto wameuwawa, picha zipo na ushahidi upo. Mpunga umeteketezwa, vijiji vimeteketezwa, kwa hiyo, naomba wakaangalie hilo.

Waende kuangalia pia migogoro ya wawekezaji na wakulima wa kawaida, hiyo imeenea ndani ya Mkoa wa Morogoro. Naomba mwende mkaikazie hiyo hadidu ya rejea, karibu Wilaya zote kuna wawekezaji wamefuga mapori wanawakodisha wakulima, tunataka waje hapa tuwatambue ili tuone kama wanafanya kazi hiyo kihalali.

Mheshimiwa Spika, je, Wananchi wameshirikishwa kama Sheria inavyosema?

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema sana maana nitakuwa ninasema yale ambayo nikiiitwa kwenye hiyo Kamati, nitaenda kufanya kazi. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita mtoa hoja.

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuwashukuru sana, wachangiaji kumi wa hoja ambayo nimeitoa mchana huu. Wote kwa ujumla wao wameunga mkono kusudio la kuunda Kamati Teule ili ichunguze kwa undani migogoro ambayo imekuwa ikiendelea hapa nchini kwa muda mrefu kati ya wafugaji na wakulima. Vilevile kuhusiana na maeneo mengine ya wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi yamezungumzwa, nafikiri inatosha kusema kwamba, haya yote ambayo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P. M. MSOLLA]

yanazungumzwa kwa nia ya kuboresha hizo hadidu za rejea, yatazingatiwa. Yametajwa maeneo ambayo kwa kweli ni ya kimsingi, Taarifa za Tume zilizopita zimetajwa za Profesa Shivji, kwamba, tupitie Taarifa za Kamati zilizopita, ili yasijirudie yale yale badala ya kufanya kazi ambayo ni kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, walio wengi wamesema kwamba, wale waliohusika itafutwe njia ya kuhakikisha kwamba, wanawajibishwa kwa namna moja au nyingine. Vilevile imezungumzwa Taarifa ya Mheshimiwa Halima Mdee kwamba, hii nayo Taarifa yake na namna ambavyo imechukuliwa, ingefaa tupate maoni na yaweze kupitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamezungumza kwa hisia kali juu ya vifo vya watu na mifugo na kwamba, hili limewagusa watu wengi na limeleta hisia nyingi.

Limezungumzwa jambo la kuwa na muda maalum, kwa kuzingatia umuhimu wa jambo hili na kwamba, leo hii vilevile imetolewa kauli ya kusitisha Operesheni ya Majangili na kwamba, kama kazi ikikamilika mapema, ni dhahiri kwamba, amani na utulivu miongoni mwa Wananchi itadumu.

Vilevile wengine wamependekeza hususan Mheshimiwa Michael Laizer, kwamba, kama kuna maeneo nchini ambayo kwa sasa hivi hayatumiki kabisa na hayapo katika Mpango wa Maendeleo, basi maeneo haya yatazamwe ili yaweze kutumika kwa ajili ya shughuli aidha za wafugaji au wakulima, badala ya watu hawa kugongana katika eneo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la msingi ambalo ninafikiri linazungumzwa ni kwamba, kuwepo na utaratibu ambao kuanzia wakati Ripoti itakapotolewa, kuwepo na maeneo yanayojulikana kwamba, haya ni maeneo ya wafugaji na haya ni maeneo ya wakulima, ili kupunguza hii migogoro.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. PROF. P. M. MSOLLA]

Vilevile kumetolewa pendekezo la kwamba, kufanyike tathmini ya namna watu walivyoathirika na namna ambavyo wanaweza kupewa fidia kwa yale ambayo yamewakuta na kwamba, mipaka ya Hifadhi nayo ijulikane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Wabunge wengi wamezungumzia sana juu ya mifugo, lakini vilevile kuna waliozungumza kwa hisia kali juu ya haki za wakulima. Hili limezungumzwa sana na Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Morogoro; kwamba, huko nako kuna matatizo ambayo ni ya kipekee na kweli wengi ambao mtakuwa mmeshuhudia, hivi karibuni kumefungwa barabara kule Dumila na wakulima kwa sababu ya migogoro ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kukiri tu kwamba, haya yaliyoelezwa yataingizwa katika hizi hadidu za rejea, ili Kamati utakayoiteua iweze kuona namna itakavyoweza kujumuisha pamoja na haya mengine ili yote yaweze kupata majibu.

Nawashukuru sana wote waliochangia na kuunga mkono jambo hili kubwa ambalo limekuwa ni tatizo na kero kubwa kwa wakulima na wafugaji kwa muda mrefu katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeshatolewa na imeshajadiliwa. Sasa naomba pia nifanye ufafanuzi:-

Kuna Kamati ile ya Kawaida ya Maliasili, itaendelea na kazi yake ya kufanya tathmini na kuangalia jinsi Mpango ule wa Kupambana na Majangili ulivyopangwa. Ndani yake itashughulikia kama kulikuwa kuna uzembe ama kuna watu wanahusika katika kuondoa maisha ya watu kwa sababu ya uzembe, pia wao watatakiwa kufanya hiyo kazi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Kamati hii nyingine itaenda kuangalia kwa ukubwa wake suala zima la migogoro kati ya wakulima, wafugaji na mambo yanayohusu maeneo ya Hifadhi na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, pamoja na kuwa haitakwepa, maana kuna jambo lingine hapa mengineyo, haya mengine mliyosema hawatakwepa, mengine watayakuta, lakini kikubwa ninachoomba ni ninyi kushiriki katika kutengeneza haya mambo.

Baada ya kusema hayo, kabla sijawahoji, Mheshimiwa Mnyika, wewe ulikuwa unataka kusema nini? Siyo kunirudisha nyuma, hatujadili, *mind you*.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, ni kweli.

SPIKA: Kuhusu nini?

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru umetolea sehemu maelezo, lakini bado kwenye maelezo yamejitokeza maelezo ya kwamba, Kamati hii Teule, itahusika vilevile na masuala ya uhifadhi, ambayo kimsingi yako chini ya Kamati ya Maliasili. Ni vizuri ikawekwa bayana hapa, mipaka ya hizi Kamati mbili katika kazi hii kwamba, masuala ya Tokomeza Ujangili, Uhifadhi na mambo yote yanayohusiana na hayo, kushughulikiwa na Kamati ipi na masuala mengine yote ya wakulima na wafugaji kwenye maeneo mengine yote yashughulikiwe kivipi, ili kusiwe na mwingiliano baina ya Kamati hizi mbili katika kufanya hizo kazi.

SPIKA: Sawa, ni sahihi ulivyosema. Ndio maana nimesema kuna suala zima la ujangili, ile Kamati yetu ya Maliasili itahusika. Katika haya matumizi ya ardhi ni kama alivyosema Mheshimiwa Machali kwamba, kuna wakulima walikuwa wanaendelea kulima katika maeneo fulani, halafu baadaye Serikali ikasema huku sasa ni Hifadhi; hiyo itakuwa inaingia kwenye Kamati hii. Kwa hiyo, kuna hili suala la ujangili *per se* ndiyo ile Kamati yetu, lakini hili lingine litakwenda katika misingi hiyo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[SPIKA]

Waheshimiwa Wabunge, hamuwezi kujadiliana na mimi, sasa naomba niwahoji.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Hoja ya Kuunda Kamati Teule ya Bunge Kushughulikia Migogoro ya Wakulima, Wafugaji na Hifadhi Iliafikiwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, Kamati wote mmeafiki. Kamati tutaiunda, lakini majina ya wahusika tutayataja Siku ya Jumatatu. Katibu hatua inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015

(Majadiliano yanaendelea)

(Hapa Wabunge Walikaa kama Kamati ya Mipango)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama tungekuwa tumeanza asubuhi, tungepata wachangiaji kama 30, lakini kwa sababu tuna muda wa dakika 110, kutakuwa na wachangiaji kama 11 hivi. Nataka kumwita mchangiaji wa kwanza; Mheshimiwa Stephen Ngonyani simwoni, atafuatiwa na Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Mkosamali, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Mheshimiwa Bwanausi! Wengine nitawataja baadaye.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kushukuru kwa kupata nafasi na mimi ya kushiriki katika kuujadili huu Mpango wa Maendeleo ulioko mbele yetu. Tumekuwa tukipanga Mipango mingi sana, ambayo kwa asilimia kubwa imekuwa ikileta mafanikio katika nchi yetu, lakini zipo dosari mbalimbali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. D. BWANAUSI]

ambazo zimekuwa zikijitokeza ambazo tunapenda kwenye Mpango ujao zirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningependa kuchangia kuhusiana na matumizi ya Serikali. Niungane na Wajumbe wengine waliosema kwamba, kama hatutaweza kupunguza matumizi ya Serikali, hakika kasi yetu ya maendeleo itakuwa ndogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano mdogo tu katika Taasisi ndogo hapa nchini ambazo zimewahi kuamua kwa makusudi kabisa kutenga kiasi kikubwa zaidi kwenye maendeleo na kubana matumizi kwenye matumizi ya kawaida na kuleta tija, nayo ni moja ya Halmashauri ya Manispaa za Dar es Salaam, nayo ni Manispaa ya Temeke. Katika kipindi nilichoiongoza (2005 - 2010), tulifanya maamuzi magumu kuhakikisha tunatenga 60% kwa matumizi ya kawaida na 40% kwa matumizi ya maendeleo. Kwa hakika tulifanya mapinduzi makubwa na wale wanaokwenda Temeke sasa wanayaona Mapinduzi hayo, yalitokana na siri hiyo. Kwa hiyo, ninayo imani kabisa kwamba, kama Serikali itaamua kwamba, tupunguze matumizi ya Serikali, kasi ya maendeleo hapa nchini itaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni usimamizi. Moja ya jambo linalotuletea matatizo makubwa ni kukosekana kwa uzalendo kwa Watumishi na Watendaji wetu. Uzalendo wa kuipenda nchi umepungua kabisa. Asilimia kubwa ya Watendaji wetu, badala ya kushughulikia shughuli za nchi, wanaweka masilahi binafsi zaidi kuliko masilahi ya nchi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naweza nikasema Watanzania hatujalipa umuhimu mkubwa ni suala la nidhamu ya kuheshimu muda. Jambo hili kama hatukuendelea kuli-*address* vizuri hapa nchini, tukajali muda, kasi yetu ya maendeleo itapungua sana. Hili ndilo linalosababisha Mipango mingi ya Serikali na Mipango mingi ya nchi yetu kutoenda vizuri, kwa sababu asilimia kubwa ya wanaosimamia hawasimamii muda, hawaheshimu muda na kuhakikisha Mradi unaisha kwa wakati. *(Makofi)*

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. D. BWANAUSI]

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo niliona ni muhimu sana nilichangie ni la Mipango yetu. Wakati mwingine kuelemea kufanywa Kiwizara zaidi na kuacha kufanywa kwa ushirikiano; hii hupelekea baadhi ya Miradi wakati mwingine kukwama.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo vya maji; ninayo imani kabisa kama hatukuchukua hatua katika Mipango yetu, uzalishaji wa umeme utapungua sana. Kwa mfano, uzalishaji wa umeme Kidatu ni karibu *Mega Watt 200*, lakini maji ya Kidatu yanatoka Mtera. Sasa kutoka Mtera hadi kufika Kidatu, hapa katikati maji yale yamevamiwa na shughuli mbalimbali katika maeneo ambayo yanapita. Kwa hiyo, kuna hatari kwamba, wakati wowote kabla maji yale hayajawa *controlled*, mitambo ya Kidatu itazimwa. Kwa hiyo, ninaomba kwamba, Mipango ya Wizara; kwa mfano, Wizara ya Kilimo inapofanywa ni lazima iwasiliane na Wizara ya Nishati na Madini ili kujua jinsi yale maji yatakavyotumika. Hiyo hali imejitokeza pia hata kule Pangani, mtambo mmoja umezimwa kabisa, kwa sababu maji yale ambayo yalikuwa yanategemewa kuja pale sasa yanatumika kwa shughuli zingine na hivyo kupelekea hatari kwamba, mitambo ile inaweza ikazimwa. Kwa hiyo, ni vizuri mipango inapopangwa ikawa inawajibika katika Wizara mbalimbali ili kuhakikisha jambo linalopangwa linapangwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa ninafikiri nilichangie ni juu ya hatua zinazofanywa na Hazina kupeleka fedha katika mipango hii ambayo tunaipanga sasa. Fedha nyingi kwenye Miradi yetu huchelewa kufika na kusababisha Miradi hiyo kutotimia kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine juu ya masuala haya ya matumizi ya fedha ni katika suala zima la manunuzi. Taratibu zetu za manunuzi ambazo tumekuwa tukizikarabati mara kwa mara, bado nacho ni chanzo kikubwa sana cha Mipango yetu kutoenda kwa kasi kwa sababu ya urasimu wa jinsi ambavyo manunuzi yetu yanafanywa. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. D. BWANAUSI]

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia katika mpango huu ni kuishauri Serikali katika suala zima la mipango ya barabara. Niipongeze Serikali kwa jinsi inavyofanya kazi katika kusambaza mtandao wa barabara hapa nchini, kwa kweli kila mmoja ni shahidi jinsi Serikali inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini ninalo pendekezo kwa mfano, katika suala zima la barabara za mpakani katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji, Serikali imejitahidi kuhakikisha kwamba, tunajenga Daraja la Umoja kule Mtambaswala, lakini ili mtu wa Mtwara aweze kufika katika Mji wa Msimbua kule Msumbiji anapaswa atumie kilomita 400 kufika katika daraja lile la Mtambaswala.

Mheshimiwa Spika, tuna kilomita 40 kutoka Mtwara kwenda Kilambo ambapo kama Serikali ingeweza kuikarabati barabara ile ya kilomita 40 kwa kiwango cha lami, tungeweza kufika katika Mji huo huo wa Msimbua kwa kilomita 100 tu. Bahati nzuri kutoka mpakani mwa Tanzania, kutoka Kilambo kwenda Msimbua ni barabara ambayo inapitika katika kipindi chote cha masika. Kwa hiyo, ningependa hii barabara nayo itazamwe katika mipango ya Serikali ili tuone maeneo yale ya Mtwara badala ya kwenda kwenye mpaka kwa kilomita 400, basi tungeweza kutembea kilomita 40 kuweza kufika mpakani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni juu ya kasi ya utekelezaji wa miradi. Kwa mfano, barabara ya Ndundu-Somanga, ningependa kupata majibu ya Serikali, ile barabara imebaki si zaidi ya kilomita 30, lakini kwa sasa ni kama Mkandarasi amesimama, Serikali haina maelezo yoyote juu ya kusimama kwa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni moja ya barabara iliyojengwa kwa miaka mingi sana. Kwa hiyo, ningependa katika majibu ya majumuisho Waziri atueleze kwa nini barabara ile kwa sasa imesimama na wananchi hawana mategemeo tena ya barabara ile kwisha kama Serikali ilivyoahidi kwisha mwezi Disemba.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. D. BWANAUSI]

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nilikuwa nafikiri ni vizuri nikachangia ni juu ya uimarishaji wa barabara zetu ambazo zinaonekana ni za kiuchumi. Tunayo barabara muhimu sana ya kutoka Mtwara, Tandahimba, Newala mpaka Masasi. Barabara hii ipo kwenye mpango na mwaka huu ilitengewa fedha kidogo kwa ajili ya *feasibility study*, lakini kwa jinsi tunavyoona kasi ilivyo kule, ningependa katika bajeti ijayo barabara hii iweze kutengewa fedha ili tuhakikishe wananchi wa Mikoa hii ya Mtwara hususani katika Wilaya ya Mtwara, Newala, Tandahimba na Masasi waweze kunufaika na barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ningependa kuchangia katika suala la Viwanda vya Korosho ambalo Wajumbe wengi wameelezea hapa na kusikitishwa kwao kuhusiana na jinsi ambavyo jambo hili tusivyolfanya kwa mtazamo wa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la Viwanda vya Korosho vya kubangua hapa nchini, naweza nikasema ni vita kubwa sana, kwa sababu kwenye maeneo ambayo korosho ghafi zinanunuliwa kutoka Tanzania wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha korosho hatubangui Tanzania. Kwa sababu kule tunakopeleka ndiko ambako wananchi wake wanapata ajira, wanapata fedha za kigeni kutokana na zao hili. Naomba katika mipango ya Serikali, jambo hili ilipe umuhimu kama ilivyokuwa imejenga vile Viwanda 12 vya Korosho. Serikali iamue ifanye makusudi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, namwomba Waziri Mkuu, naomba Baraza la Mawaziri, wahakikishe kwamba wanakaa na kuona jinsi ambavyo wanaweza wakatenga fedha, liwe ni jambo maalum ili kuhakikisha tunafufua Viwanda hivi vya Korosho na hilo peke yake pia litamsaidia mkulima kuinua kipato chake na kuwafanya waanze kuondokana na umaskini ambao umegubikwa kutokana na bei ndogo ya zao la korosho.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. D. BWANAUSI]

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza haya ambayo niliona nichangie katika mpango huu wa maendeleo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Felista Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kuweza kuchangia katika ajenda iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inapopanga mambo mbalimbali au mikakati mbalimbali kuhusu maendeleo ya nchi, ni mategemeo ya wananchi kwamba mipango ile itatekelezwa kwa wakati muafaka. Serikali imeleta mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015 ili Wabunge wajadili na watoe mapendekezo yao ili Serikali itimize yale ambayo yatapendekezwa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, kwa siku za nyuma kuna baadhi ya mapendekezo ya Wabunge yametekelezwa, lakini kuna baadhi ya mapendekezo ya Wabunge hayajatekelezwa, mengine kwa miaka 40 sasa. Nasema hivyo kwa sababu hili ninalolisema linanigusa na linawagusa wananchi wangu wa Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nimepekua kitabu hiki kilicholetwa na Waziri wa Nchi, Uratibu na Mahusiano kinachohusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa, sikuona habari yoyote ya Serikali kujenga japo Wizara mbili, tatu katika Mkoa wa Dodoma. Suala hili lina miaka 40 tangu mwaka 1973 mpaka leo. Nimepekua kurasa moja baada ya nyingine na jambo ambalo halijawekwa kwenye mpango huu haliwezi kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, suala la kuhamia Dodoma limekuwa ni kitendawili, hivi kama haiwezekani si tuambiwe tu! Watoto wakifanya mitihani wakiulizwa Makao Makuu ya

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. BURA]

Nchi wakiandika Dar es Salaam wanakosea, wanaambiwa ni kosa mpaka waandike Dodoma, lakini wanapoandika Dodoma ni kiini macho tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilidhani ndani ya kitabu hiki nitakuta Serikali imetoa mapendekezo ya Wizara tano au sita kuhamia Dodoma, lakini hakuna kitu kama hicho. Tuambiwe, Serikali iwe wazi tu, kwa nini tunadanganywa kama watoto? Huu mradi wa kuhamia Dodoma ni mradi usiotekelezeka.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wanakuja kila baada ya miaka kumi, hakuna aliyewahi kutekeleza hili, nitaambiwa kwamba tumejengewa barabara, Mwanza wamejenga barabara kwa msaada wa *World Bank* kwani Mwanza ni makao makuu ya nchi; Mbeya wamejenga barabara kwa msaada wa *World Bank* kwani Mbeya ni Makao Makuu ya nchi? Kwa hiyo, nisiambiwe kwamba ujenzi wa barabara ni maandalizi ya Makao Makuu siyo kweli! Tuambiwe kama Serikali haitaki kuhamia Dodoma. Kwa nini suala hili limekuwa hadithi kwenye vitabu? Kwa nini mmeliacha kwenye vitabu jamani!

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama alijibu hili wananchi walisikie na siyo wananchi wa Dodoma tu, ni wananchi wa Tanzania nzima kwa sababu siyo Dodoma, ndiyo wanaojua kwamba Makao Makuu ya Serikali ni Dodoma, hapana! Ni mikoa yote Tanzania nzima tuambiwe ni lini Serikali hii itajenga ofisi za Wizara mbalimbali hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulikataa bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini walipoomba kujenga jengo kule Dar es Salaam tukakataa, lakini kwa sababu sijaona dalili yoyote ya Wizara ya Nishati kujenga Makao Makuu, Dodoma najua hilo ni funika kombe mwanaharamu apite, najua wanajenga Dar es Salaam sasa. Baadhi ya Mashirika ya Umma, baadhi ya Ofisi za Serikali, sasa hivi Ofisi ya Ushirika inahamia Dar es Salaam. Wanatoka Dodoma wanakwenda kupanga nyumba ya shilingi milioni mia nne kwa mwezi hapa wanakaa bure!

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. BURU]

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya kuhamia Dodoma imefutika, kama haijafutika tuambiwe huu mradi unatekelezeka lini na unaingizwa kwenye mpango upi kwa sababu kitabu cha mpango ninacho. Nitawapelekea wananchi wangu wasome maana leo wananisikia na yaliyoandikwa humu yameandikwa kwenye magazeti, wameshasoma na wanajua Serikali haina azma ya kuhamia Dodoma, ni maneno matupu.

Mheshimiwa Spika, nichangie pia jambo ambalo Wabunge wengi wamelizungumza kwamba, tunayo miradi mingi sana katika nchi yetu lakini haitekelezeki kwa wakati. Tulikuwa na Miradi ya Maji ya *World Bank*, Makandarasi wamepewa pesa nyingi lakini miradi mingi haijatekelezeka. Wananchi wamebaki wanahangaika kutafuta maji, miradi haijatekelezeka na tuna miradi mingi ambayo Wabunge wameizungumzia.

Mheshimiwa Spika, sisi Dodoma tuna mradi wa kujenga hospitali ya Mkoa pale, wodi ya wazazi, tangu mwaka 2008 mradi ule ulikuwa unagharimu bilioni 1.5, mpaka leo ule mradi haujakamilika, tangu mwaka 2008. Hii ni kwa sababu tuna miradi mingi, lakini hatuna pesa.

Mheshimiwa Spika, nimesoma kitabu hiki kilicholetwa na Waziri, anasema robo ya mwaka huu, robo iliyopita wamepeleka shilingi bilioni 94 tu kati ya bilioni 291 fedha za miradi. Hatuwezi kufanikisha miradi yetu!

Mheshimiwa Spika, katika miradi inayosimamiwa na Mikoa wamepeleka asilimia 17 tu. Miradi yetu haiwezi kutekelezeka kwa wakati kwa sababu ya upungufu wa fedha. Serikali iangalie namna ya kwenda na miradi michache ili miradi ile iliyopo itekelezeke na ikamilike.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ndiyo mnunuzi namba moja, bado Serikali yetu inakubali mapato yavuje kwa kutumia risiti ambazo hazijaidhinishwa na *TRA*. Kuna risiti

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. F. A. BURA]

ambazo zimeidhinishwa na TRA kwa sasa na Serikali inatakiwa itumie kwa manunuzi risiti hizi ambazo haziruhusu uvujaji wa pesa katika biashara.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama tulivyoona kwamba walipa kodi katika nchi hii ni watu milioni moja tu na laki mbili, kati ya watu milioni 44. Kwa hiyo, tukiacha mapato yaendelee kuvuja bado miradi yetu itasimama na bado miradi mingi haitatekelezeka kwa wakati. Kwa hiyo, ni lazima tubadilishe mtazamo.

Mheshimiwa Spika, pia nimeona katika sekta zinazochangia kwa wingi, sekta ya kilimo...

MWENYEKITI: Naona muda wako umekwisha.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Cecilia Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Jafo.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Mpango huu wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako lilipitisha Mpango wa Miaka Mitano na tathmini ya mpango huo kwa sababu sasa hivi tunaelekea mwaka wa nne kuutekeleza mpango huu, lakini tathmini ya kina ya miaka mitatu ambayo imepitishwa na Bunge lako, bado hatujaiona kwa usahihi na kwa upana na wala hakuna matumizi ya kina ya baadhi ya miradi ambayo iliainishwa katika mipango katika hiyo miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia uhalisia wa Mpango huu wa miaka mitatu na hali halisi kuna utofauti mkubwa. Yaliyoandikwa na utekelezaji unakuwa ni tofauti. Hii inatokana na kuwa bajeti yetu ni tegemezi, bajeti yetu kubwa inategemea wahisani walete fedha, bajeti yetu inategemea

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. D. PARESSO]

mikopo. Kwa hiyo, haiwezekani kuona maendeleo kwa haraka, hatuwezi kuona ufanisi wa hiyo mipango tuliyoipitisha. Kwa hiyo, naona ni vema tupate tathmini ya jumla ya miaka hiyo mitatu ya Mpango huo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini nikiingia kwenye suala la Utawala Bora, unaona kabisa suala la Utawala Bora halipo, hakuna uwajibikaji kwa watumishi wa Serikali, hakuna uwajibikaji kwa viongozi wa kisiasa waliopeva dhamana. Hii inatokana na kwamba tumezoea kufanya kazi kwa mazoea, wafanyakazi wa Serikali hawafanyi kazi kwa masaa yanayotakiwa. Mambo yote yanakwenda kama biashara inavyokwenda kawaida. Kwa hiyo, kama haya yasipobadilika na kutiliwa mkazo katika Mpango wa Taifa, hakika nchi hii haitaweza kupiga hatua na kusogea mbele.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho kinashangaza ni kwamba, Serikali hii imekuwa inaibuka na mambo bila kutafakari, kulikuwa kuna Mpango unaitwa MKUKUTA I ulikuwa utekelezwe mwaka 2000 – 2010, sijui imeishia wapi. Kukawa na MKURABITA ulikuwa utekelezwe mwaka 2002, kukawa na MKUKUTA II utekelezwe mwaka 2010, kikaja kingine kinachoitwa Kilimo Kwanza 2010, tukaja na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, lakini kikaja kitu kingine sasa hivi kinaitwa *Big Results Now* na mwakani sijui kitaibuka kitu gani kingine. Haya ambayo yanaibuka hayafikii mwisho, hayafanyiwi tathmini, hatujui matokeo yake. Huu ni udhaifu mkubwa sana wa Serikali ya CCM wa kushindwa kuangalia kwamba waanze na kitu gani, watoe matokeo, ndiyo wasogee kwenye kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye suala lingine la kazi na ajira. Ukiona katika utekelezaji katika *program* ya kazi na ajira katika Mpango wa miaka mitatu uliopitishwa, Serikali iliahidi kwamba itakuwa na *program* ya kukuza ajira kwa vijana, lakini hatujaona, vijana wa Kitanzania leo wamekosa matumaini. Vijana wanaomaliza Vyuo Vikuu hawana uhakika wa kupata kazi, hakuna hizo fursa za kupata kazi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. D. PARESSO]

Mheshimiwa Spika, wao wenyewe kwenye kitabu hiki cha Maendeleo wanakiri kwamba kuna tafiti imefanyika mwaka 2011, inaonesha kwamba sekta ya umma ni asilimia 36.9 ambao wamepata ajira rasmi na sekta binafsi ni asilimia 63.1. Kwa hiyo vijana ambao wanaweka matumaini kupata ajira nyingi zaidi kwenye sekta ya umma ndiyo inaaajiri kidogo kwa asilimia 36 tu, lakini kwa sekta binafsi unakuta ajira ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hata katika mpango huu ambao tunaujadili sasa hivi Serikali haijaonesha ni namna gani wanakwenda kukuza ajira, ni *program* zipi ambazo zitakuwa endelevu za kuwasaidia vijana kukuza ajira, kuna mwongozo unaozitaka Halmashauri nchini zitenge asilimia tano katika Mifuko ya Vijana, lakini hakuna kinachofanyika. Hatuoni vijana wakiwezeshwa, hatuoni vijana wakipata ajira, vijana wa Kitanzania wamekosa matumaini, lakini hata leo katika Mpango huu hakuna kilichooneshwa dhahiri ambacho tunaona kinakwenda kuwasaidia vijana.

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuchangia katika suala la ardhi. Mpango huu unaonesha kwamba, kutakuwa na suala la upangaji wa Miji na Vijiji pamoja na upimaji wa ardhi, lakini kuna migogoro mikubwa sana ya ardhi. Nashukuru Bunge lako limeongelea mambo haya na kutolea maamuzi kuhusiana na migogoro iliyopo, lakini ukiangalia Mpango huu, hakuna mpango mahsusi wa kuangalia migogoro na kutatua migogoro iliyopo ndani ya vijiji; migogoro kati ya wawekezaji ambao wana ardhi na wananchi, migogoro kati ya vijiji na hifadhi za Taifa zinazopatikana na migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Spika, hakuna mpango bora wa ardhi katika vijiji vyetu au katika Halmashauri zetu. Ukiangalia tafiti zinaonesha ni asilimia 11 tu ya vijiji ambavyo vina mipango ya ardhi na ni Halmashauri 20 tu nchini ambazo zina mipango bora ya ardhi. Kwa hiyo, hata katika Mpango huu bado hatujaoneshwa *serious* ni namna gani Serikali itakwenda kutatua matatizo haya ya migogoro ya ardhi. Kwa hiyo, bado hatuoni utayari wa Serikali kutatua migogoro ya ardhi.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. D. PARESSO]

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala lingine la afya na ustawi wa jamii. Sera ya afya inaeleza kwamba Zahanati kwa kila Kijiji, kituo cha Afya kwa Kata, hospitali kwa *level* ya Wilaya. Lakini kuwa na zahanati kwa maana ya jengo ni jambo lingine, kuwa na Madaktari, Manesi na madawa ni jambo lingine. Katika zahanati zilizoko katika vijiji, nyingi hazina dawa, kuna ukosefu mkubwa sana wa dawa, kuna uzembe katika uagizaji wa dawa, hatujaona mikakati iliyowekwa hapa na Serikali kuonesha kwamba ni namna gani dawa zinapatikana katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile hatuoni pia kipaumbele kinahotolewa katika bajeti ya afya. Bajeti ya afya imekuwa ni kidogo sana, hatujaona mikakati au mipango madhubuti ya Serikali hii kutaka kuwatibu Watanzania ambao wanatafuta dawa. Mwananchi anakwenda zahanati anakosa dawa, anakwenda kwenye maduka ya watu binafsi dawa inapatikana kuna nini hapo? Mwananchi analipa kodi kwa njia mbalimbali lakini hapati huduma inayostahili. Kwa hiyo, bado kuna upungufu katika Mpango huu, hawajaonesha ni namna gani wanakwenda kuhakikisha afya za Watanzania zinaimarika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni sheria na utoaji wa haki. Katika mpango wa mwaka 2012/2013, mpango ulionesha kwamba, kuna ujenzi wa Mahakama ya Kazi na Mahakama Kuu za Mikoa katika baadhi ya Mikoa. Lakini kuna tatizo lingine kubwa sana katika utoaji wa haki, kuna mrundikano mkubwa sana wa kesi hasa Mahakama za Mwanzo, ucheleweshaji wa kesi, ukosefu wa watumishi wa kutosha na vitendea kazi katika Mahakama zetu za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki yoyote inayocheleweshwa ni haki iliyonyimwa, hakuna mpango ambao unaonesha namna gani wanakwenda kumaliza mrundikano wa kesi. Wananchi wetu kila siku wanakwenda kwenye kuhudhuria kesi mbalimbali Mahakamani. Taifa ambalo wananchi wake kila siku wanahangaika na kesi Mahakamani na kurudi ni Taifa ambalo halitakaa liendelee. Ni Taifa ambalo wananchi wake wataendelea kuwa maskini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. D. PARESSO]

kwa sababu kila siku wanafuatilia kesi Mahakamani. Hakuna mpango madhubuti wa Serikali kuonesha namna gani inamaliza mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu. Namna gani Mahakama za Mwanzo zinaboreshwa, kwa sababu huko ndiko kwenye kesi nyingi zaidi ambazo zimerundikana.

Mheshimiwa Spika, nielezee suala la deni la Taifa. Ukisoma Mpango huu wanaelezea kwamba, deni linaendelea kukua na wao wenyewe wanakiri kwamba, deni linaendelea kukua, lakini ni himiilivu na wanasema katika matokeo ya uchambuzi wameonesha kwamba kuna umuhimu wa kuendelea kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukajiuliza badala watuletee taarifa kuonesha namna gani deni la Taifa linapungua, taarifa inakuja deni la Taifa linaendelea kukua na wao wenyewe wanakiri kabisa kwamba matokeo yao ya uchambuzi yanaonesha kwamba kuna uwezekano wa kuendelea kukopa, lakini hatujaletewa mikakati hapa namna gani hili deni la Taifa linapungua, badala yake tunaambiwa linazidi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tutaendelea kuona kwamba wanaendelea kukopa, kama hatuoni kwamba Serikali ina mkakati wa kudhibiti mapato, kudhibiti ukwepaji wa kodi, tutaendelea kukopa, tutakopa, wananchi wataendelea kuumia na mwisho wa siku wananchi Watanzania watahusika katika kulipa hili deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo kusema suala la mahitaji ya fedha katika bajeti. Katika bajeti ambayo imeoneshwa katika Mpango kwa bajeti 2014/2015 inakisiwa kuwa ni bajeti ya shilingi bilioni 19. Lakini ukienda kwenye mchanganuo wa bajeti hii ya bilioni 19; fedha za matumizi ni shilingi bilioni 14. Fedha za miradi ya maendeleo ni bilioni 5 tu. Kwa hiyo, ni aibu kuona asilimia karibu yote inakwenda kwenye matumizi. Asilimia kidogo sana inaendelea kwenye maendeleo. Ni lini Watanzania watapata huduma inayostahiki. Ni lini tutaacha matumizi makubwa ya Serikali

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. C. D. PARESSO]

hii ili fedha hizi zingine ziende kwenye maendeleo. Hatuoni Mpango huu ukituonesha namna gani tunakwenda kupunguza matumizi ya Serikali ili wananchi waweze kupata kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Jafo atafuatiwa na Mheshimiwa John Lwanji na Mheshimiwa Moses Machali ajjandae.

MHE. SELEMANI S. JAFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kukushukuru sana kunipa nafasi hii japo niongee machache jioni hii ya leo katika suala zima la Mpango wa Taifa. Lakini kwanza tunaambiwa kwamba, usipowashukuru binadamu wenzako, basi utashindwa hata kumshukuru Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujadili mipango toka tunaanza kuingia Bungeni hapa, mpango wa kwanza tulipojadili, tulipokuwa pale *St. Gasper*, lakini mpaka tumefikia hapa, kwanza nashukuru sana sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa sababu wakati tunajadili mipango na mimi toka nimekuwa Mbunge pale kwangu Kisarawe nilikuwa na changamoto nyingi sana. Lakini nashukuru sana Mipango ya miaka mitatu tuliyopitisha mpaka hivi sasa, nashukuru sana katika suala zima la umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunajadili mpango mzima lazima nitoe *analysis* huko nyuma tumetoka wapi. Kwangu Kisarawe tulikuwa na vijiji vinne tu vyenye nishati ya umeme, lakini leo hii wana Kisarawe tunakwenda vijiji 25. Kwa hiyo, kuna matarajio na namshukuru sana Profesa Muhongo alipokuja kuzindua mradi mkubwa wa umeme pale Kisarawe, kwamba sasa umeme utafika mpaka kule Vikumburu na mpaka kule Gwata maeneo ya ndani kabisa. Naishukuru sana Serikali katika hilo kwa sababu la msingi ni kwamba, tulikotoka ni mbali hivi sasa na mimi lazima nishukuru kama binadamu. (*Makofi*)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. S. JAFO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ni suala zima la afya. Kwetu kulikuwa na changamoto kubwa na kuna changamoto kubwa sana ya miradi ya afya. Nashukuru katika kipindi hiki Serikali ya Chama cha Mapinduzi imenisaidia sana, kutekeleza wajibu wangu. Leo nikikaa pale na Madiwani wangu tumepata ujenzi wa zahanati mpya nane kwangu napata faraja kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Serikali za Mitaa walivyokuja pale Kisarawe waliona dhahiri jinsi gani Mfuko wa Jimbo uliweza kujenga wodi ya wazazi au akinamama pale Maneromango. Kwa hiyo, haya yote yamefanyika kupitia mipango hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi namshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Hapa siku zile nilikuwa nazungumzia shida ya hospitali ya Kisarawe na hapa Mheshimiwa Mwanri alipokuwa akijibu swali langu la msingi na alikubali shida ya hospitali ya Wilaya ya Kisarawe kwamba haina *mortuary*, alituomba tutengeneze ombi maalum. Nashukuru sana Tume ya Mipango imekubali ombi letu lile la shilingi bilioni moja na milioni 500. Lakini namshukuru Rais, mpaka hivi sasa tumepata hivi sasa tumepata milioni 300 na tarehe 6 alipokuja alituhadi bilioni moja. Naiomba sasa Wizara ya Fedha ihakikishe inatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais alilolitoa alipokuja tarehe 6 pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi wenzangu wengine hapa asubuhi nimesikia wanalalamika Mahakama hawana. Mimi nashukuru sana Serikali hii imetengenezea Mahakama nzuri kweli kweli ambayo pale Kisarawe kwangu najidai hivi sasa na Mheshimiwa Angellah alikuja siku hiyo. Kwa hiyo, lazima nitoe shukrani katika maeneo hayo ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina shida ya maji na siku zote huwa nazungumza hapa. Kwangu Kisarawe maji ni shida, najua shida bado inaendelea, lakini hivi sasa kidogo angalau sisi Wazaramo kule tuna lugha moja tunasema

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. S. JAFO]

vivalume mmakono, kwamba huwezi ukajua unacho mpaka umekishika mkononi. Angalau sasa hivi badala ya kutoka vijiji sifuri sasa hivi tunakwenda karibu vijiji saba mpaka ifike mwezi wa kumi na mbili tutakuwa na miradi ya maji inayofungua maji ya bomba mitaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu nashukuru sana, lakini nawashukuru Wizara ya Maji kuhusu ile mradi ya visima 30 sasa vinaendelea kuchimbwa katika maeneo mbalimbali kule Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujielekeza katika Mpango wetu wa Taifa. Nashukuru sana Mpango huu unaainisha suala zima la bandari kavu ya Kisarawe. Nikiangalia bandari kavu ya Kisarawe najua kwamba, hapa tunakwenda kuufungua uchumi wa nchi yetu. Watu wanalalamikia sana foleni za Mji wa Dar es Salaam, lakini sababu ni kwamba, malori yote yanaingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam. Kama malori yanaingia katikati ya Jiji la Dar es Salaam maana yake ni lazima Jiji lile litakuwa na foleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mpango huu unavyoonesha kwamba kutakuwa na ujenzi wa bandari kavu ya Kisarawe, hii ni faraja kubwa sana kufungua uchumi wa nchi yetu. Katika hili nimwombe Waziri wa Uchukuzi na Waziri wa Ujenzi kwamba barabara ya Kisarawe iko pale eneo la Vihing'o, tuhakikishe basi kile kipande cha lami kinatengenezwa kuanzia pale Mlandizi mpaka kwenda maeneo ya Mzenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia inawezekana tufungue barabara kilomita 62 mpaka kufika Kisarawe Mjini tupunguze ikiwezekana hata malori sasa badala ya kupitia huku Kimara yapitie eneo la Kisarawe. Barabara hii ya Kimara, Mlandizi-Kimara-Dar es Salaam itumikie kwa ajili ya mabasi, hii itawasaidia sana Watanzania katika suala la foleni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapojadili Mpango huu lazima tujadili fedha tutapata wapi. Tuna matatizo makubwa katika upatikanaji wa fedha. Najjuliza hivi kwa nini tuwabane

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. S. JAFO]

watu wadogo na tuwaache watu wakubwa. Hainiingii akilini hata kidogo kuona katika Makampuni ya Madini kuna misamaha mikubwa ya kodi. Kwa kweli katika hilo nasema na nawashawishi Wabunge wenzangu katika Mpango huu kuimarisha suala zima la ukusanyaji wa mapato. Tuangalie katika Makampuni ya Madini jinsi gani tutapunguza misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza hasa katika suala zima la mafuta mazito yanayokwenda katika Makampuni ya Madini. Ukiangalia hapo ni kwa nini kodi ya mafuta mazito haitozwi katika Makampuni ya Madini. Naamini kwamba, tukihakikisha kama tunapata kodi katika maeneo haya, tutaweza kupata pesa nyingi kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni changamoto kubwa, naomba Waziri wa Fedha na timu yake wanisikilize katika eneo hili. Katika sehemu ya *Payee*, sasa hivi katika nchi yetu ukiangalia, naomba watu wa *TRA* wafanye *analysis* hiyo. Ukienda katika mashirika mbalimbali na makampuni mbalimbali kuna wafanyakazi wengine wanakatwa kodi, lakini kuna uwezekano mkubwa zile kodi za wafanyakazi haziendi Serikalini. Kuna wengine saa nyingine wanaajiri pengine watu 1,000, lakini kodi anayopeleka Serikalini pengine ya 250 au watu 300. Nini maana yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake mtu huyu au kampuni hii itakuwa imekusanya kodi kutoka kwa wafanyakazi, lakini inashindwa kupeleka kodi Serikalini na ndiyo maana kama mnakumbuka, nilileta maelezo yangu binafsi, kwamba, inahitajika kama ikiwezekana kila mfanyakazi akatwe kodi yake kupitia *TIN Number*, kwamba kila mfanyakazi apewe *TIN Number* yake. Unapompa mfanyakazi *TIN Number* yake maana yake tutakuwa na uhakika kwa kila mfanyakazi kuhakikisha analipa kodi yake na mapato yanakwenda Serikalini.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. S. JAFO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kulizungumzia ni suala zima la usimamizi wa pesa za Serikali. Ukiangalia Serikali inatenga pesa, lakini jinsi gani hizi pesa tunaweza kuzisimamia katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendekezo na nilitoa hoja binafsi pale, lakini ilionekana kwamba ilikuwa bado haijakaa vizuri. Ni suala zima tufanyeje, ikiwezekana tuanzishe itifaki ya usimamizi wa matumizi ya pesa za Serikali. Hili nililipendekeza makusudi, nilisema kwamba, katika Halmashauri, katika Taasisi mbalimbali ikiwezekana kuwe na utaratibu maalum kwamba Wasimamizi wakubwa wawe na fursa ya kutosha moja kwa moja kujua jinsi gani pesa zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Halmashauri ni kwamba, kuna vikao vya Kamati ya Fedha, lakini katika vikao vile...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha
kwa muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili hiyo.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa John Lwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ajiandae.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nitoe mchango wangu katika mapendekezo haya ya Mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, bila takwimu sahihi, hatuwezi kuwa na mipango mizuri na sensa ya mwaka jana 2012, naweza nikasema kwamba hatukuwa makini kwa sababu pamoja na kwamba Serikali ilijua kuna sensa na ilipaswa kujiandaa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. P. LWANJI]

kipindi cha miaka kumi iliyopita, lakini tulijionea wenyewe jinsi sensa hii ilivyokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakukuwa na maandalizi ya kutosha, Serikali ikawa haina fedha ikaziagiza Halmashajuri ndiyo ziweze kushughulikia kulipa wasimamizi na Makarani wa hiyo sensa na wakaifanya vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe Lwanji naweza nikathubutu kusema kabisa kwamba, hawakutundea haki, maeneo mengi tu watu hawakuhesabiwa na wale waliokuwa wanafanya hiyo kazi walishindwa kwa sababu hawakuwa na nyenzo za kuweza kuwasafirisha haraka pamoja na mambo mengine ya kuwawezesha na ushahidi ni kwamba wengine sasa wamekuja kulipwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unapokuwa na takwimu ambazo hazieleweki unaambiwa kwamba Jimbo lako lina watu 70,000, wakati wewe mwenyewe unapopita au unapoongea na watu unakuta watu wengine wanasema kabisa hawakuhesabiwa. Hatuwezi tukapanga mipango mizuri na hali halisi ndiyo hivyo takwimu zetu nyingi hazikukaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetuambia kwamba, tuwe tunajikita kwa masuala ya Kitaifa kwa ujumla kimipango, lakini hatuwezi kuacha kutolea mifano maeneo yetu. Kwa hiyo inabidi utuvumilie tu. Sasa unapoambiwa kwamba Mkoa wako ni wa mwisho, lakini unapowaambia kwamba toeni takwimu sahihi hupati, sasa unashindwa kuelewa, hii kengele ya umaskini inatoka wapi? Unaambiwa wewe ni maskini wa kutupwa na ndiyo wa mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hatujisikii vizuri tunapowaambia wataalam wetu toeni takwimu hizo, hawatoi, matokeo yake watu wetu na sisi wenyewe tunakata tama. Kwa hiyo, ningepomba kitengo hiki cha takwimu kiimarishwe basi ili tuweze kupata takwimu sahihi. Huwa tunapewa kijitabu kidogo kinasema Tanzania *in figures* lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. P. LWANJI]

ukikisoma hakikupi taarifa za kutosha. Kwa hiyo, nashauri Serikali ijiandae vizuri kwenye eneo hilo ili tuweze kupanga mipango iliyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelia sana hasa katika kipindi cha Bunge la Tisa kuhusu kuwekwa kwa Kiwanda cha Saruji pale Manyoni, Itigi. Sisi ndiyo tunaolisha viwanda hapa, sehemu yetu inalisha viwanda vile kwa malighafi ya *gypsum* inapelekwa Tanga, inapelekwa Mbeya na inapelekwa maeneo mengine ya nchi za Rwanda na Burundi. Sasa sisi pale tunaachiwa mashimo tu na magonjwa yanayotokana na hiyo kazi na malori yanakuja usiku na mchana yanaharibu barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumelia na ninapozungumza hili naambiwa kwamba, Serikali haijengi viwanda, lakini ukiangalia kwa undani unakuta tunanyang'anyana wawekezaji. Wawekezaji wanapokuja hapa wanaelekezwa katika maeneo ambayo wale wanaowaelekeza au wanaowahamasisha wanapenda wao wapate. Sasa kilio hiki baadhi ya watu wamenisikia, wamenisaidia, walikuja Wachina hapo wakaahidi wangerudi, lakini hawakurudi, walikuja waswahili, walikuja na wengine kutoka Zanzibar, wakaja wakaangalia *gypsum* ipo ya kutosha, lakini wanasema kwamba tatizo ni *limestone*, chokaa ndiyo haitoshi, lakini *gypsum*; miundombinu yote, barabara, reli pamoja na nishati ya umeme vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa wataalam wanakwenda mbele zaidi wanasema siyo lazima ujenge Kiwanda cha Saruji tu kwa sababu malighafi ya *gypsum* unaweza ukatengeneza *POP (Plaster of Paris)*. *POP*sasa hivi tunaagiza kutoka Iran wakati malighafi ipo hapa. Kwa hiyo, vitu kama hivi vinaumiza unapoambiwa na wewe tafuta mwekezaji. Sasa kitengo hiki cha *TIC* kipo pale, nadhani inajua maeneo gani nchi hii yawekezwe, hayaendi kwa *individuals* wanakwenda kwa maeneo, hapa tukiweka kiwanda je, Serikali au nchi itanufaika vipi. Kwa hiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. P. LWANJI]

ningeomba huu mtindo wa kunyang'anyana wawekezaji nadhani tuuache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu katika ule mpango wa *MCC*/hatukupata mradi hata mmoja na sikuona katika Mpango huu wa *MCC* // kama tuna mradi wowote. Sasa hatuwezi kunyamazia hili sualam ni lazima tuzungumze, unaambiwa wewe ni maskini, lakini inapokuja katika kugawana hiyo miradi wewe hupati. Kwa hiyo, utashi upo pale kwamba wewe uendeleo kuwa maskini mpaka mwisho wa dahari. Sasa kitu hiki ningeomba Serikali ijaribu kutuona itusaidie kwenye *MCC* // ili angalau tuweze kupata mradi unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna barabara hii ya kutoka Mkiwa, Itigi kwenda Rungwa mpaka Makongorosi, Mbeya; hakuna asiyejua umuhimu wa barabara hiyo kutoka Mbeya kuja Mkoa wa Singida. Hii ndiyo iliyotumika sana kuwasomesha watu wa maeneo ya Nyanda za Juu za Kusini, kulikuwa hakuna barabara nyingine isipokuwa hiyo ili uweze kwenda Tabora, Mwanza na hata Dar es Salaam, lakini imesahauliwa. Ni barabara nyeti, kuna rasilimali za kutosha eneo lile, lakini hakuna mikakati ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeishauri Serikali katika mpango wa *MCC* // unaokuja, basi waone uwezekano wa kuipatia fedha barabara hii iweze kujengwa kwa lami mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwamba tuna barabara inayojengwa kati ya Manyoni, Itigi na Chaya kuunganisha Tabora, mahali ambapo Serikali inastahili pongezi tunatoa. Kwa kweli nashukuru sana kwa eneo hilo. Sasa basi ielekeze nguvu zake kwenye hii barabara ninayoisema ambayo hata Rais ameona umuhimu wake ameahidi, lakini hatujaona mipango yake. Reli ya kati inaeleweka umuhimu wake, tunasikia kwamba Wachina wamekubali, wanafanya mipango ya kujenga hiyo barabara, basi itakuwa ni faraja kwetu.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. P. LWANJI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa umeme, niishukuru Serikali kwa kuja na mpango wa kuihuisha au kufanya *restructuring* ya TANESCO. Tumesikia juzi juzi hapa Waziri akisema kwamba, toka iundwe TANESCO mwaka 1964 mpaka leo haijawahi kufanyiwa mabadiliko makubwa. Kwa hiyo, inatakiwa kwanz yafanyike mabadiliko makubwa ili iendane na haja ya kuweza kusambaza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

MHE. MOSES J MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Labda nianze tu kwa kusema kwamba, siungani na Serikali kwa vipaumbele vingi ambavyo Serikali imekusudia kuvichukua na hatimaye kutekeleza shughuli mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Mpango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kupitia Mpango huu na kuweza kubaini kwamba kuna *priorities* zaidi ya ishirini, lakini bajeti yetu ya maendeleo ni kiasi gani, utakuta bado ni kidogo sana. Sasa hili tatizo la kuwa na vipaumbele vingi limekuwa tatizo la miaka nenda rudi, matokeo yake hata katika baadhi ya miradi ambayo Serikali imekuwa inaji-*commit* kwamba itatekeleza au itafanya miradi imekuwa haitekelezwi kwa maana kwamba, miradi haipelekewi fedha ili kusudi utekelezaji wa shughuli ambazo zilikusudiwa katika mipango ya bajeti zifanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nittoa mfano katika hilo. Zipo barabara nyingi ambazo Serikali ilikusudia kwa miaka, takribani nichukue miaka mitatu iliyopita, hadi leo hii, lakini hakuna hata shilingi moja ambayo imepata kupelekwa katika barabara hizo. Hapa nitoe mfano tu wa barabara ya kutoka Kidahwe kule kwetu kupita Kasulu kwenda Kibondo mpaka Nyakanazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2010/2011, zilitengwa zaidi ya shilingi bilioni sita, hakuna hata shilingi moja iliyoweza kutolewa ili barabara ile iweze kujengwa. Mwaka uliofuata mwaka 2011/2012, Serikali ikatenga zaidi ya shilingi bilioni mbili, hakuna pia hata shilingi moja iliyotolewa na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J MACHALI]

hakuna kazi yeyote ambayo imefanyika. Mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ikatenga bilioni tatu na milioni mia tano, hakuna hata shilingi moja iliyoweza kutolewa, ni miaka mitatu mfululizo. Huu mwaka tunaokwenda nao Serikali imetenga shilingi bilioni kumi kwa ujenzi wa barabara ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo robo ya kwanza ya mwaka wa Serikali imani yangu inaelekea kwisha au imekwisha. Hakuna shughuli yoyote ambayo imefanywa kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile. Tatizo nini, ukiwauliza wanakwambia ufinyu wa bajeti, makusanyo ni kidogo, tunategemea tukusanye halafu ndio tupeleke kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Serikali kwa nini mnakuwa wazito wa kupunguza vipaumbele ili kusudi muwe na vipaumbele vichache ambavyo mnaweza mkaenda kutekeleza shughuli ambazo, baadaye unapokuja kufanya *impact assessment*, unaweza ukaonesha kwamba, hapa umefanya jambo moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwashauri kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, ili kuweza kuepuka kuwa na aina ya hotuba moja, ningewashauri kwa mfano, kwenye masuala ya miradi ya barabara ambayo inahitaji fedha nyingi, hebu muanze kutenga bajeti kubwa kikanda. Labda mnaweza mkasema kwa mwaka ujao *concentration* labda kwa miradi ya ujenzi itakuwa ni *Southern Corridor*. Mwende mseme kwamba, sasa ujenzi wa barabara za lami itakuwa ni kwa ajili ya ukanda wa Mikoa ya Kusini mwa Tanzania, labda mwaka mzima mtafanya hivyo.

Mkimaliza kule, mwaka mwingine mtahamia labda *Northern Corridor*, mtakwenda labda *Western Corridor*, mtakuja *Central Corridor*; tunaweza tukajikuta kwamba sasa unapokwenda kuangalia umefanya kazi gani katika hizi *zone* utakuta kwamba imefanyika kazi kubwa, kuliko kama mnavyotwambia hesabu ya kilomita moja ya lami inacheza kati ya milioni mia sita na bilioni moja na kidogo, sasa unakuja kututengea bilioni tatu, unategemea utajenga kilomita ngapi? (Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J MACHALI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama hamwezi kukubaliana na ushauri huu na nimeona kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti, imewashauri vizuri kabisa kwamba, mwangalie na ni namna gani ambavyo mmekuwa mna-*set priorities* zenu. Punguzeni vipaumbele vyenu, tena ningewashauri kwa upande wa sekta ya miundombinu kwa Mwaka wa Fedha wa 2014/2015 mwende m-*concentrate* na maeneo kama matatu tu. Nendeni mwangalie reli, nendeni mwangalie barabara na barabara tujenge kwa kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tungeacha ubinafsi kutaka kila mmoja aonekane kwamba, amepewa kasungura kadogo; maana hapa inakuja ni kama tunafanya maamuzi ya kisiasa, mambo ambayo hayatusaidii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tatu katika suala la miundombinu, mngeangalia suala la nishati. Angalieni barabara, angalieni reli na pia tuangalie suala la nishati kwa maana ya umeme, lakini ukishatoka hapo sasa pengine *focus* ya Serikali ingekuwa ni kuangalia hasa zile sekta ambazo zina-*generate income*, zipewe *priority*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la reli tunajua kwamba, kama tunaweza ku-*invest seriously* kwenye sekta ya reli, tunaweza tukasafirisha shehena kubwa ya mzigo kutoka kwenye bandari zetu na tukaenda kwenye maeneo mengine. Kwa hiyo, sasa *focus* iwea ni kuangalia kwenye bandari zetu, tunafanya kazi gani kuhakikisha mizigo haikai kwa muda mrefu na inatoka eneo moja kwenda eneo lingine. Kwa hiyo, angalieni vipaumbele vyenu, mimi binafsi hayo ndiyo ambayo nilikuwa nataka kuzungumzia katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo la pili ni Serikali inashindwa hata kuseti mipango yake au vipaumbele vyake vizuri kwa sababu ya kukosekana kwa maadili kwa baadhi ya watendaji ndani ya Serikali yetu. Ukijaribu kupitia kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo imekuwa

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J MACHALI]

inafanywa na Serikali, ukifanya *assessment* utakuta *value for money* haipo kwenye Miradi mbalimbali, kuna uchakachujaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme tu kwamba, wakati mwingine nimepata kusema hapa na leo narudia tena, hakuna sababu ya kusema masuala ya haki za binadamu kwa watu ambao ni wahujumu wa uchumi. Leo baadhi ya Wizara mmeamuru kufanya hizo operesheni, mnapiga ng'ombe, nendeni mkatumie risasi kuwapiga wahujumu wa uchumi katika nchi hii; hapo ndio nitasema kwamba, kweli Serikali iko *serious* na kwamba, kweli tunataka tu-*move*, tutoke kwenye wimbo ambao tumekuwa tunaimba kila siku; wizi, wizi, wizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ikitokea kwa mfano, mmebaini Machali wewe ni mhujumu wa uchumi, mtangaze tu pale kwenye uwanja wa Jamhuri, Machali atanyongwa kwa risasi. Kama wewe ulikuwa ni rafiki yangu unanipenda, napigwa risasi, haki ya Mungu wengine wote kesho mtaogopa kwenda kuiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yatakuwa ndiyo maamuzi makini, siyo maamuzi magumu tu, ni maamuzi magumu na maamuzi makini. Hakuna sababu ya kuwalinda wezi wa fedha za madawa, watu wanakosa madawa huko vijijini, halafu mnasema tulinde haki za binadamu zinakataza kuweza kuwanyonga watu, kwa sababu gani? Watu wanaiba fedha, watu wanakosa madawa huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kwenye sekta ya elimu, hakuna; wadogo zetu na wakubwa zetu wanakosa fedha za mikopo katika vyuo vikuu, dada zetu wanajiuza na watoto wenu wengine, halafu kuna watu wanapiga *deal*; *integrity* imekuwa ni tatizo katika nchi hii. Ndiyo maana Serikali hata kama ungeishauri namna gani, punguzeni vipaumbele wengine watakuwa wabishi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme inawezekana, tutamsikia Waziri ambaye anashughulikia

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. M. J MACHALI]

masuala ya mipango atakapokuja ku-*wind up* atakuwa *rigid*, lakini Kamati ya Mheshimiwa Chenge, imezungumza vizuri sana juu ya kupunguza masuala ya vipaumbele, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, katika hili wamefanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni kuhusu upembuzi yakinifu umekuwa ni kichaka cha kuficha utekelezaji...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Hamad Rashid; atafuatiwa na Mheshimiwa Arfi, atafuata Mheshimiwa Engineer Mnyaa, halafu Mheshimiwa Malecela na Mheshimiwa Chiligati. Nadhani hawa wanatosha kwa leo.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na niwashukuru kwanza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Bajeti kwa kazi nzuri tuliyoifanya na nawashukuru Wabunge kwa kutupongeza kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niseme hii nidhamu ya bajeti ndiyo kwanza tatizo la msingi na nafikiri kuna haja ya kuli-*address*. Ukichukua ukurasa wa tisa wa hotuba ya Waziri wakati anafanya marejeo, wanasema wamefanikiwa kujenga kilomita 558.92 za kilomita za barabara, imepita lengo la kilomita 414. Sasa unajiuliza fedha za ziada zilipatikana wapi ambazo hazikupitishwa na Bunge hili mpaka kilomita zikazidi? Ama kulifanywa *reallocation* zikapelekwa mahali pengine fedha, je, palipokosekana fedha hizo palifanywa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema nidhamu ya bajeti kama haipo hatuwezi kwenda vizuri na mipango. Hii

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. H. R. MOHAMED]

ni kasoro moja na ni lazima tui-*address* katika mipango inayokuja. Kwa hiyo, basi katika Mipango anayoileta Waziri, la kwanza katika tathmini ni lazima aeleze kila mradi na thamani yake; hapa ameeleza miradi mingine, ametoa thamani ya fedha, mingine hakuleta. Mara ya pili alete na thamani yake ili tujue mradi huu tumeutekeleza kwa thamani ya fedha kiasi gani na fedha zimetoka wapi ili tuwe *clear* katika hilo, hili lilikuwa jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ambalo ningependa walifanye, ukichukua Kitabu cha Mpango, utakuta miradi mingine haikutekelezwa kabisa, lakini kwa mpango mwaka huu wa tatu ingekuwa imeshamalizika, lakini haijatekelezwa hata kidogo. Nafikiri katika *review* ni vizuri wakaja wakasema, katika mpango tulipanga mipango hii, lakini mradi fulani na fulani hatukuitekeleza kabisa, iko mingi humu ndani, sitaki niichambue. Hilo ni jambo la pili ambalo ningependa wali-*address* katika mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni mfumo huu wa uchumi tunaofanya unatabia kubwa sana ya kujenga tabaka la walionacho na wasionacho. Ukichukua kwa mfano, Marekani 44% ya utajiri wa Marekani unamilikiwa na 1% tu ya Wamarekani na 43% inamilikiwa na 19% ya *middle class*. 80% ya Wamarekani wanamiliki 16% tu ya utajiri wa Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huo ndio mfumo huu tulionao, ni vizuri watu wanapo *plan* katika Soko Huria waangalie hii jamii imbayo ni kubwa, maskini na yenyewe itaingiaje katika uchumi huo. Ndio maana tunazungumzia suala zima la *distribution* ya *wealth* na *power* katika nchi. Sasa tunasikitika sana tu kusikia kwamba, Watanzania hatuwezi kuingia kwenye Miradi ya Gesi na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati fulani tulikwenda mahali fulani kutaka kuwekeza, mtu mmoja akaniambia wewe Hamad, kwa nini usiende kuuza chumvi kuliko mradi huu unaotaka kufanya? Kwamba mimi sistahiki kufanya baadhi ya miradi, sasa nasema iko tabia hii tunajenga katika mawazo yetu. Lazima tuwajenge Watanzania kuweza

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. H. R. MOHAMED]

kushiriki katika uchumi vinginevyo hatutakuwa na amani tulivu; leo *Europe* unaona maandano makubwa ni kwa sababu, jamii iliyokuwa kubwa haiko katika kumiliki utajiri wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni moja, katika mipango lazima tuliangalie. Ni kwa kiasi gani Watanzania tunawasaidia na wao kushiriki katika uchumi, lakini kumiliki katika uchumi na nyenzo za kiuchumi. Hilo ni lazima tulifanye katika mipango inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la nne, ni suala la deni la Taifa. Kuna haja ya kuangalia mfumo mzima wa deni la Taifa. Kuna taarifa mbalimbali zimetoka kwenye *principles and guidelines of sovereign financial borrowings by African Countries*; hiki kitabu kinaelezea ni kwa kiasi gani na Bunge nalo linaweza kushiriki katika suala zima la mikopo na matumizi yake. Kwa sasa hivi Bunge letu halina fursa hiyo, Serikali inakopa halafu inakuja inaeleza tumekopa kiasi gani, lakini hatushiriki katika mchakato mzima. Wakati umefika Bunge kushirikishwa kikamilifu katika mikopo na matumizi yake, fedha nyingi inatumika nje ya mikopo iliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni tatizo moja kubwa sana, tuna deni kubwa la Taifa, tunalipa riba kubwa sana, lakini matumizi yake ya miradi hiyo sio miradi hasa ya kuweza kuzalisha na ikaweza kulipa madeni yenyewe. Bunge sasa ni lazima lishirikishwe katika mipango unayotugawia mwaka huu utuoneshe ni kwa kiasi gani Bunge litashiriki kama kwa kutunga Sheria au katika kanuni zetu za Bunge tuliweke, lakini ni lazima Bunge lishiriki katika kuona mikopo inayokopwa na matumizi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano, ni suala la uwekezaji katika nishati ya umeme. Ukiangalia katika mipango utakuta kwamba, tumezungumzia *STAMICO* itafanya nini, *PPP* zitakuwaje na kadhalika, lakini hakuna mradi uliotayarishwa na watu wa *PPP* wakaingia. Baya zaidi ni hata pale ambapo Serikali tayari iko kwenye miradi ya *PPP* kwa mfano *NDC*,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. H. R. MOHAMED]

wanazungumza na TANESCO zaidi ya miaka miwili kujua *tarrifs* za kiasi gani wao walipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tuna *proper planning* ingekuwa tayari imetoka, iko katika *planning* kuonekana kwamba, wewe unataka kuwekeza katika *wind, rate* zetu sisi za kununua umeme ni hizi kwa sababu, bado hatujaruhusu kuza umeme. Unataka kuwekeza katika jua *rate* katika jua ni hizi, unataka kuwekeza katika *coal, rate* yake ni hii, siyo tu unakwenda ku-*negotiate* na TANESCO miaka mitatu haimalizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake tuna miradi ya *coal*, haifanyiki, iko tu kwa sababu tu TANESCO bado hawajakubaliana juu ya viwango vya kuuziana umeme. Sasa nasema haya ni mambo ambayo yanaweza kuingizwa kwenye *plan*, mtu akija kuwekeza hapati tena usumbufu, anajua masharti yako haya na inakuwa *clear*, anaweza kuwekeza kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la sita, ni suala la *financial institutions*. Tumejitahidi kujenga taasisi za fedha, lakini bado hazijaweza kuwasaidia wananchi; taasisi zetu za fedha ukiona hata ukitazama katika mipango hii tuliyoifanya sasa hivi, kwenye *trading* watu wamekopa sana, lakini kwenye *investment* mikopo iliyokuwepo ni kidogo sana. Kama watu hawakopi kwenye *investment* uchumi hauwezi kuwa *sustainable*, hauwezi kuwa himilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tutafute *mechanism* ya *Banks* ziweze kutukopesha katika *investments* na hakuna njia ni mbili tu zilizobaki; ya kwanza ni *Investment Bank* yetu tuliyonayo iwe *highly capitalised*, iwe na fedha za kutosha. *TIB* tumepitisha hapa katika Bunge mara chungu nzima itapewa *50 million* au ngapi, lakini ukienda kuwauliza pesa zilizopelekwa ni chache sana. Kwa hiyo, tunahitaji kuhakikisha kabisa *TIB* kama *TIB* inaimarishwa, lakini na benki zinazoanzishwa hivi sasa kama vile za *Agriculture* na kadhalika, bado zinafuata masharti yale yale yaliyoko *Central Bank*.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. H. R. MOHAMED]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, *Planning Commission* na wengine wote wanahitaji kukaa na *Central Bank* kuangalia Sheria zinazotawala *Central Bank* juu ya mabenzi katika kukopesha na yale masharti yaliyopo; *the Central Bank* masharti yake yanasababisha mabenzi yawe na riba kubwa. Leo sehemu hizi ndogo ndogo, hizi *NGOs* zinakopa kwenye mabenzi kwa 23%, hivi wataweza kumkopesha mwananchi wa kawaida kwa kiasi gani? Aweze kutengeneza faida na aweze kurudisha mkopo na aweze kusomesha watoto wake? Kwa hivyo bado Sheria za Fedha na mazingira ya fedha hayajawa mazuri ya kumwezesha mtu kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la saba, ni suala zima la *Human Resources*. Hapa tumezungumza juzi wenzetu wa Kenya wanatuacha na hawa nao wanatuacha, sisi wakubwa. Nikasema suala la ukubwa na udogo sio msingi, Singapore ni nchi ndogo sana, lakini ukienda Malaysia wanakwambia tunajifunza mambo yalivyo Singapore, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu, Singapore wame-*invest heavily* katika *Human Resources*. Kanchi kao kadogo, hawana rasilimali, wakasema tuwekeze katika elimu kwa nguvu zote. *Highly refined* mafuta ya kula unayapata kutoka Singapore, lakini *raw material* inatoka Malaysia. Kwa hiyo, suala la msingi hapa sio ukubwa wa nchi isipokuwa ni namna gani unatumia rasilimali zako, ndio msingi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa *speed* hii ya wenzetu wanaotuacha na tukafikiri kwa sababu tu wakubwa ndio tutabaki wakubwa, tutakuwa ukubwa wa tembo, lakini tembo anauliwa na sisimizi; akiingia kwenye sikio sisimizi anamuua tembo. Lazima tujipange vizuri katika hilo na njia ya kujipanga ni kusomesha watu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *VETA* tulifanyie kazi na *VETA* sio majengo, *VETA* ni Walimu na vifaa. Kwa nguvu sana, yaani hili tufanye *operation* kama kuna *operation* ya kufanya ni hii sio *operation* ya kuua ng'ombe, hata kidogo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. H. R. MOHAMED]

Sio *operation* ya kuua ng'ombe wala kuua binadamu ni *operation* ya kuwaandaa binadamu wakamate uchumi wao, ni *operation* ya kuandaa nchi hii lenyewe soko liwe soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna *advantage*, tuna *population* kubwa, *population* hii kama itakuwa na uwezo wa *purchasing power* ndio tunaweza kuringa, huwezi ukawa na *population* kubwa ambayo ni maskini ukafikiri ina maana, haina maana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chinese walipoona wanayo *population* kubwa walichokifanya ni kuwa-*reform* wakawa na *good purchasing power*, ndio maana walipokataliwa kuuza bidhaa zao Marekani wakasema *to hell* kwa sababu, Wachina tayari walishajengwa kuwa na uwezo; walikuwa *skilled* na walikuwa na uwezo wa kifedha. Sisi Watanzania tuko wengi kweli, tuna uwezo wa kifedha? Hamna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tumesema tu kodi ya kulipa 1,000/= imekuwa kelele. Ukienda India unakatwa 10%, nunua vocha India unakatwa 10%, *they built purchasing power of the people*. Leo hizi kelele tunazopiga zote ni umaskini tu, hakuna. Kwa hivyo, hata *mentality* ya kulipa kodi nayo ni tatizo; lile wazo tu la tulipe kodi, nalo ni tatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Sasa nimwite Mheshimiwa Arfi, atafuatiwa na Mheshimiwa Engineer Mnyaa, Mheshimiwa Anne Kilango na Mheshimiwa Chiligati.

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hoja iliyo mbele yetu hii ya Mipango. Nianze tu, juzi nilikuwa nikiangalia taarifa ya habari kwenye televisheni, nikaona Mkurugenzi mmoja wa Kampuni ya Kimarekani anagawa kaptula na mashati kwa watoto wa shule kule Mererani.

MHE. HALIMA J. MDEE: Aibu, *shame*. (Makofi)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 52 baada ya uhuru, watoto wetu wanakwenda kupanga foleni wagawiwe kaptula na shati wakati wanatokana na jamii ya wafugaji na wamezungukwa na madini ambayo hayapatikani mahali pengine popote duniani isipokuwa Mererani Tanzania. Jambo hili wengine walidhani kwamba ni la kujivunia, lakini ni aibu kwa Taifa, aibu kwa nchi yetu. Kama tuna rasilimali kiasi hicho tunashindwa kuzisimamia, tunashindwa kukusanya kodi ili tuweze kuwanunulia watoto wetu mashati na kaptura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote ni kwa sababu Watanzania wanaishi kwa matumaini na kwa kauli za faraja. Maisha bora kwa kila Mtanzania. Kilimo kwanza na sasa matokeo makubwa sasa, ni kauli za faraja sana, ni kauli za matumaini makubwa sana. Leo ukienda kila mahali, matokeo makubwa sasa, ukienda kijijini matokeo makubwa. Sasa kauli ya kilimo kwanza wameisahau. Hii ndiyo Tanzania yetu. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia vipi kupata matokeo makubwa kama miradi haikamiliki kwa wakati. Tunatarajia vipi kupata matokeo makubwa kama fedha haipelekwi kwa wakati na kwa mtiririko kwa ajili ya kukamilisha miradi. Tunatarajia vipi kupata matokeo makubwa iwapo makusanyo ya fedha za ndani hayatoshelezi kuendesha gharama za uendeshaji wa Serikali. Kwa takribani toka nimekuwa Mbunge, ukiangalia sura ya bajeti kila mwaka wa fedha wa Serikali tumekuwa na makusanyo pungufu kuliko matumizi ya kawaida ya Serikali kwa trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima sasa tubadilike kwanza, kuwepo na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali na kupunguza gharama za Serikali kama tunahitaji kupiga hatua mbele. Lakini kwa bahati mbaya sana, sijui ni mvinyo wa aina gani tumekunywa mpaka sasa tunafikiri na tunaona fahari viongozi wetu wanasimama hapa ndani ya Bunge hili Tukufu wanasema bila ya uwekezaji hakuna maendeleo na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. A. ARFI]

ndiyo maana hata katika mpango wa matokeo makubwa sasa linaloangaliwa ni kutafuta mashamba kwa ajili ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hakuna mpango wowote ambao umemfikiria mkulima maskini wa Mpanda, mkulima maskini wa Kondo, mkulima maskini wa Liwale. Unazungumzia ni namna gani wata-secure land kwa ajili ya uwekezaji mkubwa. Ukiangalia Mpango ambao tunao haujagusa kundi kubwa la Watanzania maskini ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 70 au 80 ya Watanzania ni wakulima, lakini ukiangalia mpango haujakita sana katika kuelekeza ni namna gani watalisaidia kundi hili la wakulima maskini. Ukiangalia Mpango unaonesha ni namna gani tutawekeza katika kilimo cha umwagiliaji na hususan mashamba ya miwa na mpunga, lakini hakuna mahali popote wanazungumzia ni namna gani tunaweza kuongeza uzalishaji wa mazao yaliyozoeleka na ambayo tulikuwa tukisafirisha nje kama vile pamba, kahawa, katani, korosho, mkonge na kadhalika. Hakuna chochote kinazungumiwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mpango wa matokeo makubwa sasa unafikiria kuanzisha *scheme* 78 za umwagiliaji, ni jambo jema, ni jambo la kupongeza, lakini hizi ambazo tunazo sasa hivi tumeshindwa kuzikamilisha. *Scheme* ya umwagiliaji iliyoko katika Jimbo langu la uchaguzi la Momkulu imeanzishwa toka 2010. Leo miaka mitatu bado mradi huu haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Mkoa wa Katavi peke yake kuna *scheme* saba za umwagiliaji, iliyokamilika ni moja. Kwa hiyo, tunaweza tukaendelea kuishi kwa takwimu na maelezo mazuri yanayotolewa na Mawaziri hapa, tukadhani tunapiga hatua. Ifike sasa tuangalie kwamba mkono hujikuna pale unapofika. Tukamilishe miradi tuliyoianzisha kabla hatujaiibua miradi mipya. Miradi ya barabara

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. S. A. ARFI]

imesimama hususan miradi yote ya barabara katika Mkoa wa Tabora na Rukwa na Katavi ya ujenzi wa barabara za lami kwa sababu Makandarasi hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatarajia vipi kupata matokeo makubwa sasa kama barabara haziwezi kukamilika kwa wakati. Barabara ya kutoka Sumbawanga kwenda Kibaoni ambayo ilikuwa inatakiwa ikamilike ifikapo 2012, mpaka leo haijafika hata asilimia 40 ya ujenzi. Tatizo ni fedha, kwa hiyo, ni lazima tuangalie tutokane na zile hadaa za kisiasa. Miradi mingi ya barabara ilisainiwa kati ya mwaka 2009 na 2010 mpaka leo haijakamilika ni kwa sababu tulikuwa tunakwenda kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila afya ni tatizo, lakini ukiangalia katika eneo hili bado hatujawekeza vya kutosha kukamilisha au kuwa na wataalam wa kuweza kutosheleza. Tuna majengo ya Chuo cha Afya pale Mpanda yamekaa miaka nenda miaka rudi na hakuna mpango wowote ambao umeonesha kwamba chuo kile kinaweza kikatoa wataalam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli nayo ni matatizo, kila siku nakaa na kutafakari ninaposoma matarajio katika mpango wa matokeo makubwa sasa wa kusafirisha mizigo kutoka tani laki mbili leo mpaka tani milioni tatu ifikapo 2015. Najjuliza kwa muujiza gani? Kwa reli hii, kwa mabehewa haya kwa injini tulizonazo, ili kupata mabehewa kupata injini zinahitaji zaidi ya miezi 18. Watu wanafikiria kusafirisha tani milioni tatu ifikapo 2015. Watanzania wamechoka na hadaa. Tuje na mipango ambayo inaweza kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari. Kuna kibandari kidogo ambacho nafikiria kwa mtazamo wangu kwamba, itasaidia sana kuchochea maendeleo ni bandari ya Rushugi kule Lindi. Bandari hii ni muhimu sana kutokana na sasa tunakwenda kwenye uchumi wa gesi, ni lazima tuangalie kwamba bandari ile inajengwa sasa ili kuweza kuchochea na kuleta ufanisi katika sekta ya gesi badala ya kufikiria sasa kutawanya pesa zetu na kuzitapanya katika bandari nyingine nyingi ambazo nina mashaka nazo sana.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. SAID A. ARFI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu makusanyo ya fedha; ni lazima tutazame kwamba sasa wigo wa kodi unapanuliwa ili tuweze kukusanya pesa za kutosha na niungane sana na Mheshimiwa Jafo kwamba misamaha ya mafuta kwa makampuni ya uchimbaji wa madini sasa tuiangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa *Engineer Mnyaa*.

MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Hapa tunatekeleza Kanuni ya 94 na moja katika jambo zito ni kwamba ni kujadili, kuishauri Serikali kuhusu vyanzo vya mapato ambavyo vinaweza vikatumika katika Bajeti ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu, kipaumbele cha pili ni kilimo na katika hali ya kilimo kuna mazao ya chakula na biashara, kuna mambo ya malighafi ya viwandani, ufugaji, uvuvi na misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kuhusu uvuvi; Bunge hili ni kiasi cha miaka mitatu, minne huwa tunaishauri Serikali kuhusu uvuvi. Mheshimiwa Rais alipounda Wizara hii ya Ufugaji na Uvuvi, tukaipa jina kitoeo. Kwa kweli wengi wetu tulifurahi kwa sababu tumeshazoea katika Bajeti zote vyanzo vyote vya mapato ni kuhusu kukamuliwa hapo hapo kuhusu vinywaji, sigara na mambo mengine kama hayo, lakini vyanzo vipya ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hapa Bungeni kupitia Kambi ya Upinzani, miaka mingi iliyopita tumeshauri vyanzo vipya kupitia uvuvi. Ukanda huu wa bahari wa kilomita zaidi ya 800 kutoka Tanga mpaka Mtwara na Visiwa vya Unguja na Pemba, kuna mazao mengi sana baharini, lakini Serikali haijatilia maanani. Mazao ya baharini siyo samaki tu, kuna

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]

shells za aina mbalimbali ambazo zinatumika na kuna viwanda vinavyotengeneza kauri, Serikali haijafanya lolote katika eneo hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baharini kuna ufugaji, kuna kupatikana lulu ambapo kuna ufugaji kupitia chaza, Serikali haijafanya lolote kuhusu upande huo. Baharini kunapatikana hata hizo almasi na wapo watu wanaokuja kwa mwamvuli wa utalii, wanafanya *diving* au *snorkeling*, wanachukua vimelea fulani baharini ambavyo ni mali kuliko hiyo almasi na dhahabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinatumika katika *Pharmaceutical* kubwa za duniani ambavyo zinatengeneza dawa kuhusu maradhi ya moyo. Wanachukua kibunda kimoja hivi mkononi unatia mfukoni, watu wanaondoka na wavuvi wanawajua na kuna maeneo watalii wanaokwenda wakichukua hivyo vitu na Serikali inataarifiwa. Wavuvi wa Kiwani wametoa taarifa, wavuvi wa Pemba, Mkoani wametoa taarifa na kadhalika. Tunaibiwa baharini mwetu, Serikali haijafanya lolote upande huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ufugaji wa samaki, ufugaji wa samaki unaweza ukaipatia pato Serikali hasa la kutosha? *Aquaculture* ni ufugaji wa samaki baharini, Serikali haijafanya lolote upande huo. Sasa hivyo tukishauri hivi vyanzo vya mapato mnataka vyanzo gani? Kila siku Serikali inashughulikia mambo ya nchi kavu huku, madini, ufugaji na kila kitu, sawa, lakini *area* nyingine ambayo ina mapato makubwa, ziko nchi pato lao la Taifa zaidi ya asilimia 40 inategemea bahari na mazao ya baharini. Serikali yetu ifike mahali isikie ikishauriwa. Kama mnasema ni sikivu, basi msikie na hili eneo halijafanyiwa lolote bado ni *virgin*, kuna mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ukisikia watu wanashughulikia eneo la baharini, kuchomea nyavu wavuvi wetu wadogo wadogo. Kila ukisikia ni vikwazo, vikwazo, vikwanzo vya baharini, usivue *shells* hizi, usivue madondo. Usivue sijui kaa, ni vikwazo, vikwazo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uwezeshaji ambalo lipo katika huu Mpango uwezeshaji wa sekta binafsi, Serikali ituambie imewawezesha wavuvi wadogo wadogo kiasi gani? Tabianchi imesababisha samaki wasipatikane maeneo ya karibu, samaki wakimbilie mbali. Mvuvi gani katika hali ya umaskini wallonayo watu wa pwani atakayeweza kununua boti na nyavu za kuvulia bahari kuu, kama Serikali haikutia mkono wake. Ukanda wote wa pwani julize kuna Kiwanda gani cha Samaki. Kuna Kiwanda gani cha Kaure. Tunafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala ambalo linatutia uchungu, tumeshazungumza kwa miaka mitano iliyopita. Kuna suala hili la misamaha ya kodi na napenda nizungumzie misamaha ya kodi kuhusu Kampuni hizi za madini. Mheshimiwa Rais aliunda Tume hii ya Bomani, ikaleta ripoti yake tukapitisha maazimio hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja katika maazimio yale ni kuondoa hii misamaha ya kodi. Lakini imesomwa ripoti hapa Bungeni limechangia kuongeza maazimio, miezi miwili tu imeletwa bajeti hapa wakati wa Waziri Mkulo ikazungumzwa kwamba, makampuni yale matano makubwa yataendelea na msamaha. Kampuni mpya zitakazokuja ndiyo zitafutiwa msamaha. Mambo gani haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *resolution* ya UNnamba 1803 inazungumzia *right* ya Taifa, *Sovereignty* ya Taifa kuhusu rasilimali zake na isitoshe tu inazungumzia namna gani inatambua ule uwezo wa nchi na watu wa nchi hiyo kutumia haki ya rasilimali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe *Charter* ya *Economic Rights* ya *United Nations Assembly* ya 1974 inazungumzia *International Order* katika *Article No.2*, naomba ninukuu:

"Every State has and shall freely exercise full permanent sovereignty including position use and disposal of all its wealth, natural resources and economic activities".

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu inaogopa nini? Ikiwa *right* zote hizo tunazo, Serikali yetu inaogopa nini kuondoa hii misamaha ya kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo linalostaajabisha la kuwa kila siku tukae Bungeni, tuzungumzie misamaha ya kodi, misamaha ya kodi, misamaha ya kodi, Serikali inaogopa nini? Uwezo huu tumepewa na chombo kikubwa cha dunia cha Umoja wa Mataifa, kwa nini Serikali isichukue maamuzi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nishati, kila Mpango kuanzia mwaka 2006 mpaka leo kila siku tunasikia Kinyerezi, Kinyerezi, Kinyerezi; Kinyerezi hiyo isiyokamilika jamani, itakamilika mwaka gani? Katika mipango ya maendeleo ya *TANESCO* na mipango iliyopita 2010 ilikuwa miradi ya Kinyerezi iwe imeshamalizika. Lakini kila siku mabadiliko, mabadiliko, Wabunge na wananchi kwa jumla ikiwa kila jambo, kila mwaka haliishi, hata kama imepangiwa mpango wa kwisha, linavunja moyo. Naomba hili suala lizingatiwe, haiwezekani kila siku kutaja Kinyerezi, Kinyerezi, Kinyerezi, Kinyerezi isiyokwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango mzima wa suala la gesi. Tunategemea gesi ndiyo iwe mwokozi wa mazingira yanayoharibika katika nchi hii na katika mpango ulioko kwamba pengine kama mwaka mmoja au mmoja na nusu miwili ijayo tayari tutakuwa na gesi ya kutosha hapa Dar es Salaam na sehemu nyingine iweze kutumika katika kupikia na kuondoa au kupunguza ukataji wa miti ambayo hali ya mazingira inaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Mpango huu, gesi kufikia *stage* ya kutumika nyumbani kwa *level* kubwa kama hiyo kunahitaji mipango mrefu. Nchi zinazotumia gesi kuna mipango ya miundombinu ya vituo vya kuzimia moto. Kuna mitambo ya ku-*detect* gesi inapovujisha, inapovuja katika zile *pipeline*. Kuna mambo mengi ya kupanga, tutakuja kufanya muda gani wakati pana mwaka mmoja ujao.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. ENG. M. H. J. MNYAA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mpango wa 2014/2015 haujazungumzia kitu chochote kuhusu mambo haya. Sasa inakuwa kidogo, hii mipango yetu katika hali kama hii inatia wasiwasi mafanikio yake kwa sababu kuna elimu ya kutosha, watu wengi sana wanaogopa kutumia gesi, wanaogopa moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi kubwa ya watu hawapendi kutumia gesi. Sasa ilikuwa mipango ya kuelimisha watu na mikakati mizuri na ramani nzuri na namna gani vituo vya kuzima moto ambayo huwezi kutegemea kituo kimoja katika mji wa Dar es Salaam. Unategemea katika kila masafa kidogo uwe na kituo cha karibu pale na zile mita za ku-*detect fire* au *likage*, hiyo matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kusema tu kwa kukaa mpaka leo hatujapanga lolote na tukasema kwamba mwaka mmoja ujao au miaka miwili ijayo tutakuwa tunatumia gesi majumbani kwa kupikia tunajidanga. Ni kitu *complicated*, inafaa kutolewa elimu ya kutosha kwa raia, inafaa kuandaa wataalam wa kutosha na mambo kama hayo, lakini hamna katika Mpango huu. Haya ni ambayo Serikali iyafikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme la mwisho kwamba, katika hali ya leo kuna vitu vinaitwa *Mobile Hospitals* na hizi zimetoka, wamevumbua hapo Marekani. Si gharama kubwa, dola milioni moja tayari unapata *Mobile Hospital* zenye *equipment*, let us test zinaweza kutusaidia sana katika hali hii ya leo. Kwa hiyo, Serikali ifikirie pia katika *technology* ya leo na hali kupunguza badala ya kujenga mahospitali mengi kila pahali kila Mkoa, kuna *Mobile Hospital* hizo ambazo zinaweza kusaidia. Tufikirie mbele wakati kuna wenzetu tayari na Ghana wameshanunua tayari kama hamsini hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Spika.
(Makofi)

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

MWENYEKITI: Nashukuru. Huyu katika *SADC* ni Mwenyekiti wa *Extracting Industry*. Kule *SADC* wamefanya manufaa kwa wananchi kuhusu mambo ya madini. Kwa hiyo, ni Mwenyekiti wake, nadhani hiyo *Paper* ataitoa kwa Wajumbe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Anne Kilango, tutamalizia na Mheshimiwa Chiligati.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mungu na nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitapenda kuongelea mambo ambayo labda wenzangu hawajayaongea, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa kirefu na nisingependa kurudia yale yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza.

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie kidogo ukurasa wa sita wa kitabu cha Mheshimiwa Wassira, pale alipozungumzia ukuaji wa pato au ukuaji wa uchumi, alionesha kwamba kwa Tanzania kutoka asilimia 6.9 hadi asilimia saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukasimama tukajivuna kwamba tumesogea, lakini tujiulize je, sisi ambao ni wawakilishi wa wananchi, wengi wetu hapa tunawakilisha wananchi ambao ni wakulima, wengi wetu hapa tunawakilisha wananchi ambao wanaishi vijijini wakitegemea kilimo kama zao la chakula na kama zao la biashara. Lakini je, ukuaji huu wa uchumi kwa wakulima wanaona hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata nafasi ya kwenda Malaysia; tulipokuwa tunatoka *Airport* kuelekea mjini nikamuuliza Mheshimiwa Lulida, ile miti ni miti gani akaniambia Mmichikichi, mashamba ya michikichiki, yalivyopangwa vizuri, mashamba yalivyo mazuri, michikichi ilivyostawi. Nikamwambia Mheshimiwa Lulida hatukuja kwa ajili ya michikichi, tumekuja kwa ajili ya utafiti wa gesi, lakini

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. MALECELA]

hebu tuombe wenyeji wetu watutembeze kwenye michikichi hii, tuone wenzetu wanafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulijaribu kila njia, lakini ratiba ilikuwa imebana, hatukupata ila tukaomba tuwaulize maswali, jamani hii michikichi ni ya namna gani? Tuliokuwa nao ni mashahidi tuliambiwa michikichi hii mbegu tulitoa mahali panaitwa Kigoma. Kigoma ni wapi? Ni Afrika, lakini hawajui kama ni Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo limeniuma hilo mpaka leo, wamechukua mbegu Kigoma, Tanzania leo wao zao la michikichi linaongoza kwa *income* ya *export* kwa nchi yao. Sasa unaweza ukaona hiki kitu sio kidogo hatupeleki nguvu zetu, ubunifu wetu, uongozi wetu kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoke hapo niende mahali panapofanana na hapo, mtaniwia radhi kwa sababu nitawaudhi, naomba nianzie pale alipoishia Mheshimiwa Kombo. Baba wa Taifa katika uhai wake alipata kurudia hili neno mara nyingi kwamba, ili nchi iendelee au ili wananchi tuendelee tunahitaji vitu vine; watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu tunao mimi hapa kama Mbunge wa Jimbo nyuma yangu nina watu na wananchi; ardhi ipo; twende hapa sasa, siasa safi na uongozi bora, hapa kunagomba? *(Makofi)*

Msipige makofi! Hapa kunagomba, tuko Vyama Vingi; Vyama Vingi haina maana kwamba tupingane kwenye kuleta maendeleo ya nchi hapana, wote tuchangie kwenye mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuja kwenye uongozi, naomba nivue miwani. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote hapa ndani tuna matatizo, tuko Wabunge 357, kama sijakosea, ndani yetu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. MALECELA]

wako Mawaziri 31, Manaibu Waziri 25, kama nikikosea mnirekebeshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Wabunge sisi tujiulize, hebu kila mtu akae peke yake ashike kitabu chake cha dini aongee na Mungu, zile kura alizopewa na wananchi anafanya kazi, maana yake msikae tu mnapiga makelele? Tujulize, *at the end of the day* wewe mwenyewe jiulize hivi leo nimefanyia kazi wananchi wangu tangu asubuhi mpaka jioni. Hivi leo tangu asubuhi mpaka jioni nimefanyia kazi nchi yangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika tena nasema nina uhakika, iwapo viongozi wote wa nchi hii, sisi tulioko humu ndani, kila mtu kwenye nafasi yake, angeshika kazi, akafanya kazi, leo tusingekuwa tunalalamikia uchumi wa nchi hii kiasi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri sio wote wanaomsaidia Rais, sio wote wanamsaidia Rais wako wachapa kazi, lakini wachapakazi utakuta wanaundiwa vikao tutammalizaje, tutamwondoaje, tutammalizaje, viongozi wenzangu tuache, kazi iliyotuleta hapa ni kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Watanzania, tunakwenda kwenye uchaguzi wa 2015, Mbunge mnayemuona hafai, hachapi kazi, hawaletai maendeleo, Same Mashariki nyie ndiyo muamue, Anne Kilango hatuletei maendeleo, ondoeni, wekeni Mbunge anayefanya kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunabaki kila wakati tunasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi hapa, wewe unafanya kazi, tukienda kwenye Jimbo lako unatumikia wananchi vizuri, hapana wote tuwajibike, Serikali iwajibike, Wabunge tuliochaguliwa na wananchi tuache majungu, tuache kukaa na kusengenyana; leo lazima tumwondoe Anne Kilango, lazima asirudi, wewe utakaa uniondoe, wanaoniondoa wananchi, Anne Kilango

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. A. K. MALECELA]

haondokeki hivi hivi, watakaoamua ni wapiga kura, kama sikuwafanyia kazi wataniondoa, lakini wewe unakaa vikao, tutamuondoa je, *you are wasting your time. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu muhimu sisi wenyewe tujiulize, leo hapa na Mheshimiwa nimeshukuru umenipa nafasi, ningeondoka leo roho ingeniuma, tunafanya kazi, tujiulize tunafanya kazi? Hivi wote humu ndani 357 kila mtu tangu asubuhi mpaka jioni *sixteen hours* angefanya kazi, hii nchi ingekuwa hapa? Tunapewa kura za wananchi tunabaki kila wakati kukaa mikutano isiyo na maana, ya majungu, kutafutana, kama wewe huna uwezo wa kufanya tulia, acha wanaochapa kazi wachape kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waheshimiwa wajue kwamba, bila ya kupata viongozi bora, bila Wabunge bora, bila Madiwani bora, nchi hii itateketea tu, tutabaki kila siku tunategemea misaada kutoka nje, naomba tujirekebishe kuanzia leo. Ambaye anaona hawezi aache wale wanaoweza wafanye kazi na wananchi amueni nani aingie humu ndani, asiyefaa mtoeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Kujikosoa ndiyo huko, anachosema sio utani, kiongozi ni kila mmoja hapa, si utani. Hii tunazungumza habari ya *unemployment*, Waheshimiwa mna vijana wangapi pale, umefanya mpango gani wa kuwahudumia wananchi, hamna. Halafu kuna vitu vingine mnafanya vya hovyoy, mnapoteza muda wenu kwa kufanya mambo ya hovyoy haisaidi kitu, tuendelee. Ahsante kwa mchango wako. *(Makofi)*

MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hoja hii. Nilipokuwa nasikiliza baadhi ya hotuba ya Wabunge wenzangu na wananchi wanaotusikiliza kule, wengine wanapeleka ujumbe kana kwamba mipango iliyotangulia haijazaa matunda yoyote na hakuna kilichofanyika, ndiyo

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. Z. CHILIGATI]

picha ambayo baadhi ya hotuba zinapeleka ujumbe kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mipango iliyopita kuna mafanikio ambayo yameanza kupatikana ambayo ni lazima tuyatambue na baadaye tupange kwenda mbele. Kwa mfano, katika suala la barabara, nitatolea mfano Mkoa wangu wa Singida, miaka mitano. saba iliyopita, ulikuwa ni mkoa ambao haufikiki, *not reachable*, haufikiki, leo hii Mkoa wa Singida unaweza ukafika kwa barabara ya lami toka Dar es Salaam, Dodoma, Singida mpaka Mwanza ilikuwa haipo. Leo hivi unatoka Singida, Babati mpaka Arusha kwa lami ilikuwa haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza kuna ujenzi wa lami kutoka Manyoni – Itigi - Tabora mpaka Kigoma, ulishaanza kutekelezwa. Sasa yote haya baadhi ya watu hata hawaoni wala hawawezi wakaipongeza Serikali kwa haya ambayo yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza sasa kuona umeme vijijini kwa mara ya kwanza. Kwangu Manyoni kwa miaka mingi sana umeme ulikuwa unaishia pale Mjini Manyoni tu, leo hivi tunavyozungumza, awamu ya kwanza na awamu ya pili vitafika vijiji 35 kutoka zero. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa lazima haya mambo tuyatambue. Uchumi tumeambiwa unakua kati ya asilimia kati ya sita mpaka saba ni jambo jema, mfumko wa bei tunaambiwa umepungua sasa tuko katika asilimia sita, ni jambo jema, ni mambo ambayo lazima tuyatambue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato la wastani wa mwananchi, mwaka uliopita pato la mwananchi kwa mwaka wastani tulikuwa kwenye 869,000 sasa hivi tuko katika 1,025,000, ni mambo ambayo yanafanyika, ni lazima tuyatambue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ziko changamoto na ndiyo kazi zetu za Ubunge sasa tuishauri

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. Z. CHILIGATI]

Serikali jinsi ya kwenda mbele. Changamoto ya kwanza ni ukusanyaji wa mapato, ili Mpango huu uweze kutekelezeka, ni lazima tupate mapato ya kutekeleza huu Mpango. Miradi hii haitekelezeki kwa wakati kwa sababu ya kitu kinachoitwa ufinyu wa bajeti, ufinyu wa bajeti ni kwamba hatujakusanya kodi za kutosha. Sasa tunaishauri nini Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Wabunge wenzangu wameshauri kwamba tutazame suala la misamaha, Serikali itazame misamaha, imekuwa ni mingi mno, misamaha ya kodi inatupunguzia mapato, inapunguza uwezo wa Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo. Naomba Serikali itazame tena suala la misamaha ya kodi hasa kwa yale makampuni makubwa makubwa, sekta za madini na sekta zote ambazo zinapata msamaha kumbe pesa zile zingeweza zikafanya kazi nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali itazame jinsi ya kupanua wigo wa walipa kodi, kawigo ketu ni kadogo mno, katika watu milioni 45 nusu ondoa; baadhi yao ni wanafunzi, watoto wadogo, nusu tuliobaki tuko karibu milioni 20, lakini ambao wanatoa kodi ni milioni moja tu, haiwezekani. Hili ni eneo vilevile tunaishauri Serikali itazame jinsi gani ya kupanua wigo wa kodi ili Watanzania wengi zaidi walipe kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile sekta isiyo rasmi itazamwe, Serikali hebu undeni *Task Force* imulike sekta isiyo rasmi, sehemu kubwa wana mapato makubwa, lakini hawalipi kodi, tupanue wigo wa kodi, tupate pesa za kutosha za kutekeleza miradi yetu ambayo tumejipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile *TRA*, juzi nimemsikia Waziri Mwakyembe anasema kwamba pale Bandarini, kitengo cha Bandari wanafanya kazi saa 24, *TRA* wanafanya mpaka sijui saa kumi na mbili jioni wanakwenda kulala, mahali ambapo pana hela kiasi kile unakwendaje kulala? Unalalaje? Kwanini *TRA* wasifanye kazi saa 24 kama wanavyofanya Mamlaka ya Bandari na pale kuna pesa, ndiyo mgodi wetu wa pesa pale bandari.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. Z. CHILIGATI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vituo vya mipakani pale ambapo malori yanapitisha mizigo yanalipa ushuru pale, vituo vingi vyetu vya mpakani bado watu wanalala, wanafanya mpaka saa kumi na mbili halafu wanalala, malori yanakuwa msururu kilomita tano wanangoja waamke asubuhi, kwa nini? Haya ni maeneo ambayo tungependa Serikali iyatazame; vituo vya mipakani vifanye kazi saa 24, bandarini kazi saa 24, kwa sababu ndiyo maeneo ambayo yana mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni ukuaji wa uchumi, ni vizuri mpango wetu ujielekeze ili ukuaji wa uchumi unufaishe Watanzania wote, isiwe kwamba uchumi unakua lakini wanaotajirika ni wachache walio wengi wanabaki maskini. Matokeo yake pengo kati ya maskini na matajiri, pengo kati ya walionacho na wasionacho linakuwa kubwa, ni hatari hata kwa umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wataalam tutazame jinsi gani Mpango wetu utakavyoziwezesha rasilimali za nchi hii ziweze kutunufaisha sisi wote, tukaenda kwa pamoja, tusiweke matabaka, isiwe uchumi unakua lakini ndani ya kukua, unakuza na matabaka, haitatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako maeneo mawili ambayo kama Serikali tukiwekeza vya kutosha, hata hawa wanyonge na wenyewe tutakwenda nao, tunainua hali zao. Sekta ya kwanza ni kilimo, nashukuru imo katika kipaumbele, nashukuru imo katika ule mpango wa matokeo makubwa sasa, lakini tuongeze rasilimali, ile Benki ya Wakulima ambayo itatoa mikopo nafuu, mitaji nafuu kwa wakulima sasa tuione, maana tunaisoma kwenye maandishi, tunaisoma kwenye magazeti, tunaisoma kwenye hotuba, lakini ukienda mitaani ile benki haipo. Kwa hiyo, tungependa katika Mpango huu tunaouandaa, hiyo benki ya kumsaidia mkulima ili aweze kupata mitaji sasa tuione.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umwagiliaji; hatuwezi kuendelea na kilimo cha mvua kwani ni kilimo cha

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MHE. J. Z. CHILIGATI]

kubahatisha, kwa hiyo, katika Mpango unaokuja, Serikali hebu sasa tuwekeze vya kutosha katika miradi ya umwagiliaji ili kilimo kiwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo bahati mbaya hata katika mpango wa matokeo makubwa sasa halipo, ni sekta hii ya ardhi na nyumba. Hawa wakulima tunaosema maskini wana ardhi, si maskini kiasi hicho wanayo ardhi na duniani kote mtu mwenye ardhi anaitwa *Land Lord*, yaani ni mtu tajiri. Sasa sisi ma-*Land Lord* wetu ni malofa, ni malofa kwa sababu ule utajiri wao ili ardhi iwe mtaji hai, bado hatujapima, hatujamilikisha, hatujaiwekea mpango wa matumizi bora na ndiyo unaozaa migogoro yote. Tangu asubuhi tulikuwa tunazungumza habari za migogoro ya wafugaji ni kwa sababu ardhi yetu hatujaipima, hatujaiwekewa mpango wa matumizi bora, hatujamilikisha wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa niishauri Serikali, safari hii tuweke hela za kutosha kabisa katika kupima ardhi yetu, kuwamilikisha wakulima na wafugaji na vilevile katika kupanga matumizi bora ya ardhi. Hilo ni jambo linalotakiwa kupewa kipaumbele, tuweke hela za kutosha, tumalize hii migogoro tuliyoizungumza tangu asubuhi, lakini tuwatajirishe hawa wakulima kupitia ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupima ardhi ni gharama kubwa, ni lazima utumie picha za anga, sasa hivi tunanunua picha za anga ili kurahisisha kupima ardhi. Tulishapitisha katika Bunge hili ili tuwe na Kituo cha *Satellite* cha kupokea picha za anga, tulishapitisha hapa. Lakini Serikali ina kigugumizi gani katika jambo kubwa kama hili litakalorahisisha kupima ardhi, hatujaweka pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Bado tuna wachangiaji wengi kwa sababu leo tuliingia kwenye kazi nyingine na mkiangalia ratiba yetu tulikuwa tumepanga kwamba kesho tutaendelea, lakini baada ya kuangalia na kutafakari,

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI]

tukafikiria kwamba, haya tuliyozungumza angalau Kamati ya Bajeti na Wataalam wa Tume ya Mipango pamoja na Waziri wao waende wakatafakari namna gani wanaweza kuyaangalia vizuri.

Tutaendelea Jumatatu na pengine Mawaziri wachache itabidi wapate nafasi ku-*respond* mambo ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyazungumza, lakini tutaendelea kidogo siku ya Jumatatu.

Kanuni yetu ile ya 94(1) inasema tutazungumza kwa siku zisizozidi tano, kwa hiyo tutaangalia namna ku-*manage time* ya siku hiyo, lakini kesho, tumefikiri itumike nafasi huru zaidi watafakari, maana yake tunaweza tukasema yote ikawa tumesema tu basi. Kwa hiyo, watafakari kwenye Kamati ndogo na mambo mazito mliyosema waangalie jinsi wanavyoweza ku-*manage* mpango wenyewe.

Kwa hiyo, naomba kesho saa tano Kamati ya Bajeti na wataalam wa Tume wakutane waweze kupitia baadhi ya maeneo haya na mengine ambayo tumezungumza hapa. Kwa maana hiyo, kesho hatuna kikao isipokuwa wenye Kamati zinazohusika wataendelea, wenye semina zinazohusika kwenye Kamati waendeleo, lakini hatutakuwa na kikao rasmi za Bunge.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge...

(Hapa Mheshimiwa Spika alikumbushwa kwamba hakuwa katika mavazi rasmi na Bunge halijarudia)

MWENYEKITI: Nilifikiri nimevaa mavazi yangu kumbe siyo, kwa hiyo Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa tukae, samahani sababu ya mazoea. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema kesho kuanzia saa tano Kamati ya Bajeti pamoja na wataalam wa Tume ya Mipango watakaa kusudi waweze kutafakari na

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

[MWENYEKITI]

kuona namna gani wanaweza kuimarisha mpango ule ulivyotolewa. Kwa sababu ni imani yetu kwamba, tutakapokuja kipindi cha bajeti kusiwe na hitilafu kubwa sana za mabadiliko.

Tukiweza kutengeneza vizuri sasa hata wote wataandaa vizuri, hata watakaokuja kupanga watapanga vizuri. Kama tulivyosema tusifanye mambo kwa mazoea mabadiliko yapo ni mengi na lazima tuyaangalie, kwa hiyo, naamini pia na Serikali mtakwenda hivyo.

Kwa kweli hatukufurahishwa sana katika kipindi hiki na uwepo wa Mawaziri katika mjadala, hatukufurahishwa kabisa. *(Makofi)*

Kwa sababu ilionekana kama ni kazi ya Wizara moja, siyo, ni wote mnahusika, kwa hiyo, tunapenda kabisa hili suala msilipe nguvu kidogo, tulifanye pamoja.

Kwa hiyo, naomba nitishe shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

(Saa 1.40 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 4 Novemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)